**ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR**

| | | |
|---|---|---|
| **MHE. ZUBEIR ALI MAULID** | **-** | **SPIKA** |
| 1. Mhe. Mgeni Hassan Juma | - | Naibu Spika/ Nafasi za Wanawake |
| 2. Mhe. Mwanaasha Khamis Juma | - | Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Chukwani |
| 3. Mhe. Shehe Hamad Mattar | - | Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Mgogoni |
| 4. Mhe. Balozi Seif Ali Iddi | - | MBM/Makamu wa Pili wa Rais /Kiongozi wa Shughuli za Serikali/ Jimbo la Mahonda |
| 5. Mhe. Issa Haji Ussi (Gavu) | - | MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Chwaka |
| 6.Mhe. Haji Omar Kheri | - | MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ/ Jimbo la Tumbatu |
| 7. Mhe. Haroun Ali Suleiman | - | MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora /Jimbo la Makunduchi |
| 8. Mhe. Mohammed Aboud Mohammed | - | MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar/ Uteuzi wa Rais |
| 9. Mhe. Dkt. Khalid Salum Mohamed | - | MBM/Waziri wa Fedha na Mipango /Jimbo la Donge |
| 10. Mhe.Mahmoud Thabit Kombo | - | MBM/Waziri wa Afya/ Jimbo la Kiembesamaki |

| | | |
|---|---|---|
| 11. Mhe. Riziki Pembe Juma | - | MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali / Nafasi za Wanawake |
| 12. Mhe. Balozi Amina Salum Ali | - | MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko Zanzibar/ Uteuzi wa Rais |
| 13. Mhe. Balozi Ali Abeid Karume | - | MBM/Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji/ Uteuzi wa Rais |
| 14. Mhe. Rashid Ali Juma | - | MBM/Waziri wa Habari, Utalii na Michezo/Jimbo la Amani |
| 15. Mhe. Hamad Rashid Mohamed | - | MBM/Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Uteuzi wa Rais |
| 16. Mhe. Maudline Cyrus Castico | - | MBM/Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto/ Uteuzi wa Rais |
| 17. Mhe. Salama Aboud Talib | - | MBM/Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira/ Nafasi za Wanawake |
| 18. Mhe. Juma Ali Khatib | - | MBM/ Waziri Asiekuwa naWizara Maalum/Uteuzi wa Rais |
| 19. Mhe. Said Soud Said | - | MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/ Uteuzi wa Rais |
| 20. Mhe. Khamis Juma Mwalim | - | Naibu Waziri, Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora/ Jimbo la Pangawe |
| 21. Mhe. Mihayo Juma N'hunga | - | Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa pili wa Rais wa Zanzibar/ Jimbo la Mwera |

| | | |
|---|---|---|
| 22. Mhe. Shamata Shaame Khamis | - | Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ / Jimbo la Micheweni |
| 23. Mhe. Harusi Said Suleiman | - | Naibu Waziri wa Afya/ Jimbo la Wete |
| 24. Mhe. Mmanga Mjengo Mjawiri | - | Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali /Jimbo la Mkoani |
| 25. Mhe. Mohamed Ahmada Salum | - | Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji / Jimbo la Malindi |
| 26. Mhe. Chum Kombo Khamis | - | Naibu Waziri wa Habari, Utalii na Michezo/Nafasi za Wanawake |
| 27. Mhe. Shadya Mohamed Suleiman | - | Naibu Waziri wa Uwezeshaji,Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto/ Nafasi za Wanawake |
| 28. Mhe. Lulu Msham Abdalla | - | Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Nafasi za Wanawake |
| 29. Mhe. Juma Makungu Juma | - | Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira/ Jimbo la Kijini |
| 30. Mhe. Abdalla Ali Kombo | - | Jimbo la Mwanakwerekwe |
| 31. Mhe. Abdalla Maulid Diwani | - | Jimbo la Jang'ombe |
| 32. Mhe. Ahmada Yahya Abdulwakil | - | Uteuzi wa Rais |
| 33. Mhe. Ali Khamis Bakar | - | Jimbo la Tumbe |
| 34. Mhe. Ali Salum Haji | - | Jimbo la Kwahani |
| 35. Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata) | - | Jimbo la Kijitoupele |
| 36. Mhe. Ame Haji Ali | - | Jimbo la Nungwi |
| 37. Mhe. Amina Iddi Mabrouk | - | Nafasi za Wanawake |
| 38. Mhe. Asha Abdalla Mussa | - | Jimbo la Kiwengwa |

39. Mhe. Bahati Khamis Kombo - Jimbo la Chambani
40. Mhe. Bihindi Hamad Khamis - Nafasi za Wanawake
41. Mhe. Hamad Abdalla Rashid - Jimbo la Wawi
42. Mhe. Hamida Abdalla Issa - Nafasi za Wanawake
43. Mhe. Hamza Hassan Juma - Jimbo la Shaurimoyo
44. Mhe. Hassan Khamis Hafidh - Jimbo la Welezo
45. Mhe. Hidaya Ali Makame - Nafasi za Wanawake
46. Mhe. Hussein Ibrahim Makungu (Bhaa) - Jimbo la Mtoni
47. Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Jimbo la Paje
48. Mhe. Khadija Omar Kibano - Jimbo la Mtambwe
49. Mhe. Machano Othman Said - Jimbo la Mfenesini
50. Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi Makoti - Jimbo la Mtopepo
51. Mhe. Makame Said Juma - Jimbo la Kojani
52. Mhe. Maryam Thani Juma - Jimbo la Gando
53. Mhe. Masoud Abrahman Masoud - Jimbo la Bububu
54. Mhe. Miraji Khamis Mussa - Jimbo la Chumbuni
55. Mhe. Moh'd Mgaza Jecha - Jimbo la Mtambile
56. Mhe. Mohamed Said Mohamed - Jimbo la Mpendae
57. Mhe. Mohammedraza Hassanaali Mohamedali- Jimbo la Uzini
58. Mhe. Mtumwa Peya Yussuf - Jimbo la Bumbwini
59. Mhe. Mtumwa Suleiman Makame - Nafasi za Wanawake
60. Mhe. Mussa Ali Mussa - Jimbo la Ole
61. Mhe. Mussa Foum Mussa - Jimbo la Kiwani
62. Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa - Nafasi za Wanawake
63. Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis - Nafasi za Wanawake
64. Mhe. Dkt Mwinyihaji Makame Mwadini - Jimbo la Dimani
65. Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy- Jimbo la Chaani
66. Mhe. Nassor Salim Ali - Jimbo la Kikwajuni
67. Mhe. Omar Seif Abeid - Jimbo la Konde
68. Mhe. Panya Ali Abdalla - Nafasi za Wanawake
69. Mhe. Rashid Makame Shamsi - Jimbo la Magomeni
70. Mhe. Saada Ramadhan Mwendwa - Nafasi za Wanawake
71. Mhe. Said Omar Said - Jimbo la Wingwi
72. Mhe. Said Hassan Said - Mwanasheria Mkuu
73. Mhe. Salha Mohamed Mwinjuma - Nafasi za Wanawake
74. Mhe. Salma Mussa Bilal - Nafasi za Wanawake
75. Mhe. Shaib Said Ali - Jimbo la Chonga
76. Mhe. Simai Mohammed Said - Jimbo la Tunguu
77. Mhe. Sira Ubwa Mamboya - Uteuzi wa Rais
78. Mhe. Suleiman Makame Ali - Jimbo la Ziwani
79. Mhe. Suleiman Sarahan Said - Jimbo la Chakechake

| | | |
|---|---|---|
| 80. Mhe. Tatu Mohamed Ussi | - | Nafasi za Wanawake |
| 81. Mhe. Ussi Yahya Haji | - | Jimbo la Mkwajuni |
| 82. Mhe. Viwe Khamis Abdalla | - | Nafasi za Wanawake |
| 83. Mhe. Wanu Hafidh Ameir | - | Nafasi za Wanawake |
| 84. Mhe. Yussuf Hassan Iddi | - | Jimbo la Fuoni |
| 85. Mhe. Zaina Abdalla Salum | - | Nafasi za Wanawake |
| 86. Mhe. Zulfa Mmaka Omar | - | Nafasi za Wanawake |

Ndugu Raya Issa Msellem - Katibu wa Baraza la Wawakilishi

**Kikao cha Kumi na Mbili – Tarehe 22 Februari, 2018**

*Kikao Kilianza Saa 3:00 (asubuhi)*

**DUA**

*Mhe. Naibu Spika, (Mgeni Hassan Juma) alisoma dua*

**TAARIFA YA SPIKA**

**Mhe. Naibu Spika:** Waheshimiwa Wajumbe, Katika Kikao cha Baraza cha tarehe 13 Februari, 2018, Mhe. Omar Seif Abeid aliuliza swali la nyongeza kwa Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ linalotokana na swali la msingi Nam. 42. Sasa namuomba Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ asome jibu la swali la nyongeza lililoulizwa na Mjumbe huyo.

**Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ**: Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kutoa taarifa ya jibu la maandishi kwa Mheshimiwa Omar Seif Abeid, lililotokana na swali la nyongeza nilipokuwa nikijibu swali la msingi namba 42 kama ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, si vyema kutoa idadi halisi ya askari hata kama ni fundi pasipo na utaratibu maalum, lakini napenda kumuhakikishia Mhe. Mwakilishi kuwa wapo Askari ambao wana ujuzi katika viwango vya elimu ya "*Master Degree, First Degree, Diploma, F.T.C* na *Certificate*, na ni wa kutosha katika mahitaji ya Idara Maalum za SMZ.

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kuwasilisha.

## HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

**Mhe. Abdalla Maulid Diwani (Kny**: **Mwenyekiti wa Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti**

**Hesabu za Serikali na Mashirika ya Umma):** Mhe. Naibu Spika, naombaa kuweka Hati Mezani ya Ripoti ya Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiri Hesabu za Serikali na Mashirika ya Umma naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

## MASWALI NA MAJIBU

### Nam. 49

### Tathmini ya Mahitaji ya Watumishi wa Umma

**Mhe. Omar Seif Abeid** - Aliuliza:

Kwakuwa serikali ilifanya zoezi la ukaguzi kwa ajili ya kubaini wafanyakazi wake kwa wizara mbalimbali kwa lengo la kujiridhisha na kuweza kujua mahitaji halisi ya wafanyakazi, ambao wanahitajika kwa wizara na mashirika yake. Vilevile, wafanyakazi waliostaafu na wanaofariki kwa kila mwaka.

(a) Je, ni lini kwa mara ya mwisho serikali ilifanya ukaguzi kwa wafanyakazi wake wa serikali na mashirika.

(b) Je, ni wafanyakazi wangapi waliostaafu sambamba na waliofariki dunia kwenye wizara na mashirika hayo kutoka 2015/ 2017.

(c) Je, ni wafanyakazi wangapi walioajiriwa ili kujaza nafasi zilizowachwa wazi na watu waliostaafu na waliofariki dunia kwa kipindi cha 2015/2017.

**Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora -** Alijibu:

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Omar Seif Abeid swali lake Nam. 49 lenye kifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, kabla ya kumjibu swali lake Mhe. Omar Seif Abeid lenye Nam. 49 naomba kutoa maelezo yafuatayo:-

Mhe. Naibu Spika, ni kweli kuwa serikali ilifanya zoezi la ukaguzi kwa ajili ya kubaini wafanyakazi wake kwa wizara mbalimbali kwa lengo la kujiridhisha na kuweza kujuwa mahitaji halisi ya wafanyakazi ambao wanahitajika wizarani na mashirika yake na wapo miongoni mwa wafanyakazi wanaostaafu na ambao walofariki kwa kila mwaka.

Mhe. Naibu Spika, baada ya maelezo hayo sasa naomba kumjibu Mhe. Omar Seif Abeid swali lake lenye (a) (b) na (c) kama ifuatavyo:

a) Mhe. Naibu Spika, kwa mara ya mwisho serikali ilifanya Ukaguzi wa Wafanyakazi wake kwa Serikali na Mashirika ambayo yapo chini ya Serikali Kuu tu, yalikuwa mwaka 2016 uliofanywa na Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (*CAG*).

b) Mhe. Naibu Spika, wafanyakazi 1017 walistaafu kazi kuanzia mwaka 2015/2017 na wafanyakazi 445 walifariki dunia kutoka mwaka 2015/2017.

c) Mhe. Naibu Spika, serikali imekuwa ikizingatia fursa za ajira kulingana na mahitaji ya taasisi husika na kwamba katika kipindi cha mwaka 2015/2017 jumla ya vijana 899 wenye elimu kuanzia sekondari wameajiriwa katika wizara mbalimbali za serikali, ambapo wanawake ni 491 na wanaume ni 408 kwa lengo la kujaza nafasi zilizoachwa wazi na wafanyakazi wakiwemo waliofariki dunia na waliostaafu.

**Mhe. Omar Seif Abeid**: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kunipa ruhusa ya kumuuliza Mhe. Waziri swali dogo la nyongeza lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo. Kwa kuwa umekiri kwamba kunawafanyakazi jumla ya 1,462 kutokana na hesabu yako ambao walifariki duni na waliostaafu na kwa kuwa kwenye jibu pia umekiri kwamba umeajiri wafanyakazi 899 tofauti ya wafanyakazi 563.

a) Je, ni sababu gani ya msingi iliyofanya kwamba pamoja na kuwa hesabu yao na fedha zao za mishahara zilikuwepo na kila kitu chao kipo ikasekana kuajiriwa wakati hesabu yao ya mishahara kutoka Wizara Fedha ilikuwepo.

b) Fedha hizi za mishahara ambazo zilikuwa zikilipwa kwa ajili ya wafanyakazi hawa zilikuwa zinatumika kwa matumizi gani wakati fedha zao hawa zilikuwepo.

**Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora**: Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Omar Seif Abeid swali lake la nyongeza lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:

a) Mhe. Naibu Spika, katika utaratibu wa kuajiri ni swali ambalo huwa halifanywi mara moja kwa maana kwamba kuna taratibu zake mbalimbali sio kwa maana kwamba leo mtu amestaafu siku ya pili mtu huyu au mfanyakazi mpya aweze kuajiri kuna taratibu mbalimbali ambazo zinatakikana kupitiwa ili uwajiri mpya uweze kufanywa. Kwahivyo, nimwambie tu Mhe. Omar Seif Abeid kwamba mara tu wafanyakazi wanapostaafu au kufariki, basi taratibu huwa zinafatwa lakini huwa haziendi haraka haraka kwa maana kwamba leo wamefariki au leo wamestaafu siku ya pili aweze kuajiriwa mwengine kuna taratibu ambazo huwa zina vipengele hadi vikitimia hivyo vipengele basi serikali huwa inafanya *replacement* kwa maana kwamba kuajiri wale ambao zile nafasi ambazo ziko tupu.

b) Mhe. Naibu Spika, kuhusiana kwamba fedha hizi zinakwenda wapi nimueleze kwamba Mhe. Omar Seif Abeid fedha hizi zipo wala haziendi sehemu nyengine yeyote kwa hivyo fedha ziko salama kabisa.

**Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora**: Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri sana ya Naibu Waziri. Mhe. Naibu Spika, kiutaratibu ikitokezea dharura kama hiyo amefariki muda wa miezi mitatu fedha zile zinakuwepo, na zinawekewa *block* baadaye zile haziwezi kutoka fedha. Samahani Mhe. Naibu Spika, hali ya urefu ndio hiyo tena. Kwahiyo, fedha zile haziwezi

kutumika kwa mtu mwengine yeyote mpaka atakapoajiriwa mtu mwengine ndio fedha zile zitatumika.

**Mhe. Hamida Abdalla Issa**: Nakushukuru Mhe. Naibu Spika, kwa kuniona pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri ningependa kumuuliza swali moja la nyongeza lenye kitoto (a) na (b)

a) Kwakuwa utaratibu wa waliofariki na kustaafu lazima waende sambamba na kupatiwa mafao yao Mheshimiwa Waziri Je. kwa idadi hiyo ambayo umeitaja ni wasstafu wangapi na waliofariki wangapi walipatiwa haki zao baada ya kukutwa na aidha kufariki ama kustaafu kwa kipindi hicho.

b) Ni kiasi gani serikali ilitumia kwa wastaafu na waliofariki katika mwaka 2015/2017 ahsante.

**Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora**: Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Hamida Abdalla Issa swali lake la nyongeza lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo. Mhe. Naibu Spika, kiasi ambacho kilichotumiwa na serikali kwa sasa siwezi kukielewa lakini nimjulishe tu kwamba nimjibu swali hilo kwa maandishi.

**Mhe. Naibu Spika:** Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora, maswali yote yanahitaji data.

**Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora:** Mhe. Naibu Spika, nirejee kusema tena kama unavyoelewa kwamba maswali ya data yanahitaji *detail* yanahitaji uhakika zaidi kwa hivyo narejea

kusema kwamba swali lake hilo lenye (a) na (b) Mhe. Hamida Abdalla Issa nitamjibu kwa maandishi ili apate data zilokuwa sahihi zaidi

**Mhe. Yussuf Hassan Iddi**: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwa kwa kunipa nami fursa ya kuuliza swali dogo tu la nyongeza kutokana na hali ya Mheshimiwa kidogo si nzuri. Je hadi sasa hivi serikali kuu inawafanyakazi wangapi.

**Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora**: Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mheshimiwa Yussuf Hassn Iddi swali lake la nyongeza ambae anataka kujuwa idadi ya watumishi waliokuweko katika Serikali Kuu.

Mhe. Naibu Spika, ni vyema tukaelewa kwamba idadi inatofautiana siku hadi siku yaani idadi inaongezeka toka siku hadi siku lakini hadi hivi sasa hivi kwa maana kwamba kutoka Januari, 2018 tunaidadi ya watumishi katika Serikali Kuu 40,110.

**Nam. 9**

**Upanuzi wa Ofisi ya Kamisheni ya Ardhi Pemba**

**Mhe. Omar Seif Abeid** - Aliuliza:

Kaskazini mwa Ofisi ya Kamisheni ya Ardhi Pemba, kuna kiwanja cha mtu binafsi ambacho bado hajakiendeleza. Kutokana na ufinyu wa Ofisi ya Kamisheni, kuna haja ya kujenga Ofisi nyengine itakayokidhi haja.

(a) Je, wizara ina mpango wa kufanya makubaliano na mtu huyo, ili eneo hilo ipatiwe Kamisheni ya Ardhi Pemba na waweze kujenga ofisi ambayo

itakidhi mahitaji na kutatua tatizo linaloikabili kamisheni hiyo kwa hivi sasa.

(b) Je, wizara ina mpango gani wa kuliboresha jengo la ofisi hiyo kwa Pemba na kulifanyia marekebisho kwa ujenzi wa vyoo na uzio.

**Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira** - Alijibu:

Mhe. Naibu Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Omar Seif Abeid swali lake Nam. 9 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Naibu Spika, ni kweli kuwa Kaskazini mwa Ofisi ya Kamisheni ya Ardhi Pemba ipo nafasi ambayo inayoweza kutumiwa kwa upanuzi wa jengo la ofisi. Wizara yangu kupitia Kamisheni ya Ardhi imeshafanya uhakiki wa awali wa namna ya kulitumia eneo hilo na hivi sasa imo katika mashauriano ya kiufundi yatakayotoa picha ya ujenzi utakaofaa katia sehemu hiyo pamoja na kuonesha mustakbal wa maeneo ya majirani (ikiwemo njia) ambayo yanaweza kuathirika kutokana na ujenzi utakaofanywa katika eneo hilo. Baada ya hatua hiyo, kamisheni itakaa pamoja na kila mtowaji wa kiwanja atakaeonekana ataathirika na kuanzishwa kwa ujenzi wa ofisi katika eneo hilo, ili liweze kutumika bila ya matatizo.

(b) Mhe. Naibu Spika, kwa hatua za awali, jengo hilo linafanyiwa matengenezo madogo madogo yakiwemo ya vyoo kwa kutumia sehemu ya fedha zilizotengwa katika bajeti. Kwa upande wa uzio

makisio yameshafanyika na yatawasilishwa serikalini kwa mazingatio.

**Mhe. Omar Seif Abeid**: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kunipa ruhusa ya kumuuliza Mhe. Waziri swali la nyongeza. Kwakweli, niliuliza kiwanja cha Kaskazini sijauliza watu wangapi na sijuwi watu wangapi wamepewa Hati Miliki pale, lakini ninachokiulizia ni kiwanja cha kaskazini cha pale.

a) Je, ni wamiliki wangapi ni watu wangapi wenye viwanja kaskazini ya jengo lile pale Chake Chake ambao wanahitajika kuhamishwa na kupewa maeneo mengine, ili ipishwe ile nafasi wizara ile ipate kujenga jengo la kisasa litakalokidhi.

b) Umesema ukarabati mdogo mdogo. Je, haoni kwamba jengo lile kwa sasa hivi linahitaji ukarabati mdogo mdogo pamoja na matengenezo ya kina, ili kulirejesha kwenye hali yake liweze kutumika vizuri na kwa muda mrefu.

**Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira**: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Omar Seif Abeid swali lake la nyongeza kama ifuatavyo. Kama atazingatia vizuri jawabu langu la kwanza nilisema tumekubaliana kwamba kaskazini kipo kiwanja na tayari kwa mara ya kwanza tumefanya mazungumzo na muhusika lakini pia si yeye tu kwa viwanja vyote vile ambavyo vitaathirika kwa njia moja au nyengine kutokana na ujenzi huo tutakaanao na sababu za kukaa nao.

Lakini kama ulivyokuwa umeuliza swali lako ni kwamba matengenezo yanafanyikaje lakini pia hatuoni umuhimu wa kuliboresha ndio maana tukasema tunanzumza na hawa baada ya

kuzungumza na hawa tuongeze ofisi kwa hiyo katika kuongeza ofisi maanaake tumejumuisha matengnenezo makubwa ambayo wewe unayaona lakini kwa sasa tunafanya hivi hasa kwenye vyoo na vyoo tumakamilisha matengenezo yake.

**Nam. 73**

**Ongezeko la Watu wenye Ugonjwa wa Akili**

**Mhe. Simai Mohammed Said** - Aliuliza:

Kwakuwa, kumekuwa na ongezeko la watu wenye ugonjwa wa akili kutembea huru bila ya uangalizi na huduma za hospitali.

(a) Ni kwanini watu hawa hawapatiwi msaada wa huduma za afya.

(b) Ni utaratibu gani serikali inaoutumia kuwalipa fidia au hasara wanayoipata wananchi pale panapotokea uharibufu unaosababishwa na wagonjwa hawa wakati wakitembea huru.

**Mhe. Naibu Waziri wa Afya** - Alijibu:

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Simai Mohammed Said swali lake Nam 73 lenye kifungu (a) na b) kwa pamoja kama hivi ifuatavyo:

Mhe. Naibu Spika, jukumu la Wizara ya Afya kwa wagonjwa wa maradhi ya akili ni kutoa huduma za afya zipasavyo kwa wagonjwa hao, pamoja na ushauri na elimu kwa familia za wagonjwa wanaowafikisha hospitali inayohusika na maradhi hayo. Hivyo, jamaa au familia zinawajibu wa kuwapeleka wagonjwa wa akili hospitali, ili kupatiwa huduma hizo ambazo

kwa mgonjwa siyo msaada bali ana haki ya kupatia huduma na matibabu kwa mujibu wa maradhi yake.

Mhe. Naibu Spika, Wizara ya Afya haina mamlaka ya kisheria ya kuwakamata wanaozurura ovyo barabarani iwe wenye maradhi ya akili au wengineo na kwa wale wanaopelekwa katika Hospitali ya Kidongochekundu yaani, Hospitali ya Wagonjwa wa Akili kwa kuhusishwa na maradhi hayo hupokelewa, hupimwa na wakithibitishwa kuwa wana matatizo ya akili ndipo huwekwa chini ya uangalizi wa hospitali na kupatiwa huduma za afya.

Mhe. Naibu Spika, kuhusu suala la utaratibu gani unatumika unaotumika kuwalipa fidia au hasara wanayoipata wananchi unapotokea uharibifu wa makusudi unaosababishwa na wagonjwa hawa wa akili akitembea huru, ni kwamba wizara yangu haina utaratibu wowote wa kulipa fidia kwa uharibifu unaofanywa na wagonjwa hao wale haihusiki na fidia ama uchunguzi wa hasara ya aina yoyote ile inayosababishwa na mgonjwa wa akili aliyenje ya eneo husika linalowahifadhi wagonjwa hao chini ya Sheria ya Afya ya Akili ya Zanzibar *Act No*. 1 ya mwaka 2001. Ahsante.

**Mhe. Simai Mohammed Said:** Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri ningependa nimuulize swali dogo la nyongeza lenye vingu (a) na (b).

a) Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inauongozi kutoka Shehia, Wilaya, Mkoa, mpaka unafika juu katika *level* ya Mawaziri pamoja na uongozi mwengine unaofuata. Ni kwa nini wizara husika imeshindwa kuwatafuta au kuwasaka ili kuweza kuwatambua watu hawa wenye ugonjwa huu, ili kuondosha kadhia hii au kero katika jamii hasa katika maeneo ya Mkoa wa Mjini pamoja na Mkoa wa Kaskazini.

b) Wagonjwa hao wamekuwa mara nyingi wakipelekwa katika maeneo ya Hospitali ya Kidogongochekundu au maeneo mengine, lakini muda si muda kule kutokana na ukosefu wa matibabu yanayostahiki unakuta tena wanarudi hadharani au mitaani na kupelekea familia kushindwa kuwahudumia. Kwanini, serikali haiangalii mambo haya kwa jicho la huruma, ili kuweza kuwasaidia wananchi. Ahsante sana.

**Mhe. Naibu Waziri wa Afya:** Ahsante Mhe. Naibu Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza lenye (a) na (b) kama ifuatavyo.

a) Mhe. Naibu Spika, wizara yangu haihusiki na kuwatafuta wagonjwa wa maradhi yoyote majumbani mwao, isipokuwa tunapobaini panamripuko wa maradhi fulani wizara inaunda kambi maalum ya kitengo kile ambacho kinahusika na maradhi yale na kutafuta wagonjwa wale walipo, ili kudhibiti maradhi yale yasiongezeke. Lakini maradhi ya ugonjwa wa akili ni maradhi ya kawaida, wanapaswa wahusika wazee au familia wenye wagonjwa wenye matatizo hayo wajali wao kwanza majumbani kwao kuumwa au kadhia ile aloipata kijana wake ili waripoti nae katika hospitali zetu tuweze kumpatia matibabu. Kama tutafanya kuwatafuta kila wagonjwa wa akili mitaani wanaoripuka, wanaopiga makelele, wanaotembea, wanaodhurura, sio wagonjwa wa akili wote wengine ni wagonjwa lakini hawana ukosefu wa akili, wanasababisha matato wao wenyewe kwa mabangi kwa ulevi, kwa matatizo kama hayo.

b) Mhe. Naibu Spika, wanaorudi majumbani mwao ambao wameshahifadhiwa katika Hospitali yetu ya Kidongochekundu au hospitali yoyote iliyopo na kupatiwa

matibabu, wanaorudi majumbe mwao ni wale ambao wameshapona na ikitokea kukimbia bila ya kupona basi wizara inawasiliana na chombo husika, ili kutafuta mgonjwa yule na kurudishwa katika hospitali. Pia inawasiliana na wazee au familia, ili kutafutwa mgonjwa yule na kurudishwa hospitali kupatia matibabu yanayostahili.

Mhe. Naibu Spika, kwa sasa tunazo dawa kidogo za kusaidia ili kuwadhibiti pale, tunahuduma nzuri za kuweza kuwadhibiti kwa hivyo si rahisi kutokea kuripuka na kutoka bila ya usimamizi mzuri. Napenda nikueleze pia kuna wale wanaopelekwa pale hawana maradhi ya akili lakini mabangi, wamefyetuka kutokana na unga, wamefyetuka kwa mambo mbalimbali, mara nyengine wale tunashindwa kuwadhibiti. Ahsante.

**Mhe. Suleiman Sarahan Said:** Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema mwenye kurehemu, aliyeumba mbingu na ardhi na vilivyomo vyote.

Mhe. Naibu Spika, nampongeza sana Naibu Waziri wa majibu yake lakini nina swali lenye vifungu (a) na (b).

(a) Kwakuwa, mgonjwa wa akili ni mgonjwa hatari wala yule si mtu mzururaji, na wazazi au familia inawezekana ama mtu yule hana au familia yake haimuwezi. Je, ni nani muhusika kama siyo Wizara ya Afya wa kuweza kumchukua mgonjwa yule na kumpeleka maeneo ambayo yanahusika wakati yule ni mgonjwa.

(b) Kwakuwa, yeye ndiye mtabibu au ndiye anayetibu ameshawahi kuungana na sekta yoyote inayohusika, ili

kuwapitia wagonjwa wote waliokuwepo barabarani kwamba hawa wanafaa kutembea au hawafai wachukuliwe ndani.

**Mhe. Naibu Waziri wa Afya:** Ahsante Mhe. Naibu Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake (a) na (b) kama ifuatavyo:

a) Mhe. Naibu Spika, anauliza ni nani muhusika kwa vyovyote vile serikali yetu inamipango maalum ya uongozi tuna kuanzia sheha, kwa hiyo kwa vyovyote yule anayezurura mitaani au vipi kwa njia moja au nyengine atakuwa ameingia katika mkondo wa serikali wa uongozi ndani ya nchi.

   Aidha, atakuwa anatoka katika shehia fulani, anatoka katika kijiji fulani, anatoka katika familia fulani, haiwezekani akosa mambo yote, akose familia, akose kijiji, lakini pia hata akose sheha. Ule mtaa tu ambao anapenda kutembea tembea na kufanya makero pia ni ule ni mtaa ambao sheha yupo na anaweza akaiona kadhia ile, Wajumbe wa Sheha wapo wanaweza wakaiona kadhia ile na wakaripoti katika vyombo vinavyohusika, wakamkamata na kumleta ili kupatiwa matibabu.

b) Naomba nirudia kusema tena wizara yangu haina jukumu la kumfuata na kumkamata barabarani hilo ni jukumu la vyombo vinavyohusika.

Kuhusu suala pili naomba arudie kidogo swali la pili limenipita.

**Mhe. Suleiman Sarahan Said:** Nashukuru sana Mhe. Naibu Spika, na mimi pia nafurahi sana kwa majibu ya Mhe. Naibu

Waziri. Kwasababu yeye ndiye mtabibu au anayetibu wagonjwa katika serikali yetu au katika nchi yetu ikiwa ni Wizara ya Afya. Je, katika hiyo sekta ambayo ndiyo inayofanya kazi ya kuwachukua hao wagonjwa wa akili na kuwapeka katika sekta maalum ambayo wanahifadhiwa kwa ajili hiyo.

Mhe. Naibu Spika, sasa yeye kama mshauri au mtabibu katika suala hili ameshawapitia wagonjwa ambao wanatembea barabarani na hiyo sekta nyengine. Kwasababu sekta wanaingiliana kuna *ZRB* inaingiliana na polisi, yeye ameshawahi kuchukua juhudi za kuwapatia wagonjwa wanaotembea barabarani wakaweza kuwapima na kuwatizama kwamba hawa wanaweza kutembea na hawa hawafai wachukuliwe.

**Mhe. Naibu Waziri wa Afya:** Mhe. Naibu Spika, naomba kumjibu swali (b) Mhe. Mwakilishi kama ifuatavyo. Mhe. Naibu Spika, hilo nalichukua kama shauri kwasababu halijawahi kufanyika. Lakini tumeshawahi wizara kwetu kuletewa malalamiko mbalimbali na tukatoa ushauri kwa wahusika ambao walileta malalamiko kuhusu uzururaji na utembeaji wa wagonjwa ambao hawana akili, afanye nini ili waweze kuwadhibiti na baadae watuletee tuweze kutoa matibabu nakuwaruhusu. *(Makofi)*

**Mhe. Hamad Abdalla Rashid:** Mhe. Naibu Spika, na mimi naomba kuuliza swali dogo la nyongeza lenye vifungu (a) na (b) kama inavyofuata:

Kabla ya kuuliza swali kwanza namuomba Naibu Waziri wa Afya afute ule usemi wake kwamba ni ugonjwa wa makusudi ugojwa wa akili pengine ukitumia pombe au ukitumia sigara. Kwa mujibu wa *definition* ya kimataifa ugonjwa wa akili au binaadamu yeyote hakuna aliyekamilika. *(Makofi)*

a) Mhe. Naibu Spika, sasa naomba kumuliza Mhe. Naibu Waziri, kwa kuwa magojwa ya akili sasa hivi sehemu zetu ni mengi na lengo la serikali ni kuhakikisha inawapa huduma wagonjwa wa aina zote ni kwa nini Wizara yake Wizara yake haina hospitali ya wagonjwa wa akili kisiwani Pemba.

b) Kwakuwa, Pemba kulikuwa kuna utaratibu kabisa wa kupelekwa mtaalamu wa magonjwa ya akili kwa sababu serikali ilikuwa nia nzuri na ina nia nzuri ya hiyo, ni kwa nini utaratibu ule umefutika sasa kiasi kwamba Pemba kuna wauguzi wa magonjwa ya akili lakini mtaalamu wa magonjwa ya akili hakuna wala hospitali ya akili hakuna. Kwa sababu gani na lini wataijenga Hospitali ya Wagonjwa wa Akili Pemba. *(Makofi)*

**Mhe. Naibu Waziri wa Afya:** Ahsante Mhe. Naibu Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake (a) na (b) kama ifuatavyo:

a) Mhe. Naibu Spika, naomba radhi Baraza kama mmeelewa hivyo. Nililokusudia kulizungumza miye ni kwamba wengine huwa siyo wagonjwa wa akili ni wale ambao wanachemsha akili zao kwa unga, madawa ya kulevya, pamoja na mabangi. Hivyo ndivyo nilivyokusudia, naomba radhi kama Baraza limeelewa vyengine na naomba niondoshe usemi ambao mmeuelewa.

b) Pemba kwa nini hakuna Hospitali ya Wagonjwa hawa wa Akili. Napenda nimthibitishie Mhe. Mwakilishi kwamba Pemba tunayo Hospitali ya Wagonjwa wa Akili iko wodi maalum ambayo ipo katika Hospitali ya Wete, nyuma ya jengo la *Maternity* jipya ubavuni kwenye jumba hilo, pembeni kuna *incinerator* mpya hapo ipo wodi maalum ya

wagonjwa wa akili na daktari wanaohusika na maradhi hayo pia wapo na wanaendelea kutoa matibabu. *(Makofi)*

**Nam. 62**

**Ununuzi wa Meli za Kisasa**

**Mhe. Suleiman Sarahani Said -** Aliuliza:

Serikali inastahiki pongezi kwa kununua meli za kisasa *"digital na electronic".* Hatahivyo, kumekuwa na matatizo ya kiufundi pale meli hizo zinapoharibika ambapo hutafuta mafundi.

(a) Je, tuna mafundi wangapi wa fani ya *"Electronic"* katika Shirika la Meli na wangapi waliokwenda kusoma.

(b) Nini mpango wa serikali wa kuwasomesha wafanyakazi wa meli wa kozi zote za Meli.

**Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji -** Alijibu:

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 62 lenye vipengele (a) na (b) kama ifuatavyo:-

*(a)* Mhe. Naibu Spika, hadi hivi sasa Shirika la Meli halina fundi au mtaalamu alieajiriwa na shirika katika fani ya *electronic.*

*(b)* Katika kukabiliana na changamoto hii Serikali ya Mapinduzi imekubaliana na Kampuni ya *Dayanesh Shipyard* inayotarajiwa kujenga meli mpya ya mafuta ya Serikali kuwapatia mafunzo wataalamu wazalendo katika

fani zote za meli hiyo ikiwa ni sehemu ya Mkataba wa Ujenzi wa Meli hiyo.

Vilevile utaratibu wa ajira za Sekta ya Baharini, mfanyakazi yoyote hawezi kuajiriwa mpaka awe amepata mafunzo na kuhitimu katika fani aliyoajiriwa. Aidha, wafanyakazi hawa wanapatiwa mafunzo ya mara kwa mara kulingana na matakwa ya Shirika la *IMO* kulingana na mabadiliko yanayojitokeza kwa wakati husika.

**Mhe. Suleiman Sarahan Said:** Nashukuru sana Mhe. Naibu Spika, nafurahi sana na majibu ya Waziri lakini kuna swali la nyongeza.

Kwakuwa, meli yetu kwa jitihada za Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Ali Mohamed Shein kwa dhamira yake ya makusudi, ili kuondoa tatizo la usafiri katika visiwa vya Unguja na Pemba ilikuwa ni dhamira njema na meli ya kisasa, lakini kutokana na meli ile kwamba ni *full electronic*, kila kitu na sisi kama wataalamu wetu wa ndani hatuna mtaalamu wa *electronic*.

(a) Je, serikali ina mpango wa kumuajiri mtu ambaye anafani ile ili kuiokoa meli hii.

(b) Tunamifano kwamba kulikuwa na meli ya Sepidee ambayo ilikuwepo hapa ilitumika zaidi ya miaka 10 kwenda mbele ambayo ilikuwa ina wataalamu katika meli ile ya nnje, wakakaa nayo kwa muda wote huu lakini ilionesha nia kwamba lile neno la utaalamu lingesaidia je, hatuoni kwamba kuoiendesha meli ile bila ya utaalamu ni kuiuwa.

**Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji:** Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako napenda kuchukua nafasi hii kumjibu tena Mheshimiwa Mwakilishi swali lake la (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:

Mhe. Naibu Spika, kama nivyosema mwanzo ni kweli tumekiri tatizo hilo na hivi sasa tayari tumeshawapeleka vijana wetu kwa ajili ya kusomea kazi hiyo ya *electronic*. Kama unavyojua katika masomo haya wanahitajika vijana ambao wamepasi katika masomo ya hali ya juu. Tumeshafanya hiyo kazi lakini wakati huwo huwo sisi tunatoa nafasi kwa sababu tumeshatangaza nafasi kama hiyo iwapo atatokea kijana mwenye sifa basi tupo tayari kumuajiri hata kama anatoke Sepidee wapo. Ahsante sana Mhe. Naibu Spika.

**Mhe. Amina Iddi Mabrouk:** Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mhe. Naibu Spika, kwanza nichukue nafasi hii ya dhati kabisa kumpongeza Mhe. Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa nia yake nzuri sana ya kununua meli hii ili kuhakikisha kwamba wananchi wa Zanzibar wanaondokana na usumbufu wa tatizo hili la usafiri. Meli hii toka imenunuliwa hata miaka mitano haijafika. Pia meli hii tokea imenunuliwa inaharibika siku hadi siku, leo kifaa hichi, kesho kifaa hichi.

(a) Je, Mhe. Naibu Spika, nini kauli ya serikali katika hili.

(b) Kampuni hii tunasikia iliyotuuzia meli hii ni Kampuni ya *Daewood* lakini sasa hivi haifanyi kazi wala haipo. Je, serikali inaweza kutuhakikishia suala hili.

**Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji:** Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako napenda kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

(a) Mhe. Naibu Spika, kwanza nataka kumuhakikishia kwamba vyombo vyote vya *electronic* kuharibika ni kawaida si meli ya mwanzo kuharibika, *Azam Sealink II* imeharibika. Meli hii tokea ije imeharibika mara tatu, imeharibika mwanzo mwanzo tena kifaa tu kilikuwa kimechanganyika cha *electronic model* hakikuchukua hata dola elfu tatu. Mara ya pili iliharibika Septemba injini moja na hiyo ikatengenezwa na mara ya tatu imeharibika hivi karibuni. Kwahivyo, bado hii meli ni meli nzima na madhubutu na sisi tunaamini kwamba hizi ni hitilafu za kiinjinia kinaweza kukikuta chombo chochote hata gari unaweza ukanunua gari leo ikaharibika siku ya pili yake na hizo *default* zinatokezea.

(b) Kuhusu Kampuni ya *Daewood* kama ipo au haipo Mhe. Naibu Spika, hilo siwezi kulijibu kwasababu siyo swali linalohusiana na swali mama. Ahsante sana Mhe. Naibu Spika.

**Mhe. Naibu Spika:** Mhe. Naibu Waziri hilo swali linahusiana sana na hilo ambalo umelijibu.
Kama huwezi kulijibu sasa hivi tuahidi kama utalijibu. *(Makofi)*

**Mhe. Waziri Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais:** Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kuongeza majibu ya nyongeza yaliyojibiwa na Mhe. Naibu Waziri, kwanza nichukue fursa hii kumpongeza sana kwa majibu yake mazuri.

Mhe. Naibu Spika, kwa sababu Mhe. Mjumbe alitaka kujua Kampuni ya *Daewood* ipo au haipo, na kwasababu amelileta

ghafla hapa basi serikali ilichukue ikalifanyie utafiti ili majibu ya kina yaje hapa. Naibu Spika, nakushukuru. *(Makofi)*

**Mhe. Ali Salum Haji:** Ahsante Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri na mimi nilikuwa nina swali dogo tu la nyongeza lenye kifungu (a) na (b).

a) Mimi nilitaka kujua kwa kina Mhe. Naibu Spika, nipate maelezo ya kina kilichoharibika sasa hivi cha meli yetu ni *electronic system* au *engeene machine*.

b) Hilo tatizo lilojitokeza la maharibiko kama ni *electronic system* au *engeene machine* hicho kilichoharibika kinagharimu kiasi gani cha gharama ambazo zinaweza kurejesha meli yetu katika hali ya uzima.

**Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji:** Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako napenda kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:

Kama nilivyosema mwanzo watakuja wakaguzi wetu wa kimataifa Kampuni ya *Lloyd* ile kuja kuangalia nini kilichoharibika kama *engine* au *electronic* au kitu chochote, baada ya hapo sasa kama alivyosema jana Mhe. Waziri wangu tutatoa taarifa ni kitu gani kilichoharibika na matumizi yake katika kutengeneza kifaa hicho nakuombeni sana mustahamili na sisi tunaimani kubwa kabisa serikali haitoficha yoyote katika hili itatowa taarifa za uwazi na ukweli.

Ahsante sana Mhe. Naibu Spika.

**Nam. 63**

**Usafiri wa Uhakika wa Pemba – Tanga**

**Mhe. Suleiman Sarahani Said -** Aliuliza:

Pamoja na jitihada za serikali katika kupatikana kwa usafiri wa kisasa, bado kuna tatizo kwa safari za Pemba – Tanga, tatizo linalopelekea watu kupanda vyombo visivyo salama na pia kuikosesha serikali mapato na kuzidi shughuli za magendo.

a) Je, serikali ina mpango gani wa usafiri wa Tanga - Pemba - Tanga.

b) Kwa hali hii inayoendelea ya usafiri wa Pemba – Tanga, serikali imechukua hatua gani za dharura.

c) Je, hatuoni kama pasipokuwa na usafiri wa uhakika ndio tumehakikisha majahazi kubeba abiria na ni hatari.

**Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji -** Alijibu:
Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji napenda kuchukua nafasi hii kumjibu Mhe. Suleiman Sarahan Said Mwakilishi wa Wananchi Jimbo la Chake Chake suala lake Nam. 63 lenye vipengele (a), (b) na (c) nambari 63 kama ifuatavyo:

a) Mhe. Naibu Spika, kwa muda mrefu sasa meli ya *Azam Sealink II* imekuwa ikitoa huduma za usafiri baina ya Pemba-Tanga. Kwa bahati mbaya nayo meli hiyo imepata hitilafu ya *engine* na hivyo usafiri umesita kwa muda.

   Serikali kupitia Mamlaka ya Usafiri Baharini (ZMA) imekuwa ikizungumza na Kampuni ya *Azam Marine* wamiliki wa meli hiyo ili kumaliza tatizo linaloikabili meli hiyo kwa haraka

kadri iwezekanavyo lakini bado halijaweza kufikia hatua yoyote.

Pamoja na jitihada hizo, Serikali inaendelea kuhamasisha wawekezaji kuwekeza katika eneo hilo. Wapo wawekezaji ambao wamejitokeza na tayari wameanza kufanya upembuzi yakinifu kuona uwezekano wa kuwekeza katika sekta hiyo.

b) Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa meli ya Mapinduzi II haiwezi kuingia katika bandari ya Tanga kutokana na kina kidogo cha maji kilichopo katika bandari ya Tanga, Serikali imekuwa ikizungumza na Kampuni ya *Azam Marine* kuharakisha matengenezo ya meli *Azam Sealink II*, ili huduma ya usafiri katika eneo hilo irejee haraka sana lakini kama nilivyosema mwanzo bado *Azam Sealink II* hajatengenea.

Pamoja na hayo yote na majibu niliyoyatoa ya swali (a), *ZMA* kwa niaba ya Serikali inaendelea na mazungumzo na wawekezaji kutoa huduma ya usafiri wa baharini katika eneo hilo.

c) Mhe. Naibu Spika, kisheria majahazi hayaruhusiwi kabisa kubeba abiria. Inapotokea majahazi yamebeba abiria kwa kisingizio cha ukosefu wa usafiri wa uhakika wa meli au boti, huo ni uvunjaji wa sheria na kanuni za kiusalama za usafirishaji wa abiria kwa njia ya bahari zilizowekwa na *ZMA*. *ZMA* kwa upande wake inaendelea kuwahamasisha wenye meli kwa kuwafahamisha kwamba bado upo umuhimu mkubwa wa kuweka meli nyengine zaidi mbali na *Azam Sealink II*.

Ahsante Mhe. Naibu Spika.

**Mhe. Suleiman Sarahan Said:** Nashukuru Mhe. Naibu Spika na nashukuru kwa majibu mazuri Mhe. Waziri lakini mimi nimwambie waziri kwamba katika visiwa vyetu hivi ambavyo ni Unguja, Pemba, Tanga katika mazingira hii na Dar-es-Salaam sisi ni ndugu na tumeelewana na tunaelewena.

Usafiri wa meli hakuna na wa majahazi tumezuwia kama waziri atuambie chombo gani kilichokuwa kitakuwa salama kitakachukuwa kitakidhi haja za masikini na watu wote ambao wana uwezo ule, wakati majahazi katuzuia na meli hakuna na kwa kuangalia ni kwamba kuna muwekezaji mmoja ambaye ana boti za kwenda kwa kasi ambazo Pemba tunazihitaji kwa muda mrefu sana lakini kuna maneno ya kusema kwamba boti zile haziwezi kwenda Pemba kwasababu ya kina kikubwa cha maji.

a. Je, ni kwamba akitokea muwekezaji mwengine akawa na boti za kasi ambazo atakwenda nazo Pemba mfanya biashara huyu hatopeleka zile boti zake tena kule Pemba.

b. Kwasababu ni jukumu la serikali la kuwasafirisha wananchi wake kwenda katika maeneo ya kibiashara na maeneo mambo mengine ya mazingira kama upande wa Tanga. Je, serikali sasa hivi haioni kuna mkongojo wa jitihada ikafanyiwa matengezo au ikafanyiwa kila hali ikafanya biashara za Tanga na Pemba, ili kuokoa hali hiyo ya maisha ya watu wa Pemba na Tanga.

**Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji:** Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji napenda kuchukua nafasi hii kumjibu Mhe. Suleiman Sarahan Said masuala yake ya nyongeza yenye kifungu (a) (b) na (c) kama ifuatavyo:

a) Kama alisemea kwamba sisi tutaendelea kuwalinda raia wetu na sisi tutandelea kuwashauri wale watu ambao wako Tanga basi watumie usafiri wa barabarani kutoka Tanga mpaka Dar-es-Salaam baadaye wapande chombo kutoka Dar-es-Salaam waje zao Unguja japo kweli ni gharama lakini hiyo ndio njia rahisi kwao kuliko kutumia usafiri wa majahazi ambao iwapo watu wale wanapata ajali inakuwa hasara kubwa la serikali yetu.

b) Kuhusu atakapotokeza muwekezaji sisi kama tunavyosema tuko tayari huyo muwekezaji aje kufanya hiyo biashara, kwasababu hili ni soko huria hatumzuwi mtu yoyote katika kufanya kazi hiyo na *ZMA* wana masharti yao na wakishatimiza masharti basi tutamruhusu.

c) Kwamba anasema kuhusu MV Jitihada kama nilivyosema MV Jitihada ni meli yetu ambayo sasa hivi iko katika Shirika la Bandari, ambayo inatumika katika masuala la bandari. Suala lake tutaweza kulichukuwa na kulifanyia kazi iwapo itaoneka inafaaa.

Ahsante sana Mhe. Naibu Spika.

**Mhe. Naibu Spika:** Kuhusu utaratibu mpaka tumalize masuala na majibu hatujamaliza bado. Mhe. Simai Mohammed Said swali la moja la nyongeza.

**Mhe. Simai Mohammed Said:** Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa kuniona Mhe. Waziri nisikilize vizuri.

Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa miaka nenda miaka rudi sisi Wazanzibari tunamekuwa tunategemea sana bidhaa zetu kununua kwa kwenda Tanzania Bara kwa kutegemea bandari ya Dar-es-Salaam. Lakini ukuangalia kwa ndugu zetu wa Pemba wamekuwa

pia kwasababu kutokana na mazingira ya jiografia Kisiwa cha Pemba wako karibu sana pia na Mombasa pamoja na Tanga.

a) Sasa ni kwanini serikali kwa miaka mingi sana hivi sasa wameshindwa kuwasaidia wananchi wa Mkoa wa Kaskazini, ili kuwajengea mazingira mazuri hasa Mkoa wa Kaskazini Pemba kwa kutumia bandari ya Mombasa pamoja na Tanga, ili kuhakikisha maisha yao kwa bidhaa ambazo wanahitaji kila siku wanaweza kupata hiyo huduma.

b) Katika Mkoa wetu wa Kusini Unguja hasa wananchi katika maeneo ya Kikungwi, Ungujaukuu, Pete, Kizimkazi na Makunduchi wapo pia karibu sana na Dar-es-Salaam hasa hadi hivi leo hakuna bandari kama ile ya Mkokotoni kwa pale Mkoa wa Kusini, ili kuwaunganisha kwa haraka kufanya biashara zao na huduma zao za kila siku baina ya Mkoa wa Kusini pamoja na Dar-es-Salaam. Je, Mhe. Waziri una mpango gani kama serikali ahsante sana.

**Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji:** Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji napenda kuchukua nafasi hii kumjibu Mhe. Simai Mohammed Said Mwakilishi wa wananchi Jimbo la Tunguu masuali yake ya nyongeza yenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:

Kuhusu kuwajali wananchi wetu sisi tunawajali sana tulikuwa tunapeleka Mombasa Meli ya *MV Mapinduzi II* ikiwa haina hata abiria lakini kwa vile tunawajali baadhi ya wakati tunaenda kwa hasara lakini ile kuhakikisha kwamba tunawahudumia wananchi wetu na pia na mizigo yao. Lakini *Azam Sealink II* ilikuwa inakwenda Tanga inafanya kazi hiyo na kama nilivyosema mwanzo hivi sasa kazi hiyo inafanywa na majahazi na *land craft* nyengine na sisi kama nilivyosema mwanzo tutaendea na juhudi

zetu kutaka kuhakikisha kwamba wananchi wa Pemba nao vile vile wanafaidika na mapinduzi matukufu kwa kuwaletea usafiri wa uhakika na vile vile kufanya kazi zao kwa uhakika zaidi.

Kuhusu suala la kujenga bandari hivi sasa siye tuko katika mpango mkakati na katika sehemu ambazo zimependekezwa, basi Kizimkazi vile vile ijengwe bandari kwa ajili ya kusaidia mambo hayo ya usafiri. Ahsante sana Mhe. Naibu Spika. *(Makofi)*

**UTARATIBU**

**Mhe. Simai Mohammed Said:** Mhe. Naibu Spika, nasimama kwa kanuni ya 37 (1) waziri au mjumbe yoyote anauliza swali ambalo ana madaraka nalo atakuwa na wajibu wa kujibu swali hilo kwa ukamilifu, kwa usahihi na kwa ufupi.

Nilimwambia naomba unisikilize vizuri kwa sababu nilitaja eneo la Mombasa katika majibu yake hakutaja Mombasa na nimesema Mombasa wako karibu  na watu wa Mkoa wa Kaskazini hasa naomba majibu hayo.

**Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji:** Mhe. Naibu Spika, napenda kurejea majibu yangu nimesema kwamba MV Mapinduzi tulikuwa tunaipeleka Mombasa na tumeipeleka zaidi ya mara mbili kwa ajili ya kusaidia wananchi pia na vile kuwapelekea mizigo yao.

Mhe. Naibu Spika, naomba sana mheshimiwa hilo ndio jibu ambalo nimelijibu ahsante sana Mhe. Naibu Spika.

**Mhe. Hamad Abdalla Rashid:** Ahsante Mhe. Naibu Spika, na mimi kuniruhusu tena kuuliza swali dogo la nyongeza. Pamoja na

majibu mazuri ya Mhe. Waziri nilitaka na mimi kumuuliza swali moja dogo lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:

a) Kwakuwa, lengo la serikali ni kuhakikisha wananchi wake wanafaidi matunda ya mapinduzi na kuwarahisishia maisha ningependa kumuuliza Mhe. Waziri je kwa kuwa wasafiri wa Tanga na Pemba wengi ni wafanya biashara na wanatumia usafiri ule kwa kufanya biashara zao ana maana gani anapowaambia wasafiri wale wananchi wa Pemba wapite Dar-es-Salaam mtu ana magunia 50 ya mbatata unamwambia atoke Tanga aende Dar-es-Salaam halafu arudi Zanzibar aende Pemba ana maana gani kwanza kuwambia hivyo wananchi wa Pemba. *(Makofi)*

b) Ni hatua za gani za dharura narudia tena za dharura wizara yake itakazochukua kuhakikisha wananchi wa Pemba na Tanga wanapata usafiri wa kudumu pale kwenda Pemba na Tanga.

**Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji:** Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji napenda kuchukua nafasi hii kumjibu Mhe. Hamadi Abdalla Rashid swali lake yenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:

Kama nilivyosema mwanzo Mhe. Naibu Spika, sheria kanuni ambazo tumejiwekea sisi wenyewe ni muhimu kufuatwa ili kulinda maisha ya wananchi wetu, sote tunaelewa kwamba meli yoyote ile ambayo inafanya kazi za mizigo maana imewekwa kwa ajili ya kuchukulia mizigo hata unapokua katika usafiri wa nchi kavu tunapoweka daladala kazi yake ni kuchukua abiria na gari za mizigo ni kazi yake mizigo.

Kwahiyo sisi tunashauri yule mwenye mzigo ni kazi yake kuukabidhi mzigo kwa *captain* ya ile meli na wahusika na baadaye kufuatilia mzigo wake unapofika sehemu husika, huo ndio utaratibu ambao sisi tunauhimiza siku zote kwasababu tunafahamu abiria anapopanda katika meli ya mzigo kuna hatari nyingi kwanza zile meli zinawekwa kwa ajili ya mizigo na kuna vifaa maalum kwa ajili ya manahodha waliokuwemo mule, inakuwa hamna vifaa vyengine vya uwokozi. Kwa mfano, hii imetutokezea karibuni kuna jahazi ilizama Tanga vijana wengi mpaka wanafunzi wamefariki, mimi mwenyewe nimekwenda kushuhudia nimesikitishwa sana na tukasisitiza na tutandelea kusisitiza kauli ya serikali kwamba haturuhusu meli za mzigo kuchukua abiria.

Mhe. Naibu Spika, namuomba sana Mhe. Mwakilishi tuendelee kulinda sheria na kanuni tulizoziweka kwa maslahi ya wananchi wetu, ili linapotokea tatizo sasa tusipate kumlaumu mtu mwengine yoyote.

Kuhusu swali lake la pili kama nilivyosema juzi tu hapa wamekuja wawekezaji kutoka Korea bado tunaendelea kuwahimiza watu wawekeze Tanga tunajua kwamba Tanga na Pemba ni masafa karibu sana, itasaidia sana kwa biashara lakini kama ulivyosema nao wawekezaji nao wafuata faida na vile vile wanafuata matakwa ya namna gani wafanye biashara. Mhe. Naibu Spika, sisi kama serikali tutaendelea kuwahamisha wawekezaji waendelee kuwekeza na hivi karibuni kama nilivyosema wamekuja Wakorea wameonesha nia ya kuwekeza pale ambapo itakuwa tayari tunawakikishia wananchi kwamba hiyo kero itaondoka lakini hatukusudii kuwaekea tatizo wananchi wetu, lakini sisi tunawajali na tunawataka kuhakikisha wanapata usafiri wa uhakika.

Ahsante sana Mhe. Naibu Spika.

**Mhe. Naibu Spika:** Ahsante sana Mhe. Waziri, Mhe. Jaku nafahamu kwamba unataka kuhusu utaratibu lakini atakuja Mwenyekiti kuendelea na shughuli hii. Sasa nitafanya kazi moja tu iliyobakia ambayo ni kuwakaribisha wageni wetu wa leo hapa Barazani ambao ni wageni wa Mhe. Salha Mwinyijuma Viti Maalum ni wageni kutoka Umoja wa Vijana wa CCM Tanzania.

Wageni wenyewe ni hawa wafuatao:

| | | |
|---|---|---|
| 1) | Ndugu Tabia Maulid Mwita wa UVCCM | Makamo Mwenyekiti |
| 2) | Ndugu Aboud Said Mpate wake | Ambaye ni msaidizi |

Vile vile kuna wageni wa Mhe. Abdalla Ali Kombo Mwakilishi wa Jimbo la Mwanakwerekwe hawa ni wageni kutoka Ukweta Makunduchi Kibuteni ni wakulima pamoja na wafanyakazi wa mashamba hayo.

Wageni wenyewe ni hawa wafuatao:

1) Ndugu Ali Hassan Haji (ndevu) Kiongozi wa msafara
2) Ndugu Ramadhan Hassan Dolla
3) Ndugu Mohamed Saleh Ameir
4) Ndugu Omar Mohamed Said
5) Ndugu Ali Sengeru Haji
6) Ndugu Yahya Saleh Ameir
7) Ndugu Ame Sima
8) Ndugu Sunday
9) Ndugu Jopherei
10) Ndugu Ramadhani Kwagulo
11) Ndugu Abdala Makame Issa.

Wageni wetu wengine wa Mhe. Mohamed Said Mohamed (Dimwa) Mwakilishi wa Jimbo la Mpendae. Waheshimiwa Wajumbe tusikilizane tunakaribisha wageni kwa hiyo naomba tusikilizane, wageni wa Mhe. Mohamed Said Mohamed (Dimwa) Mwakilishi wa Jimbo la Mpendae ambao wageni hawa ni viongozi wa Kampuni ya Mohammed Omar bin Haidar Group of Dubai.

Wageni wenyewe ni hawa wafuatao:

1) Mr. Abdulsalam Kayoli
2) Mr. Rukhi Ali Khatib

Wageni hawa waongozwa na Mwenyeji wao Mr. Saleh Mohammed Said ambaye ni Mkurugezi mkaazi wa .. *Royal* karibuni sana wageni wetu.

Waheshimiwa wajumbe sasa nimkaribishe Mwenyekiti aweze kuendelea na shughuli yetu hii ya leo, Mwenyekiti karibu.

*(Hapa Mhe. Mwenyekiti (Mwanaasha Khamis Juma) alikalia kiti)*

## HOJA ZA KAMATI

### Ripoti ya Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali (PAC) ya mwaka 2017/2018

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** Mhe. Mwenyekiti kuhusu utaratibu

**Mhe. Mwenyekiti:** Nimekuona Mhe. Jaku kuhusu utaratibu

## UTARATIBU

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** Ahsante hoja yangu ilipokuwa ikijibiwa swali namba 62 aliuliza Mhe. Amina Iddi Mabrouk. Naibu Waziri Mohamed Ahmada alitumia lugha...

**Mhe. Mwenyekiti:** Nimekuona Mhe. Jaku umeniomba kuhusu utaratibu lakini hujanambia kanuni gani labda imesema.

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** kanuni ya 38 Mhe. Mwenyekiti nakushukuru kwa kuniongoza iwapo swali linakataliwa na Spika kwasababu ya kutouliza swali kwa masharti ya kanuni hizi katibu atarudia swali hilo kwa mjumbe alieyependekezwa kuliuliza pamoja na maelezo sababu ya kukataliwa.

Alikuwa hana haki ya kukataa swali Mhe. Naibu Spika, alitumia maneno ya hekma na busara alikuwa na haki ya kujibu kuwa hana mamlaka ya kukataa swali mwenye kukata swali ni wewe tu Mwenyekiti, Naibu Spika au Spika mwenyewe sio yeye kwa lugha aliyoitumia pale kwa Mhe. Amina sio lugha nzuri.

Na Naibu Spika nashukuru kaliona hilo lakini huko siko nilikuwa nataka kutowa darsa kidogo hoja yangu nimesimama kanuni ya 42 sijui utaniruhusu nisome Mhe. Mwenyekiti au inatosha tuu ushaiona..

**Mhe. Mwenyekiti:** Mhe. Jaku umenambia umesimama kwa kanuni ya 63 ambayo nimekuruhusu
nimekukubalia umesema kanuni unayotumia ya 38 sasa hivi kuna na nyengine ya sitini na ngapi.

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** Hoja yangu ni 42 baada ya muda wa mswali kwisha mjumbe yoyote anaweza kutoa hoja Baraza liakhirishwe shughuli zake zioneshwe katika orodha wa shughuli za Baraza hilo jambo la dharura, kuna jambo la dharura Mhe. Mwenyekiti.

**Mhe. Mwenyekiti:** Naam nakusikiliza

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** Ahsante sana nikushukuru sana Mhe. Mwenyekiti. Mhe. Mwenyekiti nilikuwa nikipiga kelele sana humu ndani kuhusu swali la lifti mnazimmoja kwa kweli swali hili ni la muda mrefu hata limejibiwa katika kikao kilichopita tarehe 25/09/2018 niliuliza swali la namba 89 kwa muda mrefu sasa karibu miezi mitatu lifti ya hospitali ya mnazimmoja imekuwa haifanyi kazi na kusababisha usumbufu kwa wagonjwa wanaohitaji kupandishwa juu hali hiyo pia inasumbua jamaa wagonjwa ambao wanalazimika kubeba wagonjwa na kwenda nao juu kwa hali hii.

Mheshimiwa hali sio nzuri ya mnazimmoja juzi katika kuchangia sikuchangia muda mrefu nilichukua mambo matatu nilitaja *city scan* na lifti na huu unakaribia mwaka. Madhimu ulisha ahidi ulipeleka timu ya chama pale kwenda kuhakikisha na lifti ile Naibu Waziri alikaribia kutaka kulia.

Suala la lifti mpya karibia milioni 150,000,000 sisi tushukuru Mwenyezi Mungu tuna kadi zetu za NHIF lakini kuna wagonjwa pale wanaumia wanateseka huwezi kuwabeba kupeleka juu kama Mhe. Abdalla Ali Kombo utampelekaji juu kule, kwa hiyo nataka kauli ya serikali humu ndani lifti hii ishakuwa muda mrefu na kuna wakati mwengine tunaambiwa ni nzima lakini hakuna dalili ya nzima kwa hiyo niombe serikali itupe kauli, suala hili la muda mrefu karibu mwaka mzima muda huu.

**Mhe. Mwenyekiti:** Mhe. Jaku Hashim Ayoub kanuni ya 42 uliyoitumia kuwa baada ya muda wa
maswali kuisha mjumbe yeyote anayeweza kutoa hoja kuwa Baraza liakhirishe shughuli zake ziliorodheshwa katika orodha ya

shughuli za Baraza na lijadili jambo la dharura na muhimu kwa umma kwa ruhusa ya Spika.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub nimekuelewa lakini kanuni hiyo inasema kwa ruhusa ya Spika kwa hiyo nakuomba kwa hivi sasa hilo suala tuliache tuendelee na shughuli na nyengine baadae serikali itatoa majibu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wajumbe, sasa naomba nimwite Mwenyekiti wa Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali.

**Mhe. Abdalla Maulid Diwani (Kny: Mwenyekiti wa Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali na Mashirika (*PAC*):** Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya *PAC* naomba kuwasilisha Muhtasari wa Ripoti ya Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali na Mashirika ya Umma ya Baraza la Wawakilishi ya 2017-2018.

Mhe. Mwenyekiti, naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa kutujaalia kutuwezesha kuhudhuria kikao hiki tukiwa wazima wa afya. Aidha, nikushukuru wewe Mhe. Mwenyekiti kwa kuniruhusu na kunipa fursa ya kusimama mbele ya chombo hiki kwa nia ya kuwasilisha Ripoti ya Kazi ya Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali na Mashirika ya Umma ya Baraza la Wawakilishi kwa mwaka wa 2017/2018 kwa mujibu wa Kanuni ya 108(14) ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi la Zanzibar, Toleo la 2016.

Mhe. Mwenyekiti, napenda kutoa shukurani za dhati kwa Kamati za Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo, Wizara, Mashirika na Taasisi zote za Serikali kwa mashikiano yao dhati waliyoipatia kamati hii wakati inatekeleza majukumu yake ya kikatiba. Shukurani pia ziwafikie watendaji wote wa Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu

wa Hesabu kwa kupitia kiongozi wao, kwa mashirikiano yao makubwa kwa kamati hii.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati ya *PAC* inatoa shukurani kwa Afisi ya Baraza la Wawakilishi la Zanzibar na Wizara ya Fedha na Mipango kwa kuiandalia kamati hii mafunzo mbali mbali ili iweze kutekeleza vyema majukumu yake ya kitaalamu na kwa ufanisi.

Mhe. Mwenyekiti, tunatoa shukurani za pekee kwa Katibu pamoja na watendaji wote wa Afisi ya Baraza kwa mashirikiano yao makubwa waliyotupatia kwa kipindi chote ambacho Kamati ya *PAC* inatekeleza majukumu yake. Mwisho ila sio mwisho kwa umuhimu, natoa pongezi na shukurani kwa Wajumbe wa Kamati hii kwa mashirikiano yao na kazi kubwa ya kuzipitia, kuzichambua na kuzifanyia kazi Ripoti za Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu zinazopokelewa na kamati kutoka kwa Baraza hili kwa kila mwaka. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, kamati hii inaundwa na wajumbe 7 na Sekretarieti ya Watendaji watatu kama ifuatavyo:

1. Mhe. Miraji Khamis Mussa - Mwenyekiti.
2. Mhe. Shaib Said Ali - Makamu Mwenyekiti.
3. Mhe. Abdalla Maulid Diwani - Mjumbe
4. Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi - Mjumbe
5. Mhe. Mtumwa Peya Yussuf - Mjumbe
6. Mhe. Rashid Makame Shamsi - Mjumbe

7. Mhe. Salma Mussa Bilali - Mjumbe

**Sekretarieti ya Kamati**

Sekretarieti ya Kamati hii inajumuisha Makatibu wa Kamati na Afisa wa Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kama wafuatao:-

1. Ndg. Nasra Awadh Salmin - Katibu
2. Ndg. Haji Khatib Haji - Katibu
3. Ndg. Wahida Mohamed Hafidh - Afisa wa Ofisi ya Mdhibiti

**Yaliyobainika kwa kila Ripoti**

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2017/2018 Kamati ya *PAC* ilizifanyia kazi ripoti tatu kama ifuatavyo:

1. Ripoti ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali kwa Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo (*CDF*) kwa kipindi cha kuanzia mwaka 2011 hadi mwaka 2015 ambayo haikumalizika kufanyiwa kazi katika mwaka wa fedha uliopita;

2. Ripoti ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali kwa Mawizara ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa mwaka wa fedha 2014/2015; na

3. Ripoti ya Ukaguzi wa Hesabu kwa Mashirika na Taasisi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa mwaka wa fedha 2014/2015.

Yafuatayo ni mambo yaliyobainika katika ripoti hiyo:

**Ripoti ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali kwa Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo (*CDF*) katika Kipindi cha Kuanzia Mwaka 2011 hadi Mwaka 2015**

Mhe. Mwenyekiti, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar iliingiza jumla ya shilingi 60,000,000 kwa kila jimbo kwa ajili ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo, fedha hizo zilitumika kuanzia mwaka 2011 hadi mwaka 2015.

Mhe. Mwenyekiti, itakumbukwa kuwa katika mwaka wa fedha 2016/2017, Kamati ya *PAC* ilifanikiwa kufanya ukaguzi katika majimbo 9 tu kati ya majimbo 49 yaliyoingiziwa fedha. Hivyo, kamati iliendelea kuyafanyia kazi katika mwaka huu majimbo 40 na kukamilisha shughuli hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, ingawa katika mwaka 2010 – 2015, serikali ilikuwa na jumla ya majimbo 50 ya uchaguzi. Hata hivyo, kamati hii iliyafanyia uchunguzi majimbo 49 kwa kuwa ndio majimbo yaliyokubali kupokea fedha hizo.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mshangao mkubwa napenda kuliarifu Baraza lako Tukufu kuwa, jimbo pekee ambalo halikupokea fedha hizo ni Jimbo la Mji Mkongwe kutokana na sababu anazozijua aliyekuwa Mwakilishi wa Jimbo hilo. Kitendo hicho ni kuwanyima haki ya kupata maendeleo wananchi wa jimbo hilo ingawa fedha hizo ni chache lakini wahenga wamesema “haba na haba hujaza kibaba”.

Mhe. Mwenyekiti, kati ya majimbo 49 yaliyofanyiwa ukaguzi na kamati hii ni majimbo 41 yaliyotoa mashirikiano ya dhati kwa Kamati ya *PAC* na majimbo 8 hayakutoa mashirikino kutokana na sababu zilizoelezwa kwa kina kwenye ripoti yetu ya kamati.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kuyataja majimbo ambayo hayakutoa ushirikiano katika kamati hii kama ifuatavyo:-

i. Jimbo la Donge;
ii. Jimbo la Uzini;
iii. Jimbo la Magogoni;
iv. Jimbo la Mgogoni;
v. Jimbo la Ole;
vi. Jimbo la Mkwajuni;
vii. Jimbo la Jang'ombe; na
viii. Jimbo la Nungwi.

Mhe. Mwenyekiti, kwa ujumla Kamati ya *PAC* imeridhishwa na matumizi ya fedha kwa baadhi ya majimbo. Hatahivyo, kamati haikuridhishwa na matumizi ya fedha yaliyofanywa na baadhi ya majimbo kutokana na sababu zifuatazo:

(a) Kamati za Maendeleo ya Jimbo zimetumia fedha za jimbo kwa ile miradi ambayo haikubaliki kisheria;

(b) Matumizi ya fedha yalifanywa kwa kutumia "*pro foma invoice*";

(c) Asilimia kubwa ya matumizi yaliyofanywa hayakuwa na vielelezo vya kuthibitisha matumizi hayo ingawa Kamati hii iliikagua miradi iliyotajwa na kuridhika na miradi hiyo;

(d) Kamati za Maendeleo ya Jimbo hazitekelezi miradi ambayo imejazwa kwenye fomu za maombi ya miradi zilizowasilishwa na kupitishwa na Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais;

(e) Kamati za Maendeleo ya Jimbo zilishindwa kuomba ridhaa kwa Katibu Mkuu – Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais pale panapobadilisha miradi hiyo;

(f) Kwa yale majimbo yaliyokuwa na fedha za bakaa, yalizitumia fedha hizo kinyume na utaratibu uliowekwa.

(g) Hakuna kiwango maalum cha ulipaji wa posho kwa Wajumbe wa Kamati za Jimbo na kupelekea baadhi yao kupeana posho kubwa.

Mhe. Mwenyekiti, sababu nyengine ni kama zinavyoonekana kwenye ripoti yetu katika kila jimbo husika kwenye eneo la uchunguzi wa Kamati ya *PAC*.

Mhe. Mwenyekiti, katika kuhakikisha kuwa kasoro hizo hazijitokezi tena katika awamu hii, kamati yetu ilipendekeza yafuatayo:

(a) Kamati za Maendeleo ya Jimbo zitekeleze miradi ambayo imejazwa kwenye fomu ya maombi iliyowasilishwa kwa Katibu Mkuu – Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais. Hii ni kutokana na kuwa miradi hiyo hufanyiwa uhakiki "*certification*" na ofisi hiyo, kwani baadhi ya majimbo yalitekeleza miradi ambayo utekelezaji wake ulikwama na kupelekea fedha hizo kutumika bila ya kupatikana tija iliyokusudiwa.

(b) Kamati za Maendeleo ya Jimbo ziombe ridhaa kwa Katibu Mkuu – Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais endapo inahitaji kubadilisha miradi,ili kuwa na uwiano wa taarifa wakati wa kuwasilisha ripoti sambamba na kufanyiwa tathmini miradi hiyo.

(c) Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais iendelee kutoa mafunzo kwa Kamati za Maendeleo ya Majimbo juu ya matumizi bora ya fedha hizo kwani imebainika kuwa baadhi ya kamati bado zinatekeleza miradi hiyo kinyume na matakwa ya sheria inayohusiana na Mfuko wa Jimbo.

(d) Kamati za Maendeleo ya Jimbo zihakikishe kuwa zinatumia fedha za jimbo kwa ile miradi inayokubalika tu kisheria.

(e) Kwa mujibu wa kifungu cha 8(4) cha Sheria ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo Nam. 2 ya mwaka 2012, Kamati ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo ibaki na nyaraka asili (*original documents*) na nakala (*copies*) za nyaraka hizo ndizo zinazopaswa kuwasilishwa kwa Katibu Mkuu - Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais.

(f) Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais ichukuwe juhudi za haraka kuhakikisha kuwa inajenga Ofisi za Majimbo kwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi ili ofisi hizo ziweze kutumika katika shughuli za maendeleo za jimbo pamoja na kuhifadhi nyaraka mbali mbali zitakazotumika jimboni hapo sambamba na kuepusha usumbufu kwa wale watakaohitaji nyaraka yoyote.

(g) Kamati za Maendeleo ya Jimbo zisichanganye matumizi ya fedha za Mfuko wa Jimbo na matumizi mengine yanayofanywa jimboni hapo kama vile msaada anaotoa mwakilishi, mbunge, diwani na kadhalika ili kuweza kupata hesabu sahihi ya fedha za mfuko.

(h) Serikali, ijitahidi kutoa fedha za Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo kwa wakati ili jimbo liweze kutekeleza miradi yake kwa wakati.

(i) Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ihakikishe kuwa inafanya ukaguzi wa fedha hizi kila mwaka kama inavyofanywa kwa Mawizara, Taasisi na Mashirika ya Umma ili iweze kupata taarifa sahihi juu ya matumizi ya fedha hizo. Hii ni kutokana na kuwa kitendo cha kuchelewa kufanya ukaguzi kinawapelekea watendaji wa jimbo kushindwa kukumbuka kila taarifa. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, mapendekezo yetu mengine ni kama yanavyoonekana kwenye ripoti yetu ya kamati.

**Ripoti ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali kwa Mawizara ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015**

Mhe. Mwenyekiti, katika kutekeleza majukumu yake ya kuchunguza Hesabu za Serikali, Kamati ya *PAC* ilifanya uchunguzi katika wizara mbali mbali za SMZ katika masuala mbali mbali yaliyobainishwa katika Ripoti ya Ukaguzi ya Mwaka 2014/2015,

**Maeneo ambayo Uchunguzi wa Kamati ya *PAC* Ulilenga**

Mhe. Mwenyekiti, katika kuifuatilia Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa mwaka 2014/2015, uchunguzi wa Kamati ya *PAC* ulilenga katika maeneo makuu mawili yafuatayo:

i. Taarifa za Mapato na Matumizi.
ii. Ukiukwaji wa taratibu za fedha na ununuzi uliofanywa na wizara

**Taarifa za Mapato na Matumizi**

Mhe. Mwenyekiti, katika uchunguzi wa taarifa za mapato, kamati imebaini kutofanyika kwa tathmini ya kutosha juu ya vyanzo vya mapato vilivyomo katika wizara na taasisi mbalimbali, ili kujua uwezo halisi wa vyanzo hivyo katika kutoa mapato hayo. Hali hii imepelekea baadhi ya vyanzo vya mapato kuwekewa makisio ya kukusanya mapato wasiyo na uwezo nayo na hivyo kuifanya bajeti katika eneo la mapato kukosa uhalisia.

Mhe. Mwenyekiti, miongoni mwa taasisi zilizokumbwa na hali hii ni Chuo cha Mafunzo ambacho kwa mwaka wa fedha 2014/2015 kilikadiriwa kukusanya jumla ya shilingi 41,000,000 ambapo hadi kufikia Juni, 2015 jumla ya shilingi 12,000,000 zilikusanywa sawa na asilimia 30 tu ya makadirio. Kutokana na hali hiyo kamati imeishauri Wizara ya Fedha na Mipango ishirikiane na taasisi husika katika kufanya tathmini ya vyanzo vya mapato na uwezo wake, ili bajeti inayopangwa iwe na uhalisia.

Mhe. Mwenyekiti, sambamba na hilo, kamati imebaini kuwepo kwa hali ya kunyang'anyiana mapato, ambapo chanzo kimoja cha mapato hutozwa na taasisi tofauti hususan baina ya Serikali Kuu na Serikali za Mitaa. Baadhi ya vyanzo vinavyoonekana kugombaniwa ni vyanzo vya maliasili, uingizaji wa mifugo, ada za utalii na michezo ya baharini. Ingawa kuna jitihada zinazofanyika za kutatua hali hiyo, changamoto hiyo bado inaendelea na kuwasumbua wananchi wetu. Hivyo, kamati inaiomba **s**erikali iandae utaratibu mzuri wa utozaji kodi katika maeneo hayo mawili ya serikali ili kuondoa kero kwa wananchi wetu.

Mhe. Mwenyekiti, wakati ilipokuwa katika Bodi ya Uhaulishaji Ardhi, Zanzibar, Kamati ya *PAC* ilisikitishwa baada ya kubaini kuwa serikali imekuwa ikikosa mapato mengi kutokana kutokusanywa kwa kodi ya "*Capital Gain Tax*" hapa Zanzibar

ambayo kwa mujibu wa sheria za nchi, kodi hii inatakiwa ikusanywe na Mamlaka ya Mapato ya Tanzania (*TRA*) ingawa ilielezwa kuwa mamlaka hiyo inaonekana kukusanya kodi hiyo kwa upande wa Tanzania Bara tu.

Mhe. Mwenyekiti, "*Capital Gains Tax* (*CGT*)" ni aina ya kodi ya ziada ya mapato ambayo ni faida inayotambuliwa kwenye mauziano ya mali ambayo ni kubwa zaidi kuliko kiwango cha mauziano ya awali. Aina maarufu ya "*Capital Gains Tax*" (*CGT*) ni ile inayotokana na mali zisizohamishika. Kodi hii ina uhusiano wa karibu sana na suala la uhaulishaji ardhi kwa kuwa uhaulishaji wowote wa ardhi utatakiwa kulipiwa "*CGT*". Kodi hii hutozwa kwa muhaulishaji anapohaulisha mali (haki ya matumizi ya ardhi) yake kwa muhaulishwaji. Faida anayoipata muhaulishaji katika uhaulishaji huu atailipia kodi kwa kiwango kitakachopendekezwa.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa kumekuwa na ongezeko kubwa la maombi ya uhaulishaji wa ardhi hapa Zanzibar, na kwa kuwa serikali hukosa mapato mengi kwa kutokusanywa kodi ya "*Capital Gain Tax*" inayotokana na uhaulishaji ardhi. Kamati ya *PAC* inaishauri serikali kufanya juhudi za makusudi zikazowezesha kutozwa kwa kodi hii hapa Zanzibar, ili serikali iweze kuongeza mapato yake kadri inavyostahiki.

Mhe. Mwenyekiti, katika eneo la matumizi, kamati imebaini kuwa matumizi mengi ya serikali yamefanywa bila ya kufanyiwa na kufuata Mpango wa Manunuzi wa Mwaka (*Annual Procurement Plan*). Aidha, katika taasisi nyingi hasa katika Serikali za Mitaa zilikuwa zikifanya matumizi yao bila hata kuwepo kwa mpango wenyewe wa manunuzi.

Mhe. Mwenyekiti, kutokana na hali hiyo kamati imezishauri Taasisi za Serikali kuhakikisha kuwa zinaandaa mipango yao vizuri na utekelezaji wa bajeti zao unaenda sambamba na

Mipango Kazi na Mipango ya Manunuzi ya Taasisi zao, sambamba na kufanya matumizi yake kwa kuzingatia thamani halisi ya fedha (*value for money*), ili kuepusha fedha za umma kutumika kinyume na matarajio.

**Ukiukwaji wa Taratibu za Ununuzi**

Mhe. Mwenyekiti, kwa mujibu wa ripoti ya ukaguzi, jumla ya shilingi 294,638,795 zimetumika katika ununuzi wa kazi na vifaa mbalimbali vya serikali kinyume na taratibu za ununuzi. Aidha, katika uchunguzi wake juu ya hoja hizo, kamati imebaini kasoro mbalimbali katika shughuli hizo za ununuzi kama ifuatavyo:-

a. Kutokuwepo kwa Bodi halali za Zabuni hasa katika Serikali za Mitaa.
b. Kutoshirikishwa kwa Bodi za Zabuni katika ununuzi na uondoshaji wa mali za umma katika taasisi zenye bodi halali za zabuni.
c. Ukiukwaji wa hatua zinazostahiki katika mchakato wenyewe wa zabuni.
d. Umakini mdogo wa baadhi ya watendaji wanapofanya kazi za ununuzi wa mali za umma.
e. Kasoro katika zabuni za kazi za ujenzi.
f. Ukosefu wa taaluma ya taratibu za ununuzi kwa baadhi ya watendaji wanaohusika na kazi za umma.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuzingatia masharti ya kifungu cha 10(1) cha Sheria ya Manunuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma (Namba 9 ya 2005), ambayo ndio iliyokuwa ikitumika kipindi hicho cha 2014/2015, kwa mujibu wa kifungu cha 27(1) cha sheria mpya ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma, Namba 11 ya 2016, Bodi ya Zabuni katika taasisi ya umma ndio yenye mamlaka ya kushughulikia masuala ya ununuzi na uondoshaji wa mali, huduma na kazi katika taasisi husika.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati ya *PAC* imebaini kuwa baadhi ya taasisi za umma hazina Bodi halali za Zabuni katika taasisi zao na badala yake huteuliwa kikundi fulani tu cha watu kinyume na utaratibu wa kushughulikia masuala ya ununuzi. Aidha, kwa zile taasisi za umma ambazo zina Bodi halali za Zabuni zimekuwa hazishirikishi bodi zao kwasababu tu wanazozijua wao binafsi.

Mhe. Mwenyekiti, tatizo la kutokuwepo kwa Bodi halali za Zabuni pamoja na kasoro nyengine za manunuzi limebainika katika Halmashauri ya Wilaya Kaskazini "B" wakati Kamati ya *PAC* ilipokuwa ikiifuatilia Hoja Namba 15.15 inayohusu ununuzi wa gari mbili (Fuso na Toyota Hiace) kwa gharama ya shilingi 55,700,000 bila ya kufuata taratibu za ununuzi, pamoja na Hoja Namba 15.15.2 inayohusu Ujenzi wa Chinjio la Wanyama (Donge Muwanda) shilingi 33,000,000 bila ya kufuata taratibu za kumpata mzabuni wa ujenzi huo.

Mhe. Mwenyekiti, hali kama hii imejitikoza katika Jeshi la Kujenga Uchumi wakati Kamati ilipokuwa ikifuatilia Hoja Namba 15.2.1 inayohusu Ukiukwaji wa Taratibu za Manunuzi katika Ununuzi wa Gari (*Nissan Civilian*) shilingi 46,020,000, ambapo pamoja na kasoro mbalimbali zilizobainika katika mchakato wa ununuzi wa gari hiyo, kamati imebaini kasoro hata katika umiliki wa gari husika. Hii ni kutokana na kwamba tangu mwaka 2014/2015 gari hiyo iliponunuliwa, bado kadi ya umiliki wa gari ina jina la mmiliki mwengine badala ya mmiliki wa hivi sasa ambae ni Jeshi la Kujenga Uchumi. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, cha kusikitisha zaidi tatizo la kutoshirikishwa kwa Bodi ya Zabuni limebainika pia kwa Wizara ya Fedha na Mipango, wizara ambayo ni msimamizi mkuu wa mapato na matumizi ya fedha za umma. Kasoro hiyo imebainika wakati Kamati ya *PAC* ilipokuwa ikifuatilia Hoja Namba 19.1.3

inayohusu dosari zilizojitokeza katika ununuzi wa matajuri (makasha) yaliyogharimu shilingi 38,135,593 ambapo makasha hayo yalinunuliwa kinyume na utaratibu kwa kutoihusishwa Bodi ya Zabuni.

Mhe. Mwenyekiti, sambamba na hilo, Kamati ya *PAC* imebaini kuwa kumekuwa na ufahamu finyu wa taratibu za ununuzi wa mali za umma ambapo baadhi ya watendaji wanaohusika wamekuwa wakinunua kienyeji mali kwa ajili ya serikali. Hali hii imebainika kwa kiasi kikubwa katika Serikali za Mitaa na na baadhi ya Idara Maalum za SMZ.

Mhe. Mwenyekiti, kutokana na kasoro hizo, Kamati ya *PAC* imeitaka serikali kufanya juhudi za makusudi za kutoa elimu ya kutosha juu ya Sheria mpya ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma katika ngazi zote za serikali. Aidha, kamati inawataka watendaji wote wanaohusika katika shughuli za manunuzi kufanya juhudi ya kuzifahamu na kuzifuata kikamilifu sheria zilizopo na kuachana na tamaa na visingizio visivyo vya msingi vinavyoweza kuwaingiza katika makosa. *(Makofi)*

**Ukiukwaji wa Taratibu za Fedha**

Mhe. Mwenyekiti, katika ukiukwaji wa tararibu za fedha zilizoainishwa katika Ripoti ya Ukaguzi, kamati imebaini kasoro mbalimbali katika maeneo makubwa yafuatayo:-

i. Uhaulishaji wa fedha za serikali kinyume na taratibu zilizowekwa.
ii. Kukosekana kwa vielelezo vya matumizi ya fedha.
iii. Ucheleweshaji wa mapato kupelekwa benki.

Mhe. Mwenyekiti, Kanuni ya 51(1) – (8) ya Kanuni za Fedha za mwaka 2005 ambazo ndizo zilizokuwa zikitumika kwa kipindi hicho cha 2014/2015 imeelezea utaratibu mzima wa uhaulishaji

wa fedha za umma katika vifungu mbali mbali vya matumizi vilivyomo ndani ya fungu (*vote*) husika, pindi inapohitajika kufanya hivyo.

Mhe. Mwenyekiti, kamati imeshtushwa sana kuona kwamba baadhi ya fedha za umma zimekuwa zikihaulishwa kinyume na taratibu za fedha zilizopo. Imebainika kuwa baadhi ya Maafisa *Masuul* walioaminiwa kushika nyadhifa hizo wamekuwa wakitumia mamlaka yao vibaya kwa kuhaulisha fedha za umma kienyeji ndani ya Taasisi zao kwa kisingizio cha udharura au shindikizo (*pressure*) kutoka sehemu fulani. Kwakuwa, baadhi ya Maafisa *Masuul* hao ni wazoefu katika nyadhifa hizo. Kamati ya *PAC* inaona kuwa hufanya hivyo kwa sababu ya mazoea na urafiki uliojengeka kati yao na viongozi wa Wizara ya Fedha wanaohusika na uidhinishaji wa uhaulishaji wa fedha au kwa utashi wao binafsi.

Mhe. Spika, kamati imeyabaini haya katika Wizara ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira wakati ilipokuwa ikifuatilia Hoja Namba 26.1.3 inayohusu Matumizi ya Fedha za Mamlaka ya Uthibiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar (*ZURA*) katika kazi zisizohusiana na *ZURA* shilingi 38,889,982. Aidha, hali hii pia imebainika kwa Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi wakati kamati ilipokuwa ikifuatilia hoja mbalimbali katika wizara hiyo. Kutokana na hali hiyo, Kamati ya *PAC* inawaomba Maofisa *Masuul* kutekeleza majukumu yao kwa mujibu wa sheria na taratibu zilizopo kwa kuwa wao ndio wasimamizi wa matumizi ya fedha za umma katika Taasisi wanazoziongoza.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mujibu wa kanuni ya 95(4) ya Kanuni za Fedha za Umma za 2005 ambazo ndizo zilizohusika wakati wa Ukaguzi huu wa mwaka 2014/2015, hati ya malipo isiyotimia kwa kukosekana kwa vielelezo vinavyohusika na malipo hayo (*supporting documents*), itahesabika kuwa hati hiyo imekosekana

(haipo). Aidha, kwa mujibu wa Ripoti ya Ukaguzi wa 2014/2015 jumla ya shilingi 634,330,960 zimeripotiwa kukosa vielelezo na baadhi yake kukosa maelezo wakati wa ukaguzi.

Mhe. Mwenyekiti, kukosekana kwa vielelezo vya malipo zikiwemo stakabadhi za malipo vinavyothibitisha uhalali wa malipo hayo ni kiashiria cha upotevu mkubwa wa fedha za umma na hali hii hutoa sura ya shaka ya "kulipwa" fedha za umma kwa watendaji wasio na uadilifu na wala uzalendo.

**Udhaifu katika Uandaaji na Usimamizi wa Mikataba ya Serikali**

Mhe. Mwenyekiti, sote tunafahamu kuwa miongoni mwa majukumu ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ni kuhakiki na kuchunguza kwa umakini mikataba mbalimbali ambayo serikali inaingia kati yake na nchi, kampuni au taasisi fulani. Katika kutekeleza jukumu hilo ofisi hiyo hupaswa kuangalia kila kipengele cha mkataba husika, ili kuondoa uwezekano wa athari mbaya kwa serikali na kujiridhisha kama mkataba husika unakidhi au unazingatia masharti ya taifa, ili hatimae iweze kuishauri vyema serikali.

Mhe. Mwenyekiti, pamoja na kazi nzuri inayofanywa na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu, Zanzibar katika kutekeleza majukumu yake mbalimbali, Kamati ya *PAC* imebaini kuwa bado ofisi hii ina udhaifu katika baadhi ya maeneo hususan katika Kitengo cha Mikataba kwa kukosa wanasheria wa kutosha waliobobea na weledi katika uandaaji wa mikataba inayogusa nyanja mbambali ikiwemo nyanja ya ujenzi.

Mhe. Mwenyekiti, hili limedhihirika wakati Kamati ya *PAC* ilipokuwa ikifuatilia Hoja Namba 29.1.1 inayohusu ucheleweshwaji wa uwekaji wa *tartan* katika Kiwanja cha

Michezo cha Gombani uliogharimu dola za Kimarekani 339,891.8.

Mhe. Mwenyekiti, kamati ilibaini kuwa miongoni mwa sababu zilizochelewesha uwekaji wa *tartan* katika uwanja huo ni kwamba wakati Kampuni iliyopewa kazi ya awali ya kuweka "*base*" ya uwanja huo, kabla ya kuwekwa *tartan* ilipokuwa ikifanya kazi zake kulitokea uharibifu wa mifumo ya kupitisha maji (*drainage system*) iliyokuwepo katika uwanja huo. Hivyo, kutokana na ukweli kuwa masharti ya mkataba hayakumbana mkandarasi juu ya kulipa gharama kwa kile kitendo cha uharibifu. Hivyo basi, serikali iliamua kusitisha mkataba na mkandarasi huyo wakati tayari alikuwa ameshalipwa baadhi ya fedha. Kitendo hiki kimeitia hasara kubwa serikali.

Mhe. Mwenyekiti, ingawa Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango alipokuwa akijibu swali la nyongeza la Mhe. Suleiman Sarahan Said katika kikao cha 4 cha Mkutano huu wa Baraza unaoendelea, tarehe 12/2/2018, alieleza kuwa suala la serikali kuingia mkataba kati yake na chombo kingine linafanywa kwa umahiri mkubwa, na kwa sasa mikataba yote ya serikali inapaswa kuwasilishwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kupitiwa na kupata ushauri wa kisheria. Hatahivyo, Kamati ya *PAC* inaona bado ofisi hii haina wanasheria "nguli" wa kutosha na baadhi yao hushindwa kujua mambo ya kuzingatiwa katika aina husika ya mkataba, jambo ambalo linachangia kwa kiasi kikubwa kwa serikali kuingia kwenye mikataba isiyo na tija.

Mhe. Mwenyekiti, kwa upande mwengine, Kamati ya *PAC* imegundua kuwa kuna tatizo la usimamizi wa mikataba kwa taasisi za serikali na kupelekea asilimia kubwa ya miradi ya maendeleo kutekelezwa chini ya kiwango kinachostahili.

Mhe. Mwenyekiti, kutokana na yote hayo, Kamati ya *PAC* inaishauri Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuongeza juhudi ya kupata wanasheria wenye taaluma za fani mbali mbali ili waweze kuandaa mikataba itakayokidhi haja na kuepusha hasara zisizo za lazima kwa serikali. Aidha, taasisi za serikali kwa upande wao zinapaswa kuhakikisha kuwa zinasimamia ipasavyo mikataba mbali mbali inayoingia serikali ili kulinda fedha za umma.

**Uwekaji Usioridhisha wa Kumbukumbu za Mali za Umma na Usimamaizi Mbovu wa Mali hizo**

Mhe. Mwenyekiti, mbali ya raslimali fedha, mtaji mkubwa wa serikali ni mali mbalimbali zinazomilikiwa na serikali hiyo kwa niaba ya wananchi, ziwe ni zenye kuhamishika na zisizo hamishika. Aidha, ni ukweli ulio wazi kuwa serikali hutumia fedha nyingi kwa ajili ya kununua vifaa na mali ambapo huzitumia raslimali hizi katika kujiendesha kiuchumi

Mhe. Mwenyekiti, ni kitu cha kusikitisha sana kuona hadi leo, taasisi nyingi za serikali zinaonesha udhaifu katika uwekaji wa kumbukumbu wa mali za serikali kwa kutokuwa na Daftari stahiki la Mali za Kudumu (*Fixed Asset Register*) au kwa kutoziorodhesha mali hizo katika utaratibu na muongozo unaokubalika na serikali.

Aidha, kuna baadhi ya taasisi haziorodheshi mali zote ilizonazo katika daftari hilo, hususan majengo na huorodhesha baadhi tu ya mali zinazomilikiwa bila ya kuainisha thamani ya mali na vifaa hivyo pamoja na pahala vilipo. Hali hii inatokezea wakati tayari serikali kupitia Wizara ya Fedha na Mipango imeshatoa muongozo maalum juu ya uingizaji wa kumbukumbu katika daftari hilo, lakini bado taasisi nyingi hazijaanza kuufuata.

Mhe. Mwenyekiti, tukumbuke kuwa "Mali bila Daftari Hughibu bila Khabar". Hivyo, ni vyema taasisi za serikali zikawa na daftari hilo.

Mhe. Mwenyekiti, sambamba na hilo, kamati imebaini kuwepo kwa usimamizi mbovu wa mali na vifaa vya serikali vikiwemo magari ambapo imebainika kuwa baadhi ya gari za serikali zilizoharibika zimeachwa kwa muda mrefu katika gereji za watu binafsi.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati ya *PAC* imelibaini hili ilipokuwa inafuatilia hoja za Mahkama Kuu, ambapo jumla ya gari tatu zimetelekezwa kwa chombo hiki. Kwa mfano, gari Namba SMZ 223 A na SMZ 229 A zimebainika kuwa zipo gereji na SMZ 220 A imewekwa Kijangwani kituo cha zamani cha mabasi bila ya shughuli yoyote.

Mhe. Mwenyekiti, mazingira yote hayo ndio yanayopelekea upotevu wa mali na vifaa vya serikali, pia kupelekea wajanja kujimilikisha mali hizo za umma kwa njia za udanganyifu. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, kutokana na hali hiyo, Kamati ya *PAC* inawataka wahusika wote wa utunzaji wa mali za umma katika taasisi za serikali kwenda Wizara ya Fedha na Mipango, ili kupata muongozo juu ya mfumo wa utunzaji wa kumbukumbu za mali za umma unaokubalika na serikali. Aidha, kamati inawataka viongozi katika taasisi za umma kuwa wasimamizi wazuri wa mali za serikali kwa kuhakikisha kuwa mali hizo na vifaa hivyo vinatunzwa na kutumika kwa mujibu wa taratibu zilizopo.

**Madeni**

Mhe. Mwenyekiti, Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa mwaka wa fedha 2014/2015 imeanisha madeni mbali bali kati ya taasisi za serikali na baina ya taasisi za Serikali na Taasisi Binafsi. Hali ya kuwepo kwa mlolongo wa hesabu za madeni katika vitabu vya Mdhibiti kati ya Taasisi za Umma, sio tu huathiri sura ya taasisi katika ufungaji wa mahesabu ya serikali kwa mwaka, lakini pia huathiri utekelezaji wa bajeti ya taasisi husika.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa deni huwa na pande mbili (Mdai au Mdaiwa), kuna Taasisi zimeripotiwa kudaiwa na kudai na nyengine zimeripotiwa kudai tu kutokana na huduma wanazozitoa. Taasisi zilizoripotiwa kudai ni Jeshi la Kujenga Uchumi (JKU) linaloidai Mamlaka ya Maji (*ZAWA*) shilingi 12,600,000, Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka kupitia Kituo cha Mafunzo ya Sheria na Utafiti shilingi 41,688,000. Aidha, Kamati ya *PAC* imebaini kuwa Wakala wa Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali imekuwa ikilidai Jeshi la Polisi katika Mikoa mbalimbali ya Zanzibar kutokana na ada ya kufanya uchunguzi wa vielelezo mbalimbali vinavyopelekwa katika maabara hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, Baraza la Manispaa Mjini pia limeripotiwa kudaiwa na wafanyabiashara mbalimbali kutokana na vifaa na huduma mbalimbali ambazo wafanyabiashara hao huzitoa kwa Baraza hilo. Pia, Baraza hilo limekuwa likidai kampuni mbalimbali hasa kutokana na ada ya mabango ya matangazo.

Mhe. Mwenyekiti, wakati Kamati ya *PAC* ikifuatilia Hoja Namba 15.2.3 inayohusu deni la JKU linaloidai Mamlaka ya Maji (*ZAWA*) shilingi 12,600,000 kutokana na huduma ya ulinzi inayoitoa, Kamati ilibaini kuwa licha ya deni hilo kuongezeka na kufikia hadi shilingi 19,800,000, zipo taasisi nyengine zinazodaiwa deni kubwa na JKU ikiwemo Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (*NIDA*)

Mhe. Mwenyekiti, kutokana na kuendelea kuwepo kwa madeni hayo kwa kipindi kirefu, pamoja na Jeshi hilo kuendeleza juhudi za kudai madeni hayo, Kamati ya *PAC* imelishauri JKU kuandaa utaratibu mpya wa malipo na kuzitaka Taasisi inazozipatia huduma za ulinzi kufanya malipo kwanza (*pre paid*), kabla ya kuwapatia huduma hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, kwa upande wa Baraza la Manispaa, Kamati ya *PAC* inapenda kutoa shukurani na pongezi za dhati kwa Baraza hilo kwani baada ya Kamati hii kufanya kikao na viongozi wa Baraza hilo na wafanyabiashara juu ya deni liliokuwa inadaiwa Baraza hilo na wafanyabiashara mbalimbali, viongozi wa Baraza hilo waliongeza kasi ya kulipa madeni hayo kwa kiasi kikubwa. Ni matumaini ya kamati hii kuwa viongozi wa Baraza hilo wataendeleza moyo wao wa kiungwana waliouonesha na kuendelea kuwalipa wafanyabishara madeni yao yaliyobakia ili wafanyabiashara hao waweze kuendesha biashara zao bila ya hofu ya kufilisika kwani *"Dawa ya Deni ni Kulipa"*.

**Ukodishwaji wa Maduka ya Chuo cha Mafunzo**

Mhe. Mwenyekiti, Hoja Namba 15.3.1 inayohusu Ukodishwaji wa maduka yaliyopo katika Chuo cha Mafunzo imeripotiwa katika Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu. Kwa mujibu wa Ripoti hiyo ni kwamba waliokodishwa maduka hayo walitakiwa kujenga maduka na maghala kwa gharama zao bila ya kuwepo kwa mkataba maalum kuhusiana na ujenzi huo. Aidha, kila mteja alijenga kulingana na mahitaji yake na kupelekea kutofautiana kwa gharama zilizotumika kwa maduka hayo. Pia, iliripotiwa kuwa, kwa vile wateja walijenga kwa gharama zao, Chuo cha Mafunzo kinalazimika kufidia gharama hizo na kukosa mapato yanayotokana na ukodishwaji wa milango hiyo kwa muda usiojuilikana.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kufuatilia Hoja hii, Kamati ya *PAC* ilielezwa na kubaini yafuatayo.

i. Maduka hayo yapo 24 ambayo yanasimamiwa na wafanya biashara tofauti ambao wanauza bidhaa tofauti kulingana na mahitaji ya wananchi.
ii. Maduka haya yamekodishwa kwa wafanyabishara kwa utaratibu wa kutumia mikataba ambayo wanaijaza mara baada ya kuanza biashara. Maduka haya yanabakia kwa kipindi chote yakiwa chini ya usimamizi wa mfanyabiashara husika hadi pale muda wake wa kodi utakapomalizika.
iii. Hesabu ya malipo ilikuwa inafanywa kwa utaratibu wa 1/3 ambapo sehemu ya 2/3 hubakizwa kwa mfanyabiashara na kujilipa gharama alizozitumia kwenye ujenzi wake. Malipo hayo hufanyika kila mwisho wa mwezi ambapo kodi iliyokuwa inalipwa ni shilingi za kitanzania 70,000/= kwa duka moja.
iv. Chuo cha mafunzo hakikuandaa *BoQ* awali ambayo ingeonesha mita za mraba (*square meter*) na gharama ambazo zingetumika katika ujenzi wa maduka hayo.
v. Viongozi wa Chuo cha Mafunzo wa wakati huo waliwaamini tu wafanyabiashara hao na kuwaruhusu kujenga kila mmoja akijega kwa gharama zake. Hali hiyo, imesababisha ugumu wa kuthibitisha uhalisia wa gharama zilizotumika ambapo baadhi ya gharama hizo ni kubwa mno na haziendani na uhalisia.
vi. Kila mkodishwaji ana muda wake anaotakiwa awe ameshamalizia mkopo.
vii. Kamati maalum imeundwa ili kufanya tathimini na kujua thamani halisi ya ujenzi huo pamoja kushughulikia kasoro nyenginezo zilizojitokeza katika maduka hayo.

viii. Hadi sasa Chuo cha Mafunzo hakijapatiwa hati miliki ya eneo hilo la maduka ingawa eneo hilo limeshapimwa na taratibu za kupata hati miliki hiyo zinaendelea, Changamoto iliyopo ni mawasiliano baina ya Chuo cha Mafunzo na Idara ya Upimaji.

ix. Baadhi ya mikataba ina kasoro za kutojazwa kikamilifu ikiwemo kutojazwa majina na saini za wakodishwaji katika baadhi ya sehemu zilizoainishwa kufanywa hivyo.

x. Kodi iliyokuwa inatozwa ya shilingi 70,000 kwa mwezi kwa kila duka ni ndogo ikilinganishwa na hali ya soko (*market value*) ya sasa ilivyo na eneo halisi la maduka hayo lilipo.

Mhe. Mwenyekiti, kutokana na yote hayo, Kamati ya *PAC* imetoa mapendekezo kadhaa yakiwemo haya yafuatayo:

i. Viongozi wa Chuo cha Mafunzo pamoja na wa Idara nyengine maalum wazingatie Sheria na taratibu za nchi kwanza kabla ya kutoa maelekezo au kuanzisha jambo ili maelekezo yao yaende sambamba na misingi ya sheria hizo na kuepusha kuitia hasara serikali.

ii. Uongozi wa Chuo uhakikishe kuwa mikataba ya ukodishwaji wa maduka inajazwa kikamilifu ili kuepusha migogoro inayoweza kujitokeza juu ya utekelezaji wa mikataba hiyo.

iii. Kamati ya tathmini ya ujenzi wa maduka hayo ifanye kazi zake kwa umakini zaidi, ili kuhakikisha kasoro zilizojitokeza juu ya ujenzi wa maduka hayo hazitokei tena.

Mhe. Mwenyekiti, kufuatia majadiliano ya kamati hii na Uongozi wa Chuo hiki, Kamati ya *PAC* ilipokea barua ya tarehe 23 Novemba, 2017 yenye kumbukumbu nambari MF/B.111/VOL.II/18 na nakala ya barua hiyo kutumwa kwa

Katibu Mkuu Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ inayoeleza kutekelezwa kwa baadhi ya mapendekezo ya kamati hii. Miongoni mwa mapendekezo hayo ni pamoja na:-

i. Uongozi wa Chuo cha Mafunzo kuvipitia upya viwango vya kodi za maduka hayo ili vilingane na hali ya soko ya sasa hivi na eneo lililopo maduka hayo, ili kuweza kusaidia kuongeza mapato ya Serikali.
ii. Uongozi wa Chuo cha Mafunzo ulifanya kikao na wafanyabiashara na kukubaliana gharama za maduka kwa sasa zitakuwa shilingi 130,000 kwa mwezi, na malipo hayo yataanza kulipwa mwezi wa Januari, 2018 kwa utaratibu wa mchanganuo kupitia gharama za ujenzi zilizotumika bila kukata moja ya tatu (1/3).
iii. Malipo haya yatakatwa kwa mwaka mzima ambapo gharama hizo zitapanda kila mwaka kwa gharama ya kiasi kisichozidi asilimia kumi (10%).

Mhe. Mwenyekiti, Kamati ya *PAC* imeona ilieleze suala hili kwa urefu kidogo kutokana na umuhimu wake na ni imani yetu kuwa suala hili limeanza kutekelezwa.

**Ripoti ya Ukaguzi wa Hesabu kwa Mashirika na Taasisi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015**

Mhe. Mwenyekiti, kutokana na ufinyu wa muda, katika mwaka huu wa fedha, Kamati ya *PAC* ilibahatika kulikagua Shirika moja tu ambalo ni Shirika la Umeme (*ZECO*). Katika ukaguzi wake, Kamati hii ilibaini kuwa mapato ya Shirika la Umeme yanazidi kuimarika kila mwaka, hii ni kutokana na kuwa, katika mwaka wa fedha 2012/2013 Shirika hili lilikusanya shilingi 46,751,577,193, mwaka 2013/2014 lilikusanya shilingi 57,006,231,214 na mwaka

2014/2015 Shirika la Umeme lilikusanya shilingi 63,607,465,185.08.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati ya *PAC* inazipongeza juhudi hizo, ingawa kwa upande wa matumizi Shirika la Umeme yamekuwa yakiongezeka kila mwaka, kwani katika mwaka 2012/2013 Shirika hili lilitumia shilingi 18,217,899,282, mwaka 2013/2014 lilitumia shilingi 20,741,907,023 na kwa mwaka wa fedha 2014/2015 Shirika la Umeme lilitumia shilingi 25,855,637,592.12.

Mhe. Mwenyekiti, licha ya ongezeko la matumizi hayo, Kamati ya *PAC* imeridhika na sababu ilizoelezwa na Shirika hili la kupelekea kuongezeka kwa matumizi hayo.

Mhe. Mwenyekiti, baadhi ya sababu hizo ni pamoja na mabadiliko ya mfumo wa maposho kwa wafanyakazi kwa kuweka posho maalum, ili kuwapa moyo wafanyakazi hao kutokana na kuimarika kwa utendaji pamoja na uwepo wa ajira mpya kwa mwaka wa fedha 2014/2015 ambapo jumla ya wafanyakazi 67 waliajiriwa.

Sambamba na hayo, Shirika la Umeme katika mwaka huu wa fedha lilimtumia Wakala wa Usafirishaji na Utoaji wa Vifaa (*Clearing and Forwarding*) katika kusafirisha vifaa vyake badala ya kutumia watu wa kawaida, ingawa huduma ya watu wa kawaida ni rahisi ukilinganisha na ile ya Wakala. Hatahivyo, baadhi ya watu wa kawaida hawana stakabadhi za malipo na endapo shirika lingewapa watu hao wangekosa kupata hati hiyo muhimu jambo ambalo ni kinyume na utaratibu za malipo.

Mhe. Mwenyekiti, pamoja na sababu zote hizo zilizoelezwa, Kamati ya *PAC* imebaini kuwa sababu kubwa iliyopelekea

ongezeko hilo ni Shirika la Umeme kushindwa kukadiria vizuri bajeti yake.

Mhe. Mwenyekiti, kutoka na hali hiyo, Kamati ya *PAC* ililitaka shirika hili kuwa makini wakati wa kuandaa bajeti yake ili kuepusha kasoro zisizo za lazima.

Aidha, Kamati ya *PAC* imeunga mkono juhudi ya shirika la kuwasomesha baadhi ya watendaji wake kuhusiana na shughuli ya usafirishaji na utoaji wa vifaa, jambo hili kwa kiasi kikubwa linaweza kulisaidia shirika kubana matumizi yake.

Mhe. Mwenyekiti, kutokana na maelezo yote hayo, Kamati ya *PAC* baada ya kukamilisha ukaguzi wake imeridhika na utendaji wa *ZECO* na hivyo, imehisi ni vyema Shirika hili likapata Hati Inayoridhisha ili kulitia moyo Shirika hilo.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati hii imebaini kuwa kasoro zilizobainika na Mkaguzi Mkuu na kupelekea shirika hili kupewa hati isiyoridhisha zimefanywa pia na taasisi nyengine za serikali kama vile iliyokuwa Wizara ya Kilimo na Maliasili, Wizara ya Ardhi, Wizara ya Fedha na Mipango lakini taasisi hizo zimepata hati inayoridhisha.

**Hitimisho**

Mhe. Mwenyekiti, naomba uniruhusu kwa kusema kuwa wananchi wenzetu tunao wawakilisha katika chombo hiki kutoka majimboni mwetu wengi wao wana hali ngumu ya uchumi. Tegemeo pekee lililobakia kwao ni uendelezaji wa serikali makini na inayowajibika pamoja na kuwapatia huduma bora wananchi wake.

Tegemeo jengine, sambamba na hilo ni kwa chombo hiki cha kutunga sheria na kuisimamia serikali, chombo ambacho kina wawakilishi makini wenye nia ya kuisimamia ipasavyo serikali kwa faida ya wananchi.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mnasaba wa matumaini waliyonayo wananchi wetu kwa serikali yao, ni wajibu wa serikali sasa kujidhatiti kujenga uchumi kwa kuongeza wigo wa vyanzo vya mapato, kukusanya kodi na kuthibiti mianya ya uvujaji wa mapato na udhibiti wa matumizi. Hatahivyo, haitakuwa na maana hata kidogo kama hakutakuwa na matumizi mazuri ya fedha na raslimali za nchi kwa faida ya wananchi na hii ndio maana ya utawala bora.

Mhe. Mwenyekiti, narudia tena kuipongeza serikali kwa kuweka misingi ya utawala bora kwa kuanzisha taasisi za kudhibiti na kuchunguza hesabu za serikali, kuweka sheria mpya zinazosimamia mwenendo wa fedha na ununuzi pamoja na kuwepo kwa Kamati za Baraza, zinazofanya kazi za kusimamia mwenendo wa shughuli za serikali.

Mhe. Mwenyekiti, ni matarajio yetu kuwa serikali itazifanyia kazi kasoro zote zilizobainika pamoja na kuyatekeleza mapendekezo ya kamati hii kwa maendeleo ya nchi yetu na taifa kwa ujumla.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya maelezo yangu hayo naomba kuwashukuru Waheshimiwa Wajumbe wote wa Baraza lako Tukufu kwa kunisikiliza na nawaomba waijadili na hatimaye kuipitisha Ripoti ya Kamati ya *PAC* kwa lengo la kutekelezwa na serikali.

Mhe. Mwenyekiti, Naomba kutoa hoja. Ahsante. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kumaliza Ripoti ya Kamati ya *PAC*, naomba dakika mbili nichangie kidogo. Katika mchango wangu nitakwenda kwenye suala zima la Mfuko wa Jimbo *CDF*. Nafikiri Waheshimiwa Wajumbe wenzangu wengi wa kutoka majimboni wanafahamu changamoto tunazozipata sasa hivi. Baada ya kuona kwamba kwa upande wa Waheshimiwa Wabunge wenzetu tayari hizi fedha wameshapewa mara tatu. Lakini kwa upande wetu sisi Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi tumepewa pesa hizi mara moja.

Kusema kweli inasikitisha na nahisi kwamba kidogo hamtutendei haki kwasababu utekelezaji wa hizi shughuli zote tunaomba sambamba. Pamoja na kwamba hatuambatanishi utoaji wa fedha zale. Lakini katika utekelezaji wa ile kazi kule jimboni anaoenekana Mhe. Mwakilishi anafanya, wenzetu Waheshimiwa Wabunge wanaopata fedha zile wanakuwa na nguvu kuja majimboni mwetu wakajitanua kwasababu wanafedha za kufanya maendeleo. Lakini sisi Wawakilishi tumekuwa hatuna na hatuwezi kujitanua na mwisho wa siku utanona Mbunge anafanya vizuri kuliko Mwakilishi. Kwahiyo, mnatubagua katika hicho. (*Makofi*)

Kutokana na hali hiyo, naiomba sana serikali Mhe. Mwenyekiti, ifanye haraka itupatie angalau na sisi tukaonekane kule jimboni tunakokwenda kwamba tunafanya kazi kama wenzetu Waheshimiwa Wabunge wameshafanya mara tatu. Pamoja na hayo lakini hata katika usimamizi tuliomba katika ripoti hiyo kwamba bado mafunzo yanahitajika kwa wasimamizi, sisi wenyeviti tunapata yale mafunzo lakini ningeomba serikali, ili kuondosha hizi kero zinazojitokeza basi mara kwa mara waweze kupata zaidi watendaji wetu ile mufuko ya maendeleo ya jimbo ili hizi kasoro zisijitokeze tena katika ukaguzi utakapopita.

Mhe. Mwenyekiti, nampongeze sana Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango kwasababu ripoti iliyopita tulitoa changamoto nyingi na kasoro nyingi zilijitokeza, na lakini kwa ripoti hii tulioisoma 2017-18 naona kwamba zile kasoro zimeondoka. Inaonesha umakini wako katika kusimamia hayo namna watu wanabadilika hatua baada ya hatua, nikupongeze na uzidishe juhudi kwamba hizi ripoti zimebakie kuwa ndogo zaidi haya hapa ambapo zilipo, ili nchi yetu ule muono wa utawala bora unapatikana.

Nikiendelea mbele katika mchango huu wakati tunatembelea kwenye majimbo tumekuta na changamoto mbali mbali kwa mfano, tuliandika kwenye ripoti kwamba kupatiwa ofisi kwa Wawakilishi. Kwakweli, ni jambo la msingi sana tumeona wenzetu wabunge baadhi ya maeneo walianza kujenga ofisi za wabunge wao na baadhi ya shughuli zetu tungekwenda kuzifanyia mule katika ofisi zile za wabunge.

Lakini kwa upande wa Wawakilishi hilo jambo halipo tunafanya sehemu zisizokuwa na hadhi kama Wawakilishi kwenda sehemu zile, leo hii tutakwenda kuwekwa kwenye Madrasa pengine hata busati hamna. Wajumbe wa Kamati ya *PAC* tunakwenda kukagua sehemu hata busati la kukalia hamna tunasimama kwa kufanyia kazi kwa kweli haitendewi haki ikiwa kama Kamati ya Baraza la Wawakilishi inakwenda kukagua sehemu husika kwa kukosekana sehemu ndio tunawekwa sehemu kama zile tulifika kukalia mawe na matofali wakati tunakagua mifuko wa majimbo.

Mhe. Mwenyekiti, suala hili lishughulikiwe haraka kujengwa ofisi, namuomba Mhe. Waziri pamoja na serikali ilichukue iangalie kwa kina, ili itoke na azimio kuwajengea ofisi katika majimbo yetu, ili kamati inapokwenda kule mara nyengine ikae katika sehemu nzuri ambayo yenye hadhi na wale Waheshimiwa Wawakilishi wake. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nataka niseme hayo machache mimi mwenyewe binafsi na kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Jang'ombe naikubali ripoti na naiunga mkono asilimia mia moja. Vilevile, naomba Waheshimiwa Wajumbe wenzangu tuichangie kwa makini, ili kuweka mustakabli mzuri wa serikali yetu. Aahsanteni sana kwa kunisikiliza. (*Makofi*)

**Mhe. Mwenyekiti:** Ahsante sana nakushukuru Mhe. Abdalla Diwani Mwakilishi wa Jimbo la Jang'ombe kwa niamba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali nakushukuru sana. Sasa Waheshimiwa Wajumbe, hoja imetolewa na imeungwa mkono majadiliano yanaendelea mchangiaji wetu wa mwanzo naomba nimwite Mhe. Simai Mohammed Said, atafuatiwa na Mhe. Rashid Makame Shamsi na Mhe. Shehe Hamad Matar ajiandae.

**Mhe. Simai Mohammed Said**: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, nichukue safasi hii kwanza kwa kukushukuru wewe kwa kuniona mimi na kuweza kunipa hii nafasi ili na mimi niweze kuchangia au kutoa mawazo yangu katika ripoti hii ya Kamati ya Kudumu ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali na Mashirika (*PAC*) ya mwaka 2017/2018, lakini pia tukiongelea hesabu hii ya mwaka 2014/2015.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kumpongeza Mwenyekiti au aliyesoma ripoti kwa niaba ya Mwenyekiti Mhe. Abdalla Diwani Mwakilishi makini wa Jimbo la Jang'ombe nimefurahi sana pia na mchango wake angalau na yeye pia ameweza kutupa mwanga ripoti hii ni nzito inagusa taasisi nyingi za serikali pamoja na serikali kwa ujumla.

Mhe. Mwenyekiti, pia nichukue nafasi kumshukuru pia kuwashukuru wananchi wangu wa Jimbo la Tunguu nikiwa msemaji wao mtetezi wao hapa Baraza la Wawakilishi, bila ya

wao mimi nisengelifika hapa kwa hivyo, nawashukuru sana na mimi nitaendelea kuwa mtetetizi wao na msemaji wao ili niweze kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar kuweza kuishauri serikali katika sehemu tofauti.

Mhe. Mwenyekiti, leo nimepata nafasi kiwa wa mwanzo kuweza kuchangia ripoti hii, lakini niseme hasa ripoti ya *PAC* ni katika ripoti moja ambazo zinakuwa ni ngumu kuzipitia, ni ripoti ambayo unahitaji kufikiria kwa umakini kabisa ni ripoti ambayo unahitaji unachokisema uwe unasema ukweli lakini pia unachokiona uwe na uhakika nacho.

Sasa moja ya changamoto ambayo ninayoipata nimekuja hapa leo kuchangia ripoti hii, lakini ukiangilia hasa ripoti hii hizo fedha ambazo zinaongelewa na ukaguzi uliofanya ni mwaka 2014/2015, Mhe. tuko 2018 leo ukiangalia hapa katikati 2015/2016 imepita 2016/2017. Sasa nataka nitoe ushauri, naomba sana ofisi ya *CAG* pale mwaka wa fedha unapomalizika kutoka mwezi wa Juni unapoanza *first of* Julai, mpaka Disemba katika kile kipindi cha mwaka hasa kile kipindi kile ndipo utumike kufanya ukaguzi wake, na kama anahitaji wafanyakazi na nyenzo, basi serikali impatie kwa mujibu kwasababu yeye ni kwa mujibu wa kifungu cha katiba anatambulika ndani ya katiba. *(Makofi)*

Leo ninaambiwa hapa nikiwa ni Mwakilishi wananchi wa Jimbo la Tunguu, nichangie ripoti hii ya *PAC* Mhe. Mwenyekiti, tunaongelea ripoti hii leo, ya *PAC* 2014/2015 ukaguzi uliofanya aliyekuwa Waziri wa Fedha 2014/2015 hayupo tena sasa ameshakuwa Balozi, aliyekuwa Naibu Katibu Mkuu wa Wizara hiyo hayupo tena saivi Naibu Katibu Mkuu wa Baraza, Aliyekuwa Kamishina wa *ZRB* pengine sasa hivi ni mwengine.

Sasa serikali iliyokuwepo mawaziri waliokuja wote hawa ni wapya hata waziri mwenyewe wa fedha ni mpya, sasa leo

nikisimama nikimtaja Waziri wa Fedha hichi hichi si ambae aliyekuwepo lakini sawa ni serikali iko pale pale lakini wale wahusika wengi washaondoka. (*Makofi*)

Sasa mimi niombe hata pengine  pia wale wambao wanadiwa au serikali inawadai inawezeka itakuwa washalipa nitakuwa ninafanya kosa kubwa sana leo kumtaja kampuni au mtu ambae alikuwa anadaiwa wakati tayari yeye ameshalipa kwasababu muda ni mrefu umepita. Mhe. Mwenyekiti, naiomba sana serikali, tujitahidi katika mwaka fedha ambao wanapomalizika tu, basi ile miezi sita inayofuata Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali aingie kazini, ili ripoti ije *on time* na sisi tuweze kuichangia leo tunachangia jambo ambalo mtu halipo, kwahiyo ni mtihani. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, naomba kutumia akili zangu za kufikiria, ili niweze kuishauri serikali, kwa upande ambacho naamini nitaweza kuwasaidia kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar na majukumu yangu ambayo ninatakiwa kuwasaidia.

Kwahivyo, naomba jambo la kwanza walibebe hii *issue* ya *CAG*, ili apatiwe hao wafanyakazi wa kutosha na fedha, ili ripoti hii ikija sasa hapa unaangalia ripoti lakini waziri mwenye dhamana yupo hapa Katibu Mkuu na watendaji wake wako juu tunaweza angalau takabana sehemu, siwezi tukabana kitu ambaye pia hayupo. *(Makofi)*

Baada yapo sasa naanza kutoa mchango wangu la kwanza nataka nianze kuchukua fursa hii kumpongeza Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kazi nzuri aliyoifanya hasa katika sekta ya afya, nimejaribu kuangalia kwa upande wa Mnazi Mmoja na maeneo mengine. Kwakweli, lazima tukiri katika hata hichi kipindi cha miaka hii tunachokwenda nacho inawezekana sana kwa Rais huyu wetu wa Zanzibar sasa hivi

Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein tangu Mzee Karume, hawa wa katikati wamefanya kazi nzuri lakini jinsi na bidii na nguvu alivyoipeleka ametoa mwanga nzuri sana katika sekta ya afya. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, lazima tumpongeze kwasababu kazi hizi na huduma ambazo wananchi wanazozihitaji, na ukiangilia kwa fedha ambazo zinatumika ni fedha nyingi. Kwahivyo, Mwenyezi Mungu amjaalie awe na umri mrefu na pia niombe pia serikali na wananchi wote wa Zanzibar katika hili jambo la sekta ya afya, ambao kuna mapinduzi makubwa yamefanyika, leo ukipita pale Mnazi Mmoja unaliona jengo zuri limependeza, ukienda kule Pemba unaona Hospitali ya Abdala Mzee ina vifaa vipo. Sasa, ukiangalia hii ripoti kazi nzuri iliyofanyika sekta ya afya, basi waendelee na pamoja na waziri mwenyewe dhamana kwa kushirikiana na pia na Ofisi ya Makamu wa Pili au Makamu wa Pili mwenyewe. *(Makofi)*

Suala la pili ambazo nataka nilizungumze ni mfumo wa tenda zetu ambazo zinatolewa, Mhe. Mwenyekiti wakati serikali inapotangaza tenda au kwa mahitaji inaweka zile *specification* na mahitaji ambayo nitaongea kwa lugha nyepesi, ili wananchi waweze kufaidika. Kwa tenda ambazo ni kubwa, kuna umuhimu mkubwa sana serikali ikiwa inaangalia sana katika taasisi zetu ambazo pamoja na idara kwa wale ambao mambo wanaohitaji.

Mhe. Mwenyekiti, kwa nini nasema hivyo, ukiangalia wakati mwengine tenda zinazotolewa na mahitaji ambao yaliyokuwepo pamoja na Sheria ya Manunuzi ambayo ile tuliyoirekebisha hapa unakuta haziendi samba samba, unaweza kwa bidhaa ambayo unataka kuinunua nje lakini bidhaa hiyo hiyo ukainunua ndani ya Jamhuri ya Muungano Tanzania ukakuta hapa ndani ni ghali zaidi kuliko ile ambayo umenunua nje.

Sasa, naomba sana naunganisha katika suala hili pamoja na mahitaji ya serikali katika suala zima la *stationary*, makaratasi, penseli kalamu, *computer*, *printer*, *UPS* na maeneo yote, ukiangalia huduma hizi na fedha ambazo serikali inatumia na matengenezo ambayo wanayofanya haziko sawa. Unaweza kununua *computer* leo ya 3,000,000 au 4,000,000 lakini kifaa chake cha *spear* kishaungua kutoka na hitilafu ya umeme haijawekwa *UPS*, kwa hivyo mchana umeme umezimika na kuwaka wakati aidha yule kiongozi wa serikali au mtendaji hayumo kitu kinaungua unakuta sasa ile huduma ambayo inayohitajika haipatikani tena.

Kwahivyo, mfumo wa vifaa ambavyo serikali inahitaji kutumia uwe ni mfumo *uniform*, ambao wanachokihitaji wanachokitumia kinaenda sambamba na kile ambacho wanachokitangaza kwa ujumla kwa wizara zote. Sasa leo ukiangalia kwa upande kwa mfano sekta ya afya juu ya madawa wana bohari yao lakini kwanini suala la matumizi ya *stationary*, *paper* vitu hivi vyote haufanyiki utaratibu ambao serikali itaweza kununua kwa pamoja.

Ukiangalia hata humu ndani ya Baraza la Wawakilishi makaratasi ambayo tunayotumia vifaa ambavyo tunahitaji, ni vingi sana. Mhe. Mwenyekiti, katika mfumo huu najaribu kuunganisha katika yale ambayo tukusudia kuyatumia katika suala zima *E – Government* na katika kutumia huo mkonga wa taifa. Kwahiyo, dhana ya suala la *E – Government* iliyokusudiwa na ukija kuangalia matumizi haya ya *stationary* haya ambayo tunayokwenda nayo haziko sawa hadi hivi sasa.

Kutokana na hali hiyo, serikali inatumia fedha nyingi katika masuala na nyezo kama hizi makaratasi huduma nyengine tofauti. Sasa ukiangalia yale dhamira ambayo tuliokusudia *E – Government* hatujaifikia bado ukiangalia moja hata ukienda katika taasisi za serikali katika zile huduma ni taasisi chache sana.

Kwahiyo, serikali katika mfumo mzima na fedha nyingi walizotumia katika kuelekeza nguvu zao katika mfumo wa *E – Government,* basi bora ni vizuri waka- *reverse* kwamba ah! *Is it realistic? Is it financial viable?* Halafu wangalie kama mfumu huu wanaokwenda nao ndio unaofaa. Kwakweli, haiwezekani tukawa tunaomba wimbo wa *E – government* lakini haupo.

Mhe. Mwenyekiti, hapo hapo nataka niulize ukiangalia katika ripoti mkataba ambao serikali ilifunga na *ZANTEL* ni fedha zile ambazo tukiluwa tunadai katika ule mkonga ni kiasi gani tayari wameshazipata. Kwahivyo, watakapokuja kuleta ripoti yao ya Septemba tuweze kuelezwa mkataba wa *ZANTEL* na serikali katika kutumia ile *fiber optic* kutoka Dar-es-Salaam mpaka hapa kwasababu walikuwa wanatoa huduma kwa tasisi tofauti hapa Zanzibar. Je, serikali katika ule mkataba ni kiasi gani zimepatikana katika mpango mzima walichokubaliana katika mkataba wao tangu 2012 kuendea juu.

Lakini nataka niuze suala muhimu sana magari ya serikali Mhe.Mwenyekiti serikali inapata hasara sana katika magari, tunatumia fedha nyingi kuwanunulia mawaziri wetu, naunga mkono sana serikali kwa manunuzi waliofanya juu magari mapya. Kwakweli, hivi sasa kwasababu tunapopokea wageni ni magari hayo hayo ya viongozi wetu yatumika kuwapakia viongozi tofauti wanaokuja kututembelea katika visiwa vyetu na tukiri hivi sasa Zanzibar tunakuwa tunapokea wageni tofauti, lakini matumizi ya magari haya tatizo ni pale vifaa vinapoharibika.

Mhe. Mwenyekiti, naomba nizungumzie suala la bima lakini matengenezo pamoja na *services* yao hatuna *garage* nzuri kwa ajili ya magari ya serikali, leo ukienda magari yote ya serikali yatengenezwa kule *Toyota,* kwasababu hakuna mtu anatakuwa na vile vifaa vinavyostahiki pamoja na *spare.* Niliwahi kushauri hapa kwamba eneo la Matrekta tutengeneze *garage* ya kisasa hata

Wanzanibari watahitaji huduma zakupata *garage* na tuta *create* ajira na katika mnasaba huu nikasema kwamba tutumie Chuo cha Karume pamoja na watendaji ndani ya vyombo vyetu vya ulinzi na usalama ambao wana elimu ya kutosha tuwafundishe na mashine za kisasa kutoka *welding*, kutia rangi, *services* kutoa maplagi, mashine, *overhaul* yote. Kwakweli, gari ya serikali unaikuta imepaki nje katika *garage* hata huijui wakati mwengine, sasa inategemea pia na fedha wizara au taasisi walizokuwa nazo.

Mhe. Mwenyekiti, naomba sana serikali ije na mpango maalum au mahasus kule Karakana ukienda sawa ipo, lakini iwe na mpango wa *garag*e maalum, ili kutumia gari za serikali, vyombo vya ulinzi na usalama. Siku hizi Mhe. Mwenyekiti, unaweza kuweka *camera* kidogo au kitu cha kurikodi ndani ya gari ya waziri bila yeye mwenyewe kujua na ukamsikia nachozunguza ndani ya gari kila unachokitaka.

Kwahivyo, gari za viongozi wetu hazitakiwi kuguswa guswa mikono mikono na *garage* yoyote zinatakiwa zisimamiwe na watu ambao wanastahiki, wanaoaminika na kulinda siri pamoja na mali zilizokuwemo ndani ya magari hayo, kwasababu gari ni ofisi ya waziri, dereva ni msaidizi wa waziri, kwa hivyo siri za serikali zimo zinatembea ndani ya gari. Kwa mfano, ukimkuta Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora Mhe. Haroun Ali Suleiman anapokwenda kama Makunduchi utamkuta nasoma ndani gari ana karatasi kabeba, anafanyakazi masaa ya ofisini na wakati anapokwenda jimboni na akirudi utamsikia yupo kwenye simu. Sasa mambo kama haya yanahitajika kwamba ofisi za mawaziri zitumike. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, nataka nizungumzie suala la *parking* ya magari. *Parking* za magari ni vizuri serikali ikaweka kusimamia mapato lakini hebu tuwaonee wananchi wetu huruma Jumamosi

na Jumapili mtu wa Manispaa anafanyanini, mwananchi anastahiki na yeye kupewa hizo huduma, dunia kote ukenda ni *Monday to Friday*, Jumamosi na Jumapili ni siku za mapumziko, mtu anatoka na mke wake na watoto wake akipaki gari kidogo alipie *park* inahusu nini, tuwaachie wananchi wa-*enjoy* huduma zao wanaipenda serikali yao. *(Makofi)*

Lakini pia kuna maeneo utakwenda pale mahakamani mtu ana *collect parking* mpaka kumi na nusu unaweka gari pale chini unakwenda ofisi ya *ZANTEL* kwenda kufanya malipo, mtu anataka ulipe namwambia kwani *time* sio zishapita honi ikilia saa tisa na nusu siku imeisha ya kazi, ina maana sasa ni wakati mwengine. Kwahivyo, huduma hizi tuangalie kwenye ma-*parking* lakini ikiwezeka kwenye masuala ya *parking* tu-*privaties* tuwaangalie wananchi hata hao watendaji wa serikali wanavovaa unawakuta wakinamama wanakamata *parking* leo Januari *temperature* nje iko 32 joto sana mtu anavaa kofia huduma ya pesa anayoipokea *parking* mavazi anayovaa hapewe ile heshima yake juu ya akinamama.

Mhe. Mwenyekiti, hebu tuangalie hakuna kibanda, hakuna sehemu kaekewa *furniture* mapumziko anakaa kaa nje ni sawa sawa na madereva wetu hawa wanokuja Baraza la Wawakilishi ukiwangalia wanazaga zaga tu nje hawana sehemu maalumu wakapumzika, ili wakisubiri viongozi. Kwahivyo, watu wanakaa katika maeneo ya *parking* wafanyiwe vizuri hizi huduma ili pale wanapokaa unajulikana unalia unaondoka.

Kwakweli, tuki-*privaties* eneo la *parking* pengine tutapata huduma bora zaidi watatafuta kwa mashine utakuta mtu kava *uniform* unamtambua na inawezekana hayo mapato yataongezeka. Kwahivyo, serikali naomba sana iangalie katika masuala haya.

Lakini pia nataka niongelee katika eneo la miradi mikubwa ya serikali ambayo imeguswa guswa humu kidogo Mhe. Mwenyekiti, serikali inatumia fedha nyingi sana katika miradi mikubwa na katika eneo moja ambalo ukiliangalia ni maskuli ambayo ina mpango wa skuli za ghorofa kujenga maghorofa kwa ajili ya kusimisha ofisi. Sambamba na hili *priority* katika hizi taasisi za serikali pia katika miradi na fedha ambazo zinazoingia ziende sambamba juu na matumizi ambayo wale wanaotumia.

Mhe. Mwenyekiti, tunaposema Zanzibar Utalii kwa Wote, unapokwenda Afisi ya Kamisheni wa Utalii ambayo juzi pia nilizungumza, ukienda katika Afisi ya *AG*, ukienda katika Wizara ya Katiba na Sheria ni majengo mazuri. Ukienda katika jengo la *ZRB* ni jengo zuri, ukienda katika Afisi ya Wizara ya Biashara ni jengo zuri. Lakini ukienda katika majengo ambayo tayari yule ng'ombe anaetoa maziwa yake, ukiangalia hasa kwa upande wa sekta ya utalii lile jengo halifai. Sasa leo ukikuta jengo hilo hilo linatakiwa linatakiwa lisimamie Mpango Mkuu wa Serikali katika suala zima na kuweza kumshauri waziri katika sekta hiyo.

Kwanini nasema hiyo, kwa mfano upande wa leseni wanatakiwa wasimamie wao, idadi ya watalii wanaotaka kuingia wasimamie wao, watalii wanapotoka *Airport* kuweka *computerize system* ya Bandari na *Airport* wasimamie wao. Mhe. Mwenyekiti, nazungumzia katika vitu ambavyo ni vitu vya mbele ni vitu vikubwa, ili zikaunganishwa katika sekta nzima ya utalii kwa pamoja, sizungumzii vitu kama mtu hajalipa shilingi elfu mia tano ya leseni aangalia *the bigger picture* kwamba hii Kamisheni ya Utalii inatakiwa moja kwa moja iwe ni sehemu ambayo inaangalia mapato yote yanayoingia kutoka *Airport* watu. Lakini kutokana na mazingira yaliokuwepo hata kutokana na changamoto tuliokuwa nazo na sheria tuliokuwa tunazo huwezi ukawa *question* kutokana na mazingira yalivyo, huwezi ukamuuniza mtu ukamtaja

ukambana katika maeneo ambayo yeye mwenyewe zile nyenzo hanazo.

Kwahivyo, naomba katika suala zima la ripoti hii ukiangalia kutokana na muda ambao ushapitwa. Sasa serikali iangalie katika *bigger up picture* ni mfumo upi unataka kwenda nao kutoka huo mfumo wa *E-Government* na kuziunganisha taasisi zote. Matumizi yao wanayoyafanya wakati mwengine ni lazima Sheria ya Manunuzi tuliyopitisha sisi hapa ukiiangalia na kama kweli itabidi watu wa serikali na wao waifate haitekelezeki mia juu ya mia, kutokana na changamoto zilizopo Zanzibar ni kisiwa kila kitu kinaletwa…

**Mhe. Simai Mohamed Said:** Mhe. Mwenyekiti, muda wangu.

**Mhe. Mwenyekiti:** Una dakika tatu malizia.

**Mhe. Simai Mohamed Said:** Haya ahsante nakushukuru Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti, nazungumzia hilo kwa ujumla kwa mfano ukienda katika ripoti hii ya mwakaa 2014/15 ukurasa 160 kuna sehemu hapa inasema:

"Dosari zilizojitokeza katika ununuzi wa matajuri shilingi milioni thalathini nane ya Wizara ya Fedha na Mipango".

Ukisoma maelezo *PAC* inafanyakazi vizuri na maelezo ya Wizara ya Fedha na Mipango ni mazuri lakini ukiangali sasa kutokana na sheria wanahitaji zile *save* na walinunua pengine kwa fedha bei ya chini kabisa na walilazimika kufanya hivyo. Je! Ingekuwa hawajafanya hivyo dosari kiasi gani ingetokezea na fedha katika uhifadhi mzima wa fedha na nyaraka za siri za serikali.

Mhe. Mwenyekiti, sasa hapa ndipo inakuja migongano mtu kama utaifuata hii sheria inakwamwisha utaratibu mzima wa kazi na ukaitia serikali hasara, unataka kufanya nia njema jambo zuri *PAC* anakuja kukusubiri sasa nani yuko sawa serikali yuko sawa maamuzi yaliyofanywa na Wizara ya Fedha na Mipango yako sawa. Mhe. Mwenyekiti, kitandawili hicho nakuachia wewe. Kwahiyo, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii kuchangia nawashukuru wananchi na Wajumbe wa Baraza hili la Wawakishi ahsanteni sana, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**Mhe. Mwenyekiti:** Ahsante nakushukuru Mhe. Simai Mohammed Said kwa mchango wako. Sasa naomba nimwite Mhe. Rashid Makame Shamsi, atafuatiwa na Mhe. Shehe Hamad Mattar na Mhe. Hussin Ibrahim Makungu ajiandae.

Waheshimiwa Wajumbe, naomba niwakumbushe majadiliano yanaendelea, lakini kwa hawa niliowataja mpaka hivi sasa huyu Mhe. Hussein Makungu ndiye atakuwa mchangiaji wetu wa mwisho kwa hivi sasa, mpaka sasa bado napokea maombi.

**Mhe. Rashid Makame Shamsi:** Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi ya kuweza kuichangia ripoti hii ya Kamati ya *PAC* ambayo inahusika na uchunguzi na udhibiti wa fedha za serikali.

Mhe. Mwenyekiti, nianze tu kuipongeza sana kamati hii ya *PAC* ambayo mimi ni mmoja wa *member* wake kwa kuweza kuwasilisha ripoti hii kwa umakini. Nimpongeze sana mwakilishi wa Jimbo la Jang'ombe Mhe. Abdalla Maulid Diwani kwa uwasilishaji wake mzuri. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nimpongeze pia aliyenitangulia katika kuichangia ripoti hii Mhe. Simai Mohammed Said mwakilishi makini. Mhe. Mwenyekiti, mimi nina kazia kazi tu kwa sababu ni

mjumbe wa kamati hii. Kwahivyo, nianze kuchangia au kukazia ripoti hii nianze kwanza katika suala zima la kukiukwa kwa taratibu za manunuzi. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, ni kweli kwamba katika taasisi zetu, katika wizara zetu sio zote lakini bado kuna kasoro katika suala zima la ukiukwaji wa taratibu za ununuzi. Mhe. Mwenyekiti, katika baadhi ya taasisi unaweza ukakuta kwamba pamoja na kuwa upo mpango kazi, ambao unaonesha *activity* mbalimbali za mwaka unaohusika wa fedha, lakini unaweza ukakuta kwamba hakuna mpango wa manunuzi. Sasa kitendo cha kutokuwepo kwa mpango wa manunuzi maana yake kunaweza kukawa kunapelekea vilevile ukiukwaji katika suala zima la ununuzi wa vifaa mbalimbali.

Vilevile, kuna tatizo la ukiukwaji hususan katika suala zima la kutoshirikisha Bodi za Wazabuni, taasisi nyingi zina Bodi za Zabuni, lakini unakuta kwamba katika baadhi ya manunuzi bodi hizi hazishirikishwi ipasavyo na inatokea pengine watu wawili au watatu ndani ya taasisi ndio wanaofanya ununuzi kutokana na utashi wao. Vile vile kunakosekana katika baadhi ya taasisi vielelezo ambavyo vinahusika na matumizi au ununuzi ambao umefanyika.

Mhe. Mwenyekiti, hii ni hatari tunahitaji wizara husika ziweze kuzingatia hili na sio suala la Waziri wa Fedha na Mipango tu, ni suala la viongozi wa taasisi zote kuweza kuhakikisha kwamba watendaji wao hususan katika kitengo au vitengo vya manunuzi, basi wanafuata taratibu zinazohusika ili kuweza kudhibiti na kutumia vizuri fedha za umma.

Mhe. Mwenyekiti, nikiondoka hapo nije katika suala zima la ukadiriaji wa mapato. Mhe. Mwenyekiti, tumeshuhudia kwamba suala la ukadiriaji wa mapato katika taasisi mbali mbali bado lina mtihani kidogo. Nipongeze kwa zile taasisi ambazo ukadiriaji

wake unakwenda vyema, sasa sijui hapa wa kulaumiwa kwasababu unapozitembelea taasisi nyengine zinadai kwamba ukadiriaji wa mapato haya unafanywa na Wizara ya Fedha na Mipango. Sasa tatizo linalojitokeza kama ripoti ilivyosema kwamba unaweza ukakuta kwamba kuna ukadiriaji ambao makadirio yanaonekana ni makubwa mno, lakini vile vile kuna ukadiriaji ambao makadirio yanakuwa ni madogo mno ukilinganisha na vyanzo vyenyewe vya mapato.

Mhe. Mwenyekiti, nashauri taasisi inayohusika yaani, Wizara ya Fedha na Mipango iweze kufanya makadirio kwa taasisi zetu kiuhalisia. Nina maana gani kiuhalisia, ni lazima katika kila mwaka wa fedha basi yafanywe mapitio katika taasisi hizi, ili kuweza kuona kwamba vyanzo vyenyewe vya mapato vilivyopo kwamba je, ni vile vile au kuna vyanzo vipya vya mapato ambavyo vimebuniwa au inawezekana vile vile Mhe. Mwenyekiti, kuna vyanzo vya mapato ambavyo vimekufa. Sasa unapofanya makadirio mezani kwa taasisi maana yake hapa huzitendei haki kwa kuangalia *trend* ya mwaka jana tuliwakadiria hiki kwa hivyo mwaka huu tuwaongezee kidogo, hapo hakuna uhalisi. Uhalisia ni kuweza kufanya mapitio, kufanya *survey* na kuweza kuvisoma vyanzo vya mapato kwa mwaka ule wa fedha.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo nielekee katika Mfuko wa Majimbo. Ripoti imezungumza na niwapongeze sana Wenyeviti wa Mifuko hii ya Majimbo ambao wamefanya vizuri katika kipindi kile. Ripoti ya Mfuko wa Majimbo iliyozungumzwa ni ya kipindi kirefu ambacho kimepita, hata hivyo nichukuwe fursa hii kuweza kuwapongeza wenyeviti na kamati zao ambao wamefanya vizuri kwa wakati ule. Lakini ilizungumziwa changamoto ya kukosa ushirikiano kamati na baadhi ya majimbo, haya yameshapita lakini tugange yajayo.

Mhe. Mwenyekiti, niwaombe sana wajumbe wenzangu wa Baraza la Wawakilishi waliopo hususan wale wenye majimbo, basi kasoro hii ambayo imejitokeza kwa wenzetu ambao wamepita katika kipindi kile basi kasoro hii isijirudie. Waipe ushirikiano mkubwa Kamati ya *PAC* ijayo ili kuweza kuona kasoro mbali mbali zinakiukwa. Ukweli haiwezi kuingia akilini kwamba Mwenyekiti wa Kamati ya Mfuko wa Jimbo kutoipa ushirikiano Kamati ya *PAC* wakati wewe na wajumbe wenzio ndio ambao mlikuwa mas-ul katika pesa ambazo tumepewa. Kwa hivyo, niwaombe sana Waheshimiwa Wajumbe, tuwape ushirikiano Kamati ya *PAC* pale ambapo itatembelea katika majimbo yetu, ili kuweza kujiridhisha na matumizi ambayo tumeyafanya na hiyo ndio ambayo itajenga imani kwa serikali kuweza kutuingizia fedha nyengine kwa ajili ya maendeleo ya wananchi wetu.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli wale ambao hawajaipa ushirikiano kamati, kwa kweli hawakutenda haki, kwa sababu fedha ambazo wamepewa zilikuwa ni fedha za serikali, kwa hivyo walipaswa kutoa ushirikiano.

Mhe. Mwenyekiti, nije sasa katika suala zima la utunzaji wa kumbukumbu za mali ya umma. Mhe. Mwenyekiti, ripoti imesema na mimi nakazia tu lakini ni ukweli kwamba baadhi ya taasisi sio zote, kuna matatizo katika suala zima la utunzaji wa kumbukumbu za mali ya umma. Baadhi ya taasisi hazina hata daftari, yaani *fixed asset register*. Kuna nyengine ambazo wanalo daftari lakini halitumiki ipasavyo, lakini kuna wengine wanalo daftari lakini lina makosa mengi ya ujazaji na kuna wengine baadhi ya mali haziorodheshwi. Vilevile, kuna baadhi ya taasisi kutokuwa na hati miliki za mali zake, hii ni hatari Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti, kuna makosa unaweza ukaona kwa mfano, taasisi pengine ina vifaa kama mafeni, lakini katika eneo la

kuweka thamani basi inaandikwa *unknown price*, maana yake hiyo bei haijulikani, sasa sijui feni hili limenunuliwa vipi au meza hii imenunuliwa vipi. Sasa hii inaashiria kwamba kuna ukosefu wa taaluma kwa baadhi ya watendaji katika ofisi mbalimbali.

Sasa nimuombe sana Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango, naona juhudi zake. Hivi sasa taaluma mbali mbali zinatolewa kwa watendaji wa taasisi za serikali kuhusiana na sheria mpya ambazo tumezipitisha mwaka jana. Kwa hivyo, tuendelee kutoa taaluma ili haya makosa mbali mbali yanayohusiana na utunzaji wa mali za umma yanaepukwa.

Mhe. Mwenyekiti, niombe tu kwa vyombo mbali mbali vya serikali ambavyo havina hati miliki za mali zao. Kwa mfano, majengo kuna taasisi mbali mbali hazina hati miliki za majengo, viwanja na mashamba. Sasa utakapoingiza katika *asset register* sijui kitu kile kitakuwa kimehalalika vipi wakati hati miliki huna. Vilevile, hata thamani yake, utakapokuja kufanya tathmini mwisho wa mwaka, sidhani kama utakuwa na uhalisia wa thamani ya mali zako katika taasisi husika. Kwahiyo, niziombe sana taasisi za serikali kuweza kutafuta hati miliki za mali zao, hiyo ndio ambayo itaweza kuweka hata katika *asset register* kuweka ule uthamini wa mali yao.

Mhe. Mwenyekiti, nimalizie katika suala zima la mnyang'anyiano wa vyanzo vya mapato. Ni ukweli usiofichika kwamba hivi sasa tuna tatizo hilo, tuna tatizo la taasisi mbalimbali kuweza kunyang'anyiana mapato au vyanzo vya mapato. Pamoja na juhudi zinazofanyika naomba ziendelee kufanyika kwasababu hali hii itakapokuwa inaendelea, maana yake inawaumiza wananchi, kwa nini inawaumiza wananchi, maana yake mwananchi wa kawaida anaweza akawa anatozwa malipo katika taasisi mbili tofauti.

Mhe. Mwenyekiti, Kanuni za Mamlaka za Serikali za Mitaa ambayo imepitishwa ni kanuni ambayo katika jadweli yake ina vyanzo vingi vya mapato ambavyo vimetajwa, vyanzo hivi vinaiingilia taasisi nyengine, vinaiingilia taasisi za utalii, taasisi za misitu, usafiri na kadhalika. Kwahivyo, kuna haja kubwa sana ya serikali kuongeza *speed* ya kuweza kulirekebisha hili, ili kuweza kuona kwamba mwananchi wa kawaida hatozwi malipo mara mbili mbili na taasisi husika. Hivi sasa watu wa usafiri wanalalamika, ukienda sehemu za maliasili. Kwahivyo, ni vyema sana kusiwe na migongano katika vyanzo hivi na malipo kwa wananchi wetu, tujitahidi sana kuweza kuona kwamba kanuni za sheria mbali mbali hazigongani ili kuweza kuona kwamba tunamfanyia haki mwananchi wa nchi hii. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nilitaka nikazie hayo. Niipongeze kamati na naunga mkono. Pia niwaombe sana Waheshimiwa Wajumbe wenzangu kuweza kuitazame vyema ripoti hii na hatimaye wachangie kwa ajili ya kuisaidia serikali yetu. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti. *(Makofi)*

**Mhe. Mwenyekiti:** Ahsante sana Mhe. Rashid Makame Shamsi kwa mchango wako. Sasa naomba nimwite Mhe. Shehe Hamad Mattar atafuatiwa na Mhe. Hussein Ibarahim Makungu.

**Mhe. Shehe Hamad Mattar:** Ahsante Mhe. Mwenyekiti, na mimi kunipa fursa hii ili niweze kuchangia ripoti ya Kamati ya Kudumu ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali (*PAC*) ya Baraza la Wawakilishi.

Kwanza, sina budi nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uhai na uzima na mimi aniwezeshe ili niweze kuchangia vyema katika ripoti hii. Mhe. Mwenyekiti, nitangulize shukrani zangu za dhati kwa kuwapongeza kamati ya *PAC* kwa kazi kubwa waliyoifanya ya kupitia taasisi zote za serikali pamoja na

mashirika ya umma, ili kuhakikisha kwamba serikali imechukua juhudi kubwa ya kuona mahesabu ya mapato na matumizi yamefanywa kama inavyostahiki sheria.

Mhe. Mwenyekiti, ni kazi kubwa sana iliyofanywa katika ripoti hii na kwa kweli waliyoyagundua humu ni mengi sana. Mimi nasema nayaunga mkono kwa asimimia mia juu ya mia au asilimia mia moja na hamsini. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, kama ingekuwa hakuna haja ya ulazima wa kanuni, basi ningesema hii ripoti siichangii tena inajitosheleza, lakini kwa kuwa kanuni inatutaka na sisi tuichangie ripoti basi tutachangia japo machache, ingawa miongoni mwao wenzangu waliotangulia wameshayasema na ndio kawaida.

Mhe. Mwenyekiti, nianze kwa kusema kwamba haya yaliyogundulikana humu, mapendekezo na maoni ambayo wameyatoa kamati hii ya *PAC* basi naishauri sana serikali iyafanyie kazi, yasibakie kuwemo humu na kitabu kama hiki kuwa ni mapambo tu, ni vyema yafanyiwe kazi ili tija ipatikane.

Mhe. Mwenyekiti, sasa niende moja kwa moja katika masuala hayo madogo madogo ambayo nitachangia kupitia ripoti hii. Kwanza niende kwenye serikali kwa upande wa majimbo. Naiomba sana serikali kutokana na taarifa zilizotokea humu katika ripoti hii kuna umuhimu mkubwa sana serikali kujenga zile ofisi za majimbo, ili kamati hii itakapopita katika kufanyakazi zake, basi iweze kufanyakazi kwa wepesi sana. Tumeona kwamba kamati imepita na baadhi ya kumbukumbu imekosa kuzipata kutokana na kwamba hakuna pahala pa kuzihifadhia.

Mhe. Mwenyekiti, lakini hata makazi, tumemsikia Mhe. Mwenyekiti pale alipokuwa akitoa ripoti yake kwamba wamefika hadi kukaa juu ya mawe na vibao, kama vile waliokuwa kwenye

anga za porini huko. Sio vizuri kamati kama hii inayokwenda pale kikazi kwa heshima na inatoka katika chombo kikubwa kama hiki ikawa hata pakufikia haiko pahali pazuri, hii ni kwamba inakosa umakini wa kuweza kufanya kazi zao kwa utulivu kabisa, yale ambayo walitakiwa kuyatekeleza pale wanaweza wakayawacha na wakafanya kwa kuripua, kitu ambacho sio sahihi. *(Makofi)*

Kwahivyo, naomba sana hizi ofisi za majimbo serikali iweze kuzijenga na kuwawekea watumishi angalau wawili au watatu kwa kuona kwamba wataweza kuzitunza hizi kumbukumbu badala ya kuwa zitatawanyika. Ingawa sasa hivi kuna utaratibu mwengine umewekwa, kuwekwa baadhi ya ofisi hizi za majimbo kumbukumbu zake zikaweko kwenye mabaraza ya miji, lakini huko kwenye Mabaraza ya Miji nina wasi wasi na kumbukumbu hizi zinaweza zikapotea, kwasababu hao waliopewa majukumu huko kwenye mabaraza ya miji au halmashauri na wao wamepewa majukumu mengine utakuta mchanganyiko, hata hizo kazi zao hao makatibu unakaribia kusema hawazifanyi ipasavyo. Kwasababu katibu huyo wa Kamati ya Maendeleo aliambiwa atoke kwenye Baraza la Mji au Manispaa, basi utakuta ana majukumu mengine zaidi kuliko yale, kitu ambacho utahitaji utulivu kuweka kumbukumbu ili zikitakikana ziweze kupatikana. Kwahiyo, ni muhimu sana kuweka ofisi kama hizi.

Mhe. Mwenyekiti, mikakati ya utekelezaji wa shughuli za majimbo kwa kupitia Mifuko ya Jimbo, hili ni jambo zuri sana ambalo kuwa wakati natoa mikakati maalum ifanywe katika majimbo basi isimamiwe ipasavyo.

Kwa mfano, leo Mfuko wa Jimbo umewekwa kwa ajili ya kutatua shida za wananchi, sasa ielekezwe mule mahala ambamo kuwa ni wapi inastahiki na wapi haistahiki kwa mujibu wa sheria. Vilevile, ni jambo la aibu kubwa kuona kwamba kamati kama hii imefika kutaka kuchunguza hesabu, lakini baadhi ya majimbo hayakutoa

mashirikiano. Hapa tunaona majimbo yanayofika tisa aliyoyasema hapa kwa niaba ya mwenyekiti, hayakutoa mashirikiano. Kwahivyo, ni vyema kamati kama hii itakapofika makosa kama haya yasirejewe, na ni imani yanagu kwa vile Chama Cha Mapinduzi ndio iliyokamata majimbo yote kwa sasa hivi, kwa nia safi kabisa watakuwa wanatoa mashirikiano. Ni imani yangu kwamba kamati hizi zitaweza kupata mashirikiano na mambo yote yatakwenda vizuri. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, ni kinyume kabisa na sasa hivi kuiona ripoti humu majimbo ambayo hata mradi mmoja haukuthibitishwa mfano wa jimbo langu la Mgogoni, hakuna mradi hata mmoja kuanzia 2012 ambao umetekelezwa na mwenzangu alopita haukuthibitishwa hii ni kasoro. Kwa hivyo ni imani yangu kwamba sisi tunaoendelea tutalifunga pengo hili tuweze kwenda vizuri kama inavyotakiwa, kwa hivyo tusije tukarejea makosa haya.

Mhe. Mwenyekiti, katika masuala ya huu mfuko wa *CDF* wa majimbo ambao kwa kweli sasa hivi ilitakiwa tutekeleze mambo mbalimbali, naomba Serikali iendelee kuangalia kwamba mfuko ni mdogo tuengeze asilimia ziliopo angalau iwe 25,000,000 lakini naomba sana mfuko huu zilipotolewa pesa mara ya mwisho 20,000,000 kwa majimbo wakati Mwezi wa Juni 2015, Fedha hizi sehemu nyingi sana hazikutumika naoba serikali izifuatilie, izifuatilie kuona zimetendeka vipi. Kwakweli, shilingi 20,000,000 si pesa ndogo na majimbo ni mengi na inavyoonyesha ripoti hizi hazikutumika. Watafutwe wahusika waliopewa fedha hizi na wakati huo walikuwa wanapewa wenye mifukoni ili kuona kuwa fedha ile inarudi, ili ziweze kutumika tena kwa shughuli za maendeleo katika majimbo.

Mhe. Mwenyekiti, niende katika suala zima la kero ya kunyang'anyiana mapato, hapa tumeziona katika ripoti hii, suala

la zima la kunyang'anyiana mapato lipo na ni mfano hai wakati Halmashauri ya Wilaya ya Kusini Unguja.

Mhe. Mwenyekiti, kuna malalamiko kama walivyozungumza wenzangu hapa kuna mfumo wa kunyang'anyiana mapato katika halmashauri lakini tuangalie yule tunaemtoza kodi ile mapato yale ni nani, na ni mwananchi wetu ambae ndie anaetuchangia mapato hayo lakini tunamuumiza, kwa mfano leo mwenye gari anachukua mzigo wa kuni kwa shilingi 500 mzigo huo akamlipe mtu wa misitu shilingi 100 lakini mtu wa halmashauri anataka 300.

Kutokana na hali hiyo, tujiangalie huyu mwenye gari anamapato chungumzima, gari akiitia barabarani ana mapato yanamsubiri yeye na halafu anamatengenezo yanamsubiri yeye, ana dereva, ana mwenye mali anaisubiri shilingi hiyo hiyo tuangalie vyema mfumo huu wa mapato ambao unatozwa na wenzetu hawa kwamba usimuumize sana yule anaechuma yale mapato. Kwakweli, yeye anatumia nguvu zaidi kuliko wewe unaekaaa kwa kwenda kupokea yale mapato. Mapato tunayahitaji lakini tusimuumize anaechuma yale mapato tutakuja kosa yote kabisa kwasababu akiona kwamba hii kazi hailipi moja moja ataweza kuiacha.

Mhe. Mwenyekiti, naomba sana suala hili liangaliwe na ushauri wangu tutizame upya katika masuala mazima ya ukusanyaji mapato katika sehemu zetu zinazohusika, kama vile sehemu zenye mali asili.

Mhe, Mwenyekiti, kuhusiana na masuala ya magari yamewekwa kwenye *garage* binafsi, magari ya serikali. Hili ni kweli naliunga mkono kwamba mara nyingi sana gari zinakuwa zinawekwa za serikali katika *garage* binafsi, hatimaye magari haya ukakuta yanapotea hivihivi, na yanapotea kutokana na kwamba hakuna ule mfumo mzima kwa baadhi ya taasisi uwekaji wa *salary system* ya

*asset register* hii. Kwa mfano, utakuta gari linapotea hivihivi mali ya serikali na fedha nyingi napengine gari ile imwekwa kule *garage* kwa kuondosha *self starter* ambayo haipo, lakini gari ile tawekwa kule yapotee kinyemela nyemela halafu usikie imeuzwa, na mfumo wa mauzo tunaujua ndio huo, gari la 30,000,000 atapewa mtu kwa laki 500,000 hii ni hasara kwa serikali.

Mhe. Mwenyekiti, naomba sana serikali itazame sana kwenye vyombo vyake vinavyohusika kwamba, hivi vifaa hasa vya mfumo wa udhibiti wa mali za serikali katika madaftari yanayohusika unapewa kipaumbele, na unapofika wakati wa mauzo mambo haya yanapewa ile mamlaka nayo inakuwa na uadilifu. Kwahivyo, ile mamlaka inayohusika lazima ifanye uadilifu haiwezekani na haikubaliki kwamba gari la 30,000,000 limewekwa tu pengine mkubwa fulani ameamua kuliweka kulifumbia fumbia macho, halafu ukajasikia gari lile linatembea na kauziwa kwa laki 500,000, ili kuifanyia kinyume serikali ambayo ina nia njema kwa wananchi wake. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, jambo jengine ambalo niliona ni kwa upande wa miradi ambayo imeshapitwa na wakati ilotekelezwa nyuma miradi ya majimbo, iliyofanywa wakati wa awamu zilizopita utakuta kuna majimbo ina miradi iliyoanzishwa na wenzetu waliopita ilitumia fedha za serikali. Sasa miradi hii kama tutaiwacha vilevile bila ya kuiendeleza, tutaona kwamba serikali hatukuitendea haki fedha ya serikali imetumika isisitizwe Wizara inayohusika ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais ifuatilie miradi yote ambayo imetekelezwa awamu zilizopita na haikukamilika basi sisi tulokuwa tunaendelea nayo basi kama bado inatija tuiendeleze. Kwahiyo, huu ndio ushauri wangu, kwasababu kuna miradi ambayo imetumia fedha lakini imedumaa na imeachwa kabisa. Kwahivyo, kama tunaona mradi huu unatija kwa serikali basi uweze kuendelezwa na kutumika kwa wananchi.

Mhe. Mwenyekiti, niende katika masuala mazima ya *parking*. Suala la *parking* kwa kweli nalizungumzia kutokana na kwamba hizi *parking* ziliopo katika nchi yetu zimekuwa wakati mwengine zinaleta bughza, na ni vyema kama walivyoshauri wenzangu kwamba suala hili ni vyema hasa kubinafsishwa. Kwahivyo, ikibinafsishwa suala hili nadhani litakwenda kwa utaratibu mzuri, hakuna atakaekuwa na malalamiko kiasi ambacho yatafanywa kwa uadilifu lakini leo unakuta mambo kila mmoja anakwenda anavyotaka yeye mwenyewe, pahala hata hapana *parking* unaambiwa utoe *parking*. Sasa *parking* kwa ilivyo itayarishwe, lakini hata kama umeweka chini ya muembe unaambiwa ni *parking*, sasa ni *parking* gani hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hivyo halmashauri au *manicpal* inayotaka kutoza *parking* basi kwanza itayarishe hizo *parking* na zijulikane rasmi, isiwe hata kama umeweka gari mara moja unaingia dukani unaambiwa ulipe aa! Nchi hii kila mmoja ana haki, ee! Mapato tunayataka lakini na haki yake mwanachi nae mwananchi aweze kuitumia vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, hili ni jambo ambalo zuri kuona linaendelea hivyo hivyo lazima tulifanyie kazi na mbapo kuwa inaleta tija basi tufanye hivyo.

Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyosema kwamba mimi sina mchango mkubwa kwa sababu hii ripoti inajitosheleza lakini niende kwenye Baraza la Mji Wete. Baraza la mji Wete katika kazi zake hapa upande wa mapato ikusanye 110,000,000, lakini ikakusanya 102,000,000 hivi kwasababu ilivyoeleza humu imejitahidi lakini nasema kwamba moja wapo ni kutokana, tangu uvunjwaji wa soko bila ya kutengenezwa jipya sasa soko leo limerudi, ni imani yangu kwamba nafasi zimo nyingi.

Kwahivyo, ule mtindo wa kuwa soko lipo limetengenezwa kwa gharma mbalimbali, leo utakuta wafanyabiashara wanafanya nje ya soko, utilie maanani kwamba ule sio mpango mzuri, hata kama mtu analipa kodi pale alipo lakini haileti haiba nzuri kwa miji yetu. Wafanyabiashara wote ambao wapo katika maeneo ya soko, basi waingizwe ndani ya soko na mji upate kupendeza sio kila mmoja anafanya sehemu yake anayotaka. Fedha hizi hizi itakuwa wepesi kuweza kuyadhibiti mapata lakini kuona kwamba utaratibu wa miji yetu unakaa vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, hili ni moja ambalo nilikuwa nataka nilisema na kwasababu naona muda ushakuwa tayari, nakupongeza asilimia mia moja ya ripoti hii, naunga mkono. Nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii. *(Makofi)*

**Mhe. Mwenyekiti:** Ahsante Mhe. Shehe Hamad Mattar kwa mchango wako. Sasa naomba nimwite Mhe. Hussein Ibrahim Makungu na atafuatiwa na Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi na Mhe. Yussuf Hassan Iddi ajiandae.

**Mhe. Hussein Ibrahim Makungu:** Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kunipa nafasi hii, awali ya yote napenda kumshuku Mwenyezi Mungu, katika kikao chako hiki kitukufu kuchangia hoja ya hii nzito katika nchi yetu. Lakini pongezi sana ripoti ya Kamati ya *PAC* ya kudumu ya Kuchunguza Kudhibiti wa Hesabu za Serikali na Mashirika ya Umma. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, niwapongeze kwanza Mwenyekiti wa Kamati hii na wajumbe wao wote kwa kazi yao nzuri, kutuletea hii ripoti kubwa sana na ina mambo mengi sana. Lakini pia niipongeze serikali kwa kazi yake nzuri walioifanya katika ripoti hii mbali ya mapungufu madogo madogo lakini kwa kweli niwapongeze sana Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa juhudi zake kubwa sana katika kazi zao wanazozifanya katika ripoti hii.

Mhe. Mwenyekiti, nianze hapa katika ripoti hii, katika miradi ya majimbo hasa katika hizi fedha tunazopewa sisi Wawakilishi katika miradi yetu ya majimbo kila baada ya muda. Lakini nisisitize ripoti ilivyosema Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli tangu Bazaza hili lianze nimepewa fedha mara moja, kitu ambacho kinaumiza sana, tofauti na wenzetu Wabunge kama walivyoswema wenzangu wamepewa fedha kama mara tatu, na washapewa na mara ya nne.

Kwakweli, fedha hizi zinasaidia sana hasa katika majimbo yetu na maendeleo mengi tunafanya, ukiachilie pesa ni kidogo kwa changamoto za majimboni lakini zinasaidia, lakini sasa mimi naomba hizi pesa tuwe tunapata kila baada ya muda haraka haraka ili tuweze.

Mhe. Mwenyekiti, niseme ripoti hii kama wenzangu walivyosema inaeleza ripoti ya 2012 mpaka 2015, hamna ya 2016, wala 2017 na hizi fedha ambazo zinatakiwa sasa hivi kuangaliwa ni fedha ambao tumepewa mara ya mwisho ambazo hazimo ripoti yake, lakini niseme.

Mhe. Mwenyekiti na ukiangalia ripoti hii haya majimbo Mhe. Mwenyekiti yamegawiwa, sasa hivi utakuta jimbo nusu limekwenda huku na nusu limekwenda huku. Kwa mfano, mimi nilikuwa Jimbo la Bububu lakini sasa nimekwenda Jimbo la Mtoni, nusu limekwenda Mtoni nusu liko Bububu. Kwahivyo, miradi mtu akingali hapa mengine ya Jimbo la Bububu ambyo ishapita, sasa hivi hatuhusiki na jimbo lile. Miradi iko huku sasa naomba sana wakaguzi wanapokwenda waangalie jimbo husika, kwasababu wamebadilika hasa wale wajumbe wa kamati, katibu nae kabadilika kaja mpya, wazamani yuko huku, wengine hawapo kabisa kwenye shughuli hizi .

Kutokana na hali hiyo, naomba waangaliwe wahusika halisi wa hawa, kwasababu hapa kuna ripoti nimeona kuna jimbo wamekwenda la Nungwi hawajawapata wahusika, sasa pengine wahusika waliokuwepo ni wengine, wanaotafutwa ni wengine. Kwahivyo, naomba sana waangalie muhusika hasa Mwenyekiti wa Kamati hii anakuwa ni Mwakilishi. Hivyo ni vyema atafutwe atoe *introduction* kwa wajumbe wake na maelezo, ili wajue nani na nani anahusika na miradi inayofanyika.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu huu Mradi wa *Terminal*. *Terminal II Airport* tukiangalia kwenye ripoti sijaona, lakini tuseme mradi huu ni muhimu sana. Mhe. Mwenyekiti, niipongeze sana serikali kwa juhudi zao kubwa ile *Airport* imepoteza pesa nyingi sana hapo nyuma, lakini sasa hivi inakaribia kwisha, naamini *Airport* ile ikisha *Terminal II* itasaidia kuongeza sana mapato yetu, ukiangalia maduka, ukiangalia ndege za kisasa zitatusaidia zaidi, abiria watakuwa wengi zaidi. Kwahivyo, niipongeze serkikali ifanye juhudi haraka haraka *Airport* ile imalizike, ili mapato pia yaongezeke kwa asilimia fulani ili kuweza kuongeza mapato ya nchi yetu na kupitia *Terminal II* hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, katika haya masoko yetu kama walivyosema wenzetu kwenye ripoti hii Manispaa sasa hivi wanakusanya kodi na fedha nyinyi wanakusanya karibu bilioni ngapi wamekusanya na mambo mengi lakini niwapongeze sana Manispaa.

Mhe. Mwenyekiti, Lakini ukitazama mfumo wao wakusikitisha wanachukua risiti za kawaida hasa ukipaki gari eneo la Malindi pale, Bank, *Manispal* yote, Darajani mpaka Mkunazini huku, Forodhani, na eneo lote la Mjimkongwe, fedha nyingi wanakusanya lakini sasa upande mwengine wanatoa risiti hizi za kawaida, vikaratasi wanakuchania wanakuandikia.

Mhe. Mwenyekiti, ukitazama wenzetu wa Tanzania Bara, Dodoma, Mikoa mingi sasa hivi wanapewa zile mashine za *electorinic* wanakuchania pale pale inakuwa ile pesa *automatic* inaingia katika mfuko wa serikali. Kwahivyo, naomba sasa tutafute zile mashine za *electronic* ili yule mtu anapolipa asipewe risiti ya mkono kuandikiwa apewe *electronic* risiti kabisa, kwa hivyo itasaidia kuengeza mapato makubwa katika nchi, kwa sababu kila unapokwenda sasahivi unalipa shilingi 1,000 ukiweka dakika 10 shilingi 1,000 wananchi wanalipa. Hivyo, tunaomba mapato haya yazingatiwe, ili yaweze kupatikana na kuangalia mambo mengine.

Mh. Mwenyekiti, katika *Bank* yetu ya *PBZ* kwanza kabisa naipongoza sana kwa kazi yao nzuri, wateja wengi wanao, kwasababu sasa hivi ukitizama fedha za serikali zote, wafanyakazi wote wanapitia *PBZ* kulipa na lakini ukifika mwisho wa mwezi watu wanakuwa wengi hata hapaingiliki pale benki.

Kwahivyo, nasema wateja wanao wengi na shukuru wananchi wanaikubali benki yao na wanaweka pesa zao nyingi. Lakini ukitazama huduma moja hamna mpaka leo ambao *Bank* kama *NMB*, na benki nyengine wanazo, na mimi pia ni mteja wa *NMB*, juzi tu nilikuwa Beijing China karibu mwezi mzima, nilikuwa natumia *Visa Card*, ambayo *Visa Card* hiyo ukipeleka pale ukitaka kutoa au ukitaka kutumia chochote huduma ile inafanyakazi haijawahi *Visa* hata moja ya *NMB* ku-*bounce* au kuwa tatizo katika nchi. Sasa naomba na *PBZ* nayo itowe hizi *Visa Card* nimetumia pesa nyingi sana kwenye kutia *Visa Card*. Nawekewe pesa huku mimi natumia kule bila shida yoyote.

Mhe. Mwenyekiti, huduma ilikuwa nzuri sana, nawapongeza sana *NMB* kwa ile *Visa Card* yao ya *Titanic*, nawashukuru sana imefanyakazi vizuri sana. Kwahivyo, nawaomba na *PBZ* mfumo huu wautumie watu wanasafiri wanakwenda kila pahali. Kwa

mfano, hivi sasa unajua huwezi kusafiri na pesa, ukitoka sasa hivi na dola 10,000 tu inakuwa shida, lazima ujaze fomu na ikizidi tu huwezi kutoka nazo.

Kwahivyo, mfumo huu wa *Visa Card* ni muhimu kwa wananchi wetu, sasa benki yetu ya *PBZ* bado na juzi nimewauliza mnayo *Visa Card*, wakaniambia bado. Mhe. Mwenyekiti, naomba sana serikali iangalie suala hili la *Visa Card*, ili wateja wao waweze kufaidika na hii huduma ya *Visa Card*. Lakini ukitizama pia benki yetu ya *PBZ* sio benki ya kibiashara sana, ukienda kwenye benki nyengine kama hizi za *NMB* wanakuomba wewe uchukuwe mkopo ufanye biashara, wanakulazimisha uchukuwe mkopo kwa masharti nafuu kabisa, lakini *PBZ* ukienda masharti yao yanakuwa ni makubwa sana.

Sasa naomba sana tuangalie sasa hivi mfumo wa biashara, kila mwekezaji sasa hivi wa pesa benki ni lazima umkopeshe, ili aweze kuweka fedha kwenye benki na unapata faida kubwa, riba unamkata na faida kila akitoa pesa akiweka mnamkata. Kwahivyo, ni lazima wafanyabiashara muwavute, ili benki yetu hii ya *PBZ* iweze kuwa na wateja wengi. Ukiangalia benki yetu sasa hivi ya *NMB* ina wateja wengi sana, hata ukienda Dar-es-Salaam, ukienda Dodoma na sehemu mbalimbali *NMB* ipo imejitanua sana. Kutokana na hali hiyo, nawaomba na *PBZ* pia ijitahidi sana katika masuala ya kibiashara, ili iweze kuwasaidia wananchi wetu.

Mhe. Mwenyekiti, nije kwenye suala la kodi kwa hawa wenzetu wa *TRA*. Kwakweli, niwapongeze sana kwa juhudi zao kubwa wanajitahidi sana, lakini ukiangalia sasa hivi kipindi cha nyuma hapa tu, mimi sina gari ya usafiri ya biashara, lakini naangalia wananchi wanalalamika sana kwa daladala, wanaokuchukua watalii pamoja na wengine, wanasema kodi ilikuwa mwanzo kulipa ni shilingi 300,000 kusajili gari yako kufanya biashara,

lakini sasa hivi imekwenda mpaka shilingi 800,000 kwa kupitia *ZRB* wenzetu wanakusanya kodi hiyo.

Kwahivyo, naomba tuangalie na hali za wananchi wetu, mwanzo ilikuwa shilingi 300,000, lakini sasa hivi imepanda sana wananchi wanasikitika sana, wanasema kodi ni kubwa sana shilingi 800,000 kwa mwaka kuisajili gari yako kufanya kazi ya abiria.

Mhe. Mwenyekiti, tutizame na hali ya mazingira wananchi wetu na biashara ilivyo, kwa kweli hizi fedha ni nyingi na gari ina gharama kubwa kuna mipira ubadilishe, kuna *service* na mambo mengi yanataka kufanywa ili yule mwananchi apate kipato chake, riziki yake apate kwa ajili ya familia yake, lakini pia na gari atengeneze na kodi alipe, kwa hivyo inakuwa mwisho wa siku apati faida. Kwahivyo, naomba sana hii kodi tuangalie sana serikali, sasa hivi *ZRB* wanavyokusanya watizame kidogo hali ilivyo waweze kupunguza kodi hii ili wafanyabiashara wetu waweze kufanyakazi zao vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, suala hili la *TRA* hawa wakusanya kodi wa bidhaa kutoka nje. Nawapongeza wanafanyakazi vizuri sana na Kamishna wetu mpya nampongeza sana kwa upendo wake na kwa imani yake, hata yale mapokezi yake ukienda ni mazuri ya kibinadamu makubwa sana, mimi nampongeza Kamishna wetu mpya wa hapa Zanzibar kwa jitihada na maelekezo yake mazuri, kila kitu anakupa mpaka unaridhika. Wafanyabiashara wanamshukuru sana wanampenda na wana imani kubwa kwake yeye.

Kwahivyo, niseme haya mapato wanayokusanya *TRA* sasa hivi wamevuka hata malengo ya fedha ambayo wamekusudia, ukiangalia kwenye ripoti ya kamati na mambo mengine. Mhe. Mwenyekiti, napongeza, lakini tukiangalia wananchi wetu wanaleta bidhaa hapa wanaingiza wanalipa kodi hii, wakishalipa

wanataka wengine kusafirisha kupeleka Bara pia bidhaa hiyo hiyo, ukitizama Bara wakienda wanalipishwa tena kodi pale Bandarini.

Mhe. Mwenyekiti, sasa ile faida yao inapungua sana. Sasa tuangalie sana hizi kodi wanaokusanya wenzetu hawa wa *TRA* ni nyingi. Sasa watizame kama kuna uwezekano wa kupunguza zaidi kodi hii basi ipunguzwe kwa bidhaa zinazoingia Zanzibar ili izidi kuwa rahisi. Kwa sababu sasa hivi ukiangalia Mhe. Mwenyekiti, kuna kitu unanunua Dar-es-Salaam rahisi lakini Zanzibar ghali. Kwa nini iwe hivi na mwanzo ilikuwa Zanzibar ndio soko ambalo kama ndio maeneo huru ya Zanzibar ni hapa, gari rahisi, nguo rahisi na kila unachotaka Zanzibar rahisi. Leo wenzetu soko lao linakuwa rahisi zaidi kuliko hapa. Kwa hivyo, tuangalie hizi kodi na wafanyabiashara wanataka faida, sasa kodi ikiwa kubwa na bei wanaongeza. Maana yake kuna *VAT, ZRB,* kuna kodi ya bidhaa. Kuna kodi tatu kwanza ulipe halafu ndio uuze biashara ile.

Kwa hivyo, naomba sana tuangalie *TRA* inapoingiza kodi wananchi wetu kidogo tuwafanyie nafuu ili soko liwe Zanzibar kwa ajili ya vitu vyote viwe rahisi, na watu waje hapa kununua hivi vitu na wananchi wetu wanategemea hii biashara kwa ajira yao ni kubwa kwa Zanzibar. Hiki ni kisiwa, hapa ni karafuu, utalii na biashara hakuna chengine. Sasa tukiwafanyia kidogo nafuu, naamini ajira itakua kwa wananchi wetu hawa ili waweze na wao wanafanya biashara. Mhe. Mwenyekiti ukiangalia huku na huku mapato wanayokusanywa na *TRA* ni makubwa na ukitizama pato la nchi hii asilimia thelathini wanalipa hawa wafanyabiashara wanachangia kwa hiyo tukiwapunguzia naamini watakuwa wengi zaidi kuleta.

Mhe. Mwenyekiti, ukiangalia sasa hivi biashara mzigo kutoka Dubai au China ama Hong Kong kote ukitia katika kontena Zanzibar ni ghali kuliko Tanzania Bara, unaambiwa Zanzibar pesa

nyingi kuliko huku Dar-es-Salaam au sehemu nyingine kwa hivyo naomba ishuke hii kwa sababu sasa hivi mzigo mwingi unashuka Dar-es-Salaam huku watu wamepunguza kidogo. Kwa maana hiyo, sisi tunategemea mapato pia mwisho wa siku kulipana mwisho wa siku kulipana mafao yetu, mishahara yetu na ajira kwa wananchi wetu. Kwahivyo, naomba sana *TRA* iangalie kiundani wanaweza kupunguza hali gani ya kupunguza kodi wafanyabiashara wetu ambao wanakazi kubwa, kwakweli nasikitika sana nawaonea huruma kwasababu mzigo huu huu baadaye wanakwenda kupeleka Dar-es-Salaam na kule wanalipishwa kodi kwa hivyo hali inazidi kuwa ngumu kidogo.

Mhe. Mwenyekiti, jambo jengine katika mgao wetu wa *BoT* wa 4.5% mimi niishukuru Serikali yetu ya Jamhuri ya Muungano ya Tanzania pamoja na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, hivi sasa mgao tunapata vizuri mafao yetu tunapata vizuri kutoka muungano. Kwahivyo, niipongeze sana mgao huu tunapata bila ya muungano mafao haya yasingepatikana. Mhe. Mwenyekiti, nawaomba wananchi waamini kabisa muungano una tija kubwa kwetu sisi kwa mapato haya ya 4.5% ukiangalia hata kwenye Bunge la Katiba tulisema sana kwenye suala hili, lakini sasa hivi mambo yanakwenda vizuri. Kutokana na hali hivyo, tushukuru na wananchi waelewe umuhimu wa muungano huu, naomba tuuheshimu na tuuenzi tusiwe tunakaa tunaubeza kila siku, lakini kuna mapato hapa 4.5% inapata serikali yetu. Kwakweli, hili ni jambo la kupongezwa na nishukuru sana.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea na mchango wangu sasa nizungumzie hospitali ya Kikosi cha KMKM, ambayo iko kwenye jimbo langu. Kwakweli, ile hospitali ya KMKM wagonjwa wa sehemu mbalimbali wanakuja pale kutoka shamba kwenye jimbo langu na sehemu nyengine. Kwakweli, niwapongeze sana hawa

vikosi wanafanya kazi usiku na mchana kazi kubwa sana ya kutumikia wananchi wetu kwa ajili ya huduma ya afya.

Lakini ukiangala pia wana changamoto nyingi hawa ndugu zetu, ukienda pale wakati mwengine dawa pia inakuwa hamna japo wanauza lakini kwa bei nafuu sana, dawa bei nafuu faida yao ni ndogo sana, lakini kubwa wanatoa huduma kwa wananchi wetu na mimi niseme madaktari hao wako makini, hodari na wananchi wanawasifu kwasababu mimi ni mwakilishi lakini napata sifa zao wananchi wanafurahia sana huduma zao pale.

Mhe. Mwenyekiti, nawapongeza na Mwenyezi Mungu awazidishie na hospitali yao iwe kubwa sana kwa ajili ya kutumikia wananchi, kwasababu mafanikio makubwa ninayoyapata mimi kwenye jimbo langu pale bila ya mtu kwenda mjini anakwenda pale anasaidiwa sio jambo dogo nishukuru sana, ingekuwa haipo hospitali ile pale mimi mwenyewe ningepata shida kwenda sehemu ya mbali, lakini sasa hivi nashukuru.

Mhe. Mwenyekiti, ukiangalia kwenye manunuzi haya kuna taratibu za manunuzi, wakati mwengine wale wanakusanya pesa hawa KMKM madaktari na huduma ya pale wote wasimamizi. Lakini wanataka kununua dawa kutoa hizi pesa pengine *emergency* sasa utakuta wanatoa zile pesa nyengine, lakini utakuta huku kwenye sheria za manunuzi ni kosa kwasababu hujaandikia ripoti au hujataka kutoa taarifa mwanzo, sasa unaweza kukuta wakati mwengine wakatumia fedha hizi kwa *emergency* lakini ikaonekana kama wamefanya hujuma fulani.

Kutokana na hali hiyo, naomba sana tuangalie sana sheria hizi na wenzetu wa huduma hii ya afya wanaweza kutumia pesa hizi wakati wowote kwa ajili ya kununua dawa na vitu vyengine kutibu wagonjwa. Kwa mfano, inaweza ikatokea *emergency* pale za ajabu ajabu na wanatakiwa wakifanya wafanikiwe. Kwahivyo,

wanaweza kuonekana wamevunja sheria lakini sio lengo lao. Kwakweli, nasema wana kazi yao nzuri na nawapongeza kwa juhudi zao kubwa sana hawa ndugu zetu. Sasa tuangalie sana ripoti ilivyoandika hapa kwa manunuzi na sheria za manunuzi lakini wanaweza kidogo kwenda upande kwa ajili ya *emergency* yao inavyotokea. Kwahivyo, nawapongeza na nawashukuru.

Mhe. Mwenyekiti, nije kwenye suala la polisi. Polisi ni suala la muungano tunajua...

**Mhe. Mwenyekiti:** Mhe. Mjumbe, zimebakia dakika mbili.

**Mhe. Hussein Ibrahim Makungu:** Haya ahsante. Lakini Mhe. Mwenyekiti, suala la polisi wakati mwengine polisi hawa wetu wanakuwa hata mafuta hawana. Sasa, naomba serikali kujua inawasaidiaje polisi wetu hasa kwenye mambo ya *emergency* kwa suala la mafuta na serikali yetu inawasaidiaje. Hivyo, naomba tuwasidie kwasababu wakati mwengine wanakuwa na shida kubwa na wao wanatakiwa kuitekeleza.

Mhe. Mwenyekiti, nije kwenye suala hili la taarifa ya Meli yetu ya Mapinduzi II. Nisikitike sana *PAC* hawajaandika taarifa ya meli hii. Mhe. Mwenyekiti, mimi nilisema jana hapa nilikuwa kwenye Baraza hili na mimi nilikuwa Mjumbe wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi, wenzangu walikwenda kununua meli ile mpaka Mkuku alikwenda kuweka Mwenyekiti wangu wa kamati Mhe, Mahamoud alikwenda Korea, mimi nilikuwa niende lakini sikubahatika kwenda. Lakini ile meli ni mpya imenunuliwe na waheshimiwa wamekwenda na mwenyekiti wangu wa kamati na picha tumeziona, lakini ile meli imefanya kazi vizuri tu hapa kipindi cha katikati juzi juzi ndio imeharibika.

Sasa kwa taarifa ninavyozisikia chini chini wanasema kwamba imetiwa mafuta machafu imeharibika ni *sabotage*. Mhe.

Mwenyekiti, jana ripoti ya kamati imesema ya Mhe. Hamza Hassan Juma hapa wazalendo wapewe meli ile washughulikie kuna watu hawana nia njema kwenye meli ile. Kwahivyo, naomba ripoti kama hii ya *PAC* ichunguze wale wafanyakazi kwanza wanaofanya mule walikuwa na nia njema na meli ile? Kwasababu fedha nyingi tumetumia hapa tuoneane huruma fedha nyingi sana serikali imetumia karibu dola milioni thalathini tumetumia kwenye meli ile. Kutokana na hali hiyo, naomba sana wachunguzwe kwanza wale kama wana matatizo wachukuliwe hatua haraka sana. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nije kwenye mradi wa maji haraka haraka. Katika mradi wa maji huu *Ras-al-Khaimah* wamechimba visima karibu 150 katika nchi hii, lakini Mkoa wa Mjini Magharibi tu visima 50 na mimi nilikuwa mjumbe wa kamati kipindi kile visima 50 zimekwisha, lakini katika 50 vinafanya kazi vinne tu kwa nini Mhe. Mwenyekiti, kila siku tunakuja hapa shida ya maji, nilijua baada ya miaka mitatu shida ya maji Zanzibar imekwisha, lakini kwa bahati mbaya shida ya maji inaendelea. Huko jimboni kwangu shida ya maji chemchem iko pale lakini maji hamna Mwanyanya maji hamna. Kwakweli, nasikitika sana visima hivi vinne vinafanya kazi Kamati ya *PAC* ilikuwa ichunguze mradi huu wa *Ras-Al-Khaimah* na visiwa vyote au vinafanyiwa *sabotage* maji yasipatikane? Kwahivyo, naomba ripoti iseme ichunguze na ilete hapa itwambie kwanini maji hayapatikani.

Mhe. Mwenyekiti nasikitika sasa hivi *ambulance* yangu imekuwa ndio inapakia maji kupeleka kwa wananchi juzi nimeona madumu ya maji yamepakiwa kupeleka kugawa badala ya kupakia wagonjwa inapakia maji kutokana na shida ya maji ilivyokuwa kubwa. Sasa visima hivi vya kazi gani *Ras-Al-Khaimah* imetusaidia wamefunga *pump* wamefunga matenki mimi nilikuwa mjumbe wa kamati napitia kila siku kwenye visima vile mpaka leo havifanyi kazi kuna tatizo.

Kutokana na hali hiyo, lazima tuunde kamati teule kama alivyosema Mhe. Machano Othman Said ichunguze kwa undani hivi hii *ZAWA* kuna wafanyakazi wanafanya *sabotage* humu? Kwa nini visima hivi, mimi nna kisima changu nyumbani kwangu huu mwaka wa tatu hakijawahi kuharibika *pump* wala nini sasa nashangaa leo wananchi maji visima vikubwa kama vile vina uhakika wa maji yaani, vina maji mengi, lakini maji hamna.

Mhe. Mwenyekiti, nikushuru kwa kunipa muda wako na kuniongeza kidogo lakini niishukuru kamati na niunge mkono asilimia mia kwa mia kwa kazi yao nzuri na kwa ripoti hii. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti nakushuru. *(Makofi)*

**Mhe. Mwenyekiti:** Nakushuru sana Mhe. Hussein Ibrahim Makungu kwa mchango wako. Sasa naomba nimwite Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi atafuatiwa na Mhe. Yussuf Hassan Iddi na Mhe. Omar Seif Abeid ajiandae.

**Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi:** Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti kwa kunipa fursa hii, nilidhani kwasababu ni Mjumbe wa kamati hii sitopata nafasi, lakini kwa imani yako umenipa nafasi hii na mimi nichangie nakushukuru sana.

Kwanza kabisa bila ya kujipendelea au kupendelea kamati napenda niipongeze sana hii kamati kwakweli imefanya kazi kubwa, ni kamati ambayo shughuli zake ni *cross cutting* yaani, wizara zote na sehemu zote zinahusika na matumizi ya fedha za serikali. Kwakweli, kazi zetu za kamati hii zina matatizo yake ni muhimu sana lakini zina matatizo yake kwasababu unaekwenda kumchunguza kwa suala la fedha usitegemee kwamba atafurahi hata kama hajafanya kosa huyo hatafurahi, kwasababu matumizi siku zote yanaandamana na kitu kama sijui kama kweli nitakuwa nimefanya ndivyo au sivyo, matokeo yake wachunguzi wanaanza

kupewa majina hao mashawishi, hao sijui maaskari hao sijui nani majina mengi tu. Lakini, kamati imeweza kuzifanya kazi hizo kwa ufanisi na leo hii kuna kitabu kikubwa kabisa kimeweza kutayarishwa na kusambazwa. Kwahivyo, nimpongeze sana Mwenyekiti wetu wa kamati hii, kwa umahiri wake na busara zake tumeweza kufikia hapa tulipofikia na bado tunaendelea kwasababu majimbo bado yapo mengi na wizara bado zinaendelea kutumia kwahiyo tutaendelea.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza nizungumzie juu ya Mfuko wa Jimbo. Mfuko wa Jimbo, kwa kweli ni muhimu sana majimbo yana matatizo mengi sana, na nitatoa mfano wa jimbo langu ni jimbo lenye milima miteremko, *nature* yake ni ya miteremko na kwasababu tupo karibu ya msitu wa Masingini hata mvua zinaponyesha zinakuwa kubwa na maporomoko yanakuwa makubwa, leo hii tengeneza barabara kwa fedha zote kama hujawekea lami ukaweka miundombinu inayotakiwa kesho ikinyesha mvua wala huwezi kuamini kama ile barabara imetengenezwa. Kwahivyo, tunashauri sana Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo utizamwe sana, kwani matatizo ya jimboni ni mengi, hivyo hizo fedha za Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo basi ziharakishwe zipatikane, ili tuweze kuzitumia na kuleta maendeleo katika majimbo. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, jengine ambalo nataka nilizungumzie ni kuhusu hizi fedha. Kwakweli, fedha zina mambo mawili matumizi na mapato yaani, uzipate na uzitumie, hayo ni mambo makubwa sana ambayo yanatakiwa. Kwanza kabla sijasema kitu nashauri Wizara ya Fedha na Mipango iwapate wafanyakazi ambao ni *specialist* wa fedha, *financial managers* au *financial management* wawepo kwa wingi sana, ili namna ya matumizi ya fedha yaweze kwenda vizuri zaidi. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nikianza na mpango wa matumizi, ni kwamba matumizi yoyote lazima yaende kwa *plan* bila ya *plan* huwezi ukatumia fedha inavyotakiwa na *plan* hizi lazima ziende kwa mujibu wa taratibu za serikali zilivyowekwa. Sasa tumegundua katika sehemu nyingi sana taratibu zile za kifedha hazitumiki vile ipasavyo na wenzangu wameshasema hapa, hakuna *procurement plan* kwa baadhi ya sehemu ambayo inaeleweka, hakuna *action plan* kwa baadhi ambayo inaeleweka matatizo yake kunakuwa na *inconsistance* ukienda kwenye *action plan* inasema vingine ukienda kwenye *procurement plan* inasema vyengine.

Mhe. Mwenyekiti, watu tunawapeleka masomoni, lakini hakuna hata *training program* utaambiwa tu akiomba mtu anapewa kwa mujibu anavyotaka yeye mwenyewe. Kwahivyo, ni vizuri tukawa na *training program* tukajua tunahitaji wataalam wa aina fulani kiasi gani, kwa miaka mingapi tuwapate hao tukaenda kwa mujibu wa ile *plan* ambayo tumeipanga.

Mhe. Mwenyekiti, pamoja na yote hayo ili kila mara ujirekebishe na *plan* zako hizi basi lazima ufanye utafiti, na utafiti si lazima sijui ukafanya ile *intensive research*, unaweza ukafanya kwa kuandaa *questionnaire* ukapita makazini humo ukawauliza zinaitwa *job satisfaction assessment.* Ukizifanya zile unaweza ukagundua mambo mengi ukaweza kupata *recommendation* ukabasilisha mifumo ambayo ipo ukaweka ile inayofaa. Kwahivyo, tunashauri pia *research* zitiliwe mkazo kwa maana sehemu nyingi tulizokwenda utakuta matumizi utakuta matumizi yame *base* kwenye mambo mengine tu lakini kwenye tafiti matumizi hakuna, wakati mwingine hata kwenye hiyo bajeti haiingizwi.

Mhe. Mwenyekiti, jambo jingine ambalo napenda kulizungumzia ni *budgeting* sasa, mwenzangu pale kazungumza bajeti kasema kwamba bajeti zinazofanywa pamoja na kwamba tunahimiza watu

wafanye *PBB* (*Program Basic Budget*), lakini bado ni ileile mtu anaambiwa akafanye bajeti anakwenda anakaa anatizama mwaka jana kafanya nini anaongezea kidogo, basi inakuwa ni bajeti. Tunashauri pia ifanyike *Program Basic Budget*, ili ujue mapato halisi kwa mujibu wa *program* yatapatikana kiasi gani ujue matumizi halisi kwa mujibu wa *program* yatakuwa kiasi gani hii itaturahisishia kuweza kujua kwamba tutapata kiasi fulani na *exactly* tutapata hicho ambapo mipango yetu tutakuwa tumeipanga kwa fasaha zaidi kuliko kubahatisha bahatisha.

Kwahivyo, bajeti zetu siku zote nadhani ziwe *smart*, na tulipokuwa tunafika huku tulikuwa tunasema sana, tunasena tufanye *smart budget* kwa sababu hizi ni *Program Basic Budget* basi ziwe *smart*. Sasa tafsiri ya *smart* naweza kusema tu kwa ufupi iwe *Specific, Manageable, Accurate*, *Relative*, *Timebound*, maana yake hiyo, ni kwamba ukiweza kufanya *smart budget* ndipo hapo utafanya matumizi *smart* vilevile na utaenda vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, jambo jingine nakwenda haraka haraka kwa sababu muda hautoshi jambo jengine ambalo tumeliona ni *documentation*. Kwakweli, *documentation* haziendi sawa kwa baadhi ya sehemu mwenzangu hapa kagusia mambo ya *asset register* yaani, *asset register* siyo kamili tunatakiwa tuwe na *asset register* ya mali zote za serikali na katika *asset register* hilo basi iwepo ile *depreciation* ifanyike *depreciation* mwaka huu pengine kitu kitakuwa na thamani kiasi fulani, mwakani kitakuwa na thamani kiasi fulani kwa kufanya hiyo *depreciation*.

Sasa hiyo *depreciation* hatuwezi kila mtu akafanya yake Wizara ya Fedha na Mipango ni vizuri itoe *recommendation* kwamba tunatumia *linear* lakini na watu pia wafahamishwe hiyo *linear depreciation* kwa kutumia *linear method* ina matatizo gani ili waweze kujua na waifanye kwa ufasihi zaidi, maana yake *depreciation method* unaweza ukenda usipo kwenda vizuri miaka

mitano utakikuta chombo au kitu kina thamani ya *zero*. Kwahiyo, kama huwezi ukairekebisha hiyo *linear depreciation* yako unaweza ukavitoa thammani vitu vipya bado vina nanii kwa hi vyo, yafanyike marekebisho kila mara *revaluation*, ili hiyo *linear depreciation* ifanyike kwa ufasihi zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea na mchango wangu wenzangu wamegusia kwamba kuna vitu havipo kwenye *documentation* kuna *inventory register* nayo hiyo inaruhusu watu waweze kuweka vitu vyao kwenye *inventory* ambayo inajulikana mali fulani ni mali ya serikali.

Vilevile, jambo jengine tulililoliona ni kuhama mtu akahama na vyombo vya sehemu ile, si vibaya ni vizuri sana lakini ni vizuri unahama nenda kule unakokwenda utakikuta kitu kama hicho kama hakipo kafanye mipango ukipate kile cha pale waachie walewale waendeleze kwasababu kimekusudiwa kupelekwa pale kwa matumizi ya pale. Kwahivyo, nishauri kwamba tunapohama kama hakuna ulazima basi ni bora vile vyombo vinavyohusika pale tuviache pale.

Mhe. Mwenyekiti, halafu kuna mambo ya *store ledger* hakuna stoo na kwa hivyo hakuna *store ledger*, kwahivyo utavikuta kwenye *corridor* tu vimewekwa au kwenye chumba fulani vimewekwa basi havina hata *documentation* ndani yake kwamba kuna kitu fulani na fulani hata ukitaka huwezi kupata. Kwahivyo, na *store* nayo store ziwepo na *store ledgers* ziwepo, ili kuweza kuweka mambo vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, sasa kuna sehemu ya mikataba *contract* mikataba mingi ambayo tumeiona haiko kamili, iko kienyeji zaidi kuliko kisheria zaidi utakuta mkaba hauna saini lakini umeshatumiwa umeshatiwa pesa umeshafanywa kila kitu baadhi ya *signatures* pengine hamna au hakuna saini kabisa. Kwahivyo,

na hiyo mikatabata tunaomba ifanyike kisheria ikilazimika basi wahusishwe wanasheria waifanye mikataba hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, jambo jengine ambalo ningependa kuligusia katika haya ni kwamba katika uchunguzi wowote wa fedha za umma kuna kitu kinajitokeza cha ubinaadamu ambayo hiyo tunaijali sana sisi, tunajali sana ubinaadamu. Lakini sasa inapofika kiwango ambacho ni kibaya ule ubinaadamu kidogo unaweza ukafata sheria zaidi ukashau kwenye ubinaadamu. Kwahiyo, tunawaomba sana wale ambao wanakaguliwa wajaribu sana kujitayarisha, wajitayarishe kama kuna makosa waweze kuyarekebisha mapema, ili wakati wa ukaguzi matatizo yale madogo madogo yasitokee yakaja yakaingiza kwenye hatia. Unaweza ukaingia kwenye hatia kwa matumizi ya fedha haya, unaweza ukaingia kwenye hatia huna kosa, lakini kwasababu jambo hilo limetokea wewe upo hapo aa! Utawajibika.

Kwa mfano, inawezekana matumizi hayo umetumia kidogo kidogo senti tano leo kesho pangine shilingi kumi, kesho kutwa elfu moja mwisho wa mwaka unakuta mamilioni yameshapotea matokeo yako unaingia umepoteza milioni huhesabiwi tena kama umepoteza senti tano tano unahesbiwa umepoteza milioni. Kwahivyo, tunaomba sana wawe waangalifu sana wenzetu, ili hizi sheria za fedha zitumike vizuri katika kutekeleza majukumu. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kusema hayo nasema napendekeza kwamba yote haya yaliyoingizwa humu kwenye ripoti yetu hii mapendekezo, maoni na mambo mengine mengine tunaomba yafatwe ili tuwe na utaratibu bora kwa matumizi ya fedha za serikali. Baada ya kusema hayo kwasababu yaliyosemwa yote tumefanya sisi tunayajua yaliyosemwa yote hatuna haja ya kuyaeleza mengi, isipokuwa nakushukuru tena kwa kunipa nafasi ila napenda kusema kwamba naiunga mkono hoja hii kwa asilimia

mia na wenzangu wote tuiunge mkono tuiunge mkono hoja hii na serikali nzima tuiunge mkono hoja hii na serikali nzima tuinge mkono hoja hii, ili mambo ya matumizi na mapato na mambo mengine yahusuyo basi yaende kwa taratibu zilizopangwa. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti. *(Makofi)*

**Mhe. Mwenyekiti:** Ahsante sana nakushukuru Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi kwa mchango wako. Sasa naomba nimuite Mhe. Yussuf Hassan Iddi, atafuatiwa na Mhe. Omar Seif Abeid, kama muda utaruhusu basi Mhe. Suleiman Sarahan ajiandae.

**Mhe. Yussuf Hassan Iddi:** Ahsante Mhe. Mwenyekiti kwa kuweza na mimi fursa mchana huu kuweza kuchangia Ripoti hii ya Kamati ya Kudumu ya Kuchunguza Hesabu za Serikali na Mashirika ya Umma kwa mwaka 2014/2015.

Kwanza kabisa mimi nitoe masikitiko kwamba ripoti hii tulikabidhiwa jana jioni, na katika ripoti za kamati hii ni ripoti kubwa ambayo ina *page* karibu 221 na tukizingatia jana hapa tuliondoka saa mbili za usiku, kwahivyo imekuwa vigumu sana kuweza kuiptia ripoti hii na leo kuweza kutoa michango yetu. Afisi ya Baraza niishauri basi ripoti kama hii mwakani tukijaaliwa basi tupate angalau siku mbili kabla ili tuweze kuipitia vizuri na kuweza kutoa michango yetu. *(Makofi)*

Lakini la pili Mhe. Mwenyekiti, kwanza tuipongeze serikali yote nzima wizara zote kumi na tatu pamoja na watendaji wao wakuu pamoja na kada nzima ya uhasibu. Kwakweli, kwa mujibu wa ripoti hii kuna mabadiliko makubwa sana ukilinganisha na ripoti zilizopita nyuma huu ukweli lazima tuuseme na kazi kubwa sana ambayo imefanywa hasa na wahasibu, wasaidizi wahasibu, washika fedha, maafisa manunuzi kwa hivyo nichukue fursa hii ya kuwapongeza sana hawa watendaji wetu kwa kazi kubwa ambazo

na ngumu wanazozifanya katika Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar. *(Makofi)*

Lakini pia nichukue fursa hii kumpongeza *CAG* pamoja na watendaji wake kwa kufanya kazi hii na tukapata ripoti hii japokuwa ripoti iko nyuma. Kwahivyo, tuiombe serikali kama wenzetu hawa wa *CAG* wana upungufu wa wafanyakazi basi ipo haja ya kuwapatia wafanyakazi wa kutosha ili taarifa hizi ziwe zinakwenda na wakati na tusiwe tunajadili viporo, maana yake hichi kiporo sasa hivi tuko kwenye kumi na saba kumi na nane, hii ripoti ya 2014/2015. Kutokana na hali hiyo tunaiomba serikali iwapatia watendaji wa kutosha Afisi ya *CAG*, ili waweze kufanya kazi kwa ufanisi zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, nianze mchango wangu kwenye ukurasa wa nne ambao Waheshimiwa Wajumbe wengi wamechangia kuhusiaa na Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo. Kwakweli, kwa mujibu wa ripoti hii yapo mapungufu ambayo Kamati ya *PAC* imeyabaini na ipo haja sisi wenyeviti wa Kamati hizi za Maendeleo ya Mfuko wa Jimbo kuweza kuchukua changamoto hizi, ili zisije zikajirejea tena. Lakini kwa upande wa serikali tuombe tu kwamba ipo haja ya kuendelea kutoa mafunzo kwa kamati hii, ipo haja ya kutolewa mafunzo mafunzo yametolewa kwa mara ya kwanza tu lakini hayakutolewa tena. *(Makofi)*

Kwahivyo, changamoto ambazo zinajitokeza ni zaidi kwamba kuna ukosefu wa elimu ya kutosha katika kamati hizi, hivyo ni vyema ipo haja serikali kuliangalia hili na sisi safari hii Wenyeviti wa Kamati watushirikishe, kwasababu mafunzo waliyotoa katika kipindi kilichopita wenyeviti hawakutushirikisha katika mafunzo yale, kwahivyo mafunzo yatakayoendelea kuyatoa tena basi na sisi wenyeviti watushirikishe kikamilifu, ili na sisi tupate uelewa mzuri kwasababu sisi wengine unaweza ukasema ni wageni kwenye shughuli hizi, wengine *Alhamdullillah* wazoefu

wameshiriki katika Baraza lililopita, lakini sisi wengine ni *newcomer* ambao tumeingia juzi. *(Makofi)*

Lakini pia Mhe. Mwenyekiti, kuna suala zima hili la upatikanaji wa Fedha za Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo, kwakweli sisi wenyeviti wa kamati tunasikitika sana, tunasikitika kwasababu pesa hizi zinakuwa zinachelewa mno ukilinganisha na wenzetu wabunge. Kwahivyo, sisi wawakilishi tunaonekana hatuwajibiki vizuri kwa kuwa sababu kubwa hatuna fedha, wenzetu wale pesa zao kwakweli zinakwenda kwa mpangilio mzuri kiasi ambacho mbunge hawezi kutumia pesa yake mfukoni tafauti na sisi wawakilishi, wao wenzetu wameshapata mara tatu sisi tokea tuingie tumepata mara moja na hii mara ya pili. *(Makofi)*

Kwahivyo, nimuombe Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti nafikiri yupo hapa anatusikia, basi kabla ya kumaliza mkutano huu tarehe 28/2/2018 basi pesa hizi ziweze kuingia katika *account* yetu na tukimaliza hapa sisi iwe rahisi wajumbe kuweza kuingia katika majimbo yetu na kuweza kutekeleza. Lakini vile vile tumuombe Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango pamoja na serikali kwa jumla kwamba watuongezee hizi fedha milioni ishirini ni kidogo sana kwa hivyo tutoke kwenye milioni ishirini angalau ziwe milioni ishirini na tano. Kwakweli, tunaomba hili Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango ni mheshimiwa ambae ni makini sana msikivu, akiombwa anaombeka, basi alichukue hili ombi letu kuhusu Fedha za Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo ziongezeke kutoka milioni ishirini hadi milioni ishirini na tano. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, pia katika ripoti hii kumeelezwa kwamba kuna ukiukwaji wa taratibu za manunuzi, ambapo karibu shilingi milioni 294,638,795/= fedha hizi kwa ajili ya ukiukwaji wa manunuzi. Vilevile, manunuzi kwa mujibu wa ripoti hii yameonekana hayafuati au hayaingatii thamani halisi ya fedha

yaani, *value of money* pamoja na kwamba maafisa manunuzi hawafuati ule mpango wa mwaka wa manunuzi.

Kutokana na hali hiyo, tunaiomba serikali iwapatie mafunzo ya kutosha hawa maafisa manunuzi, ili dosari hii ambayo imeonekana na Afisi ya *CAG* pamoja na ripoti ya *PAC* hizi dosari ziweze kuondoka na tutakapojadili ripoti nyengine basi mapungufu haya yasiweze kuonekana. Mhe. Mwenyekiti, tunawaomba maafisa wanunuzi wa serikali na taasisi zote kwa ujumla, kwakweli wawe wanafuata ule mpango wa manunuzi wa mwaka ambao wameuandaa, matumizi mengi yanaonekana hayakufuata utaratibu huu yapo nje na mpango ambao wameuandaa.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mujibu wa kitabu hichi kuna jumla ya shilingi 634,330,660/= hizi ni kwa ajili ya ukiukwaji wa utaratibu wa fedha, yaani *CAG* alipokwenda kukagua *document* za malipo nyengine zilikuwa hazipo kwa hivyo vielelezo havikuonekana vya matumizi ya fedha shilingi 634 hili Mhe. Mwenyekiti, linakuwa linajirejea kila mwaka, kwa maana hapa inaonekana zaidi kwamba suala la utunzaji wa kumbu kumbu unakuwa si mzuri. Kwahivyo, tuwaombe sana watunzaji wa kumbukumbu za mahisabu wahakikishe kwamba wanavitunza kikamilifu vilelezo hivi *supporting document*, ili watakapokuja wakaguzi basi waweze kuviona na waweze kuridhia yale matumizi jinsi yalivyofanyika.

Lakini jengine Mhe. Mwenyekiti imeonekana kwamba bado kuna uchereweshaji mkubwa wa kupeleka fedha mapato haya benki, bado taasisi zinakusanya pesa hizi *cash* wanakaa nazo kwa muda mrefu ofisini na wanashindwa kupeleke benki kwa wakati. Kwahivyo, tunaiomae serikali kwa zile taasisi ambazo hawajawa na mpango wa kulipia benki moja kwa moja, basi wafanye utaratibu huo, ili kudhibiti uvujaji wa mapato ya serikali.

Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyosema awali kwamba kitabu hichi ni kikubwa na tumekipata jana usiku kwa hivyo hatukupata kwenda kwa ndani sana. Kwahiyo, nimalizie tu kwa kusema kwamba tunaiomba serikali imeanza kuhakiki mali za serikali na kuingiza kwenye daftari la kuduma, lakini mpaka sasa ni wizara tano tu ambazo zimeingizwa kwenye daftari hilo kwa hivyo bado wizara nane hazijaingizwa kwenye daftari hizo, kuna Mhe. Mjumbe alisema "Mali bila ya daftari hughaibu bila ya habari". Bila ya kuwepo madaftari haya mali nyingi za serikali zinaweza zikapotea na baadhi ya watendaji wajanja wajanja wanaweza wakazimiliki zikawa za. Kwahiyo, tunawaomba wenzetu serikali tujitahidi sana kuharakisha kwenda kwa kasi zaidi kuweza kuorodhesha hizi mali zote za serikali kwa serikali yote nzima yaani, wizara zote kumi na tatu, ili tuweze kudhidhibiti vizuri ya mali za serikali na ziweze kutumika kwa muda mrefu.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo nimpongeze sana Mwenyekiti wa Kamati ya *PAC* pamoja na wajumbe wake kwa kazi kubwa ambayo wameifanya na tumuombee tu Mhe. Mwenyekiti umuombee, ili arudi tena kuwa mwenyekiti wa kamati hii katika kipindi kinachokuja, ili ripoti basi ile inayokuja iwe nzuri zaidi na sisi wajumbe tupate muda wa mkusaidia. Baada ya maelezo hayo nakushukuru sana Mhe. Mwenyekiti, na nakuunga mkono hoja ahsante. *(Makofi)*

**Mhe. Mwenyekiti:** Ahsante Mhe. Yussuf Hassan Iddi kwa mchango wako. Sasa naomba nimwite Mhe. Omar Seif Abeid atafuatiwa na Mhe. Suleiman Sarahan na kama muta utakuwepo basi Mhe. Shaib Said Ali naye ajiandae. Waheshimiwa Wajumbe, kabla sijamuita Mhe. Omar Seif Abeid mchangiaji wetu wa mwisho kabla ya Mhe. Suleiman Sarahan nitamuomba Mhe. Waziri wa Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais atumie ile kanuni ya kutengua muda, ili tumalize kabisa palipobaki, tumalize aje Mhe.

Waziri atoe mchango pamoja na ufafanuzi kidogo na mwisho tumwite Mwenyekiti wa Kamati tumalize, ili jioni tuendelee na shughuli nyengine. *(Makofi)*

**Mhe. Omar Sief Abeid:** Ahasante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi ya kuchangia kidogo katika hotuba hii, lakini awali ya yote sina budi nimshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema aliyetujaalia tukakutana tena na mchana wa leo, nikaweza kusimama kuchangia katika hotuba hii. Vilevile, sina budi kumpongeza Mwenyekiti wa Kamati hii na kamati yake yote kwa ujumla na wizara anazozisimamia na ripoti yake aliyotuwasilishia ni ripoti kubwa ya aina yake ya kipekee, ambayo kama alivyosema Mhe. Yussuf Hassan Iddi ilihitajika tupate muda wa kuisoma ili tuweze kuiboresha zaidi. *(Makofi)*

Lakini naamini kwamba yaliyomo ni mengi na yanatosha kuyachangia kwa leo. Kwahivyo, Mhe. Mwenyekiti, moja kwa moja nataka nianze juu niende chini, nianze na ukurasa wa 156 naizungumzia Wizara ya Fedha na Mipango yenyewe. Kwanza sina budi kuchukua fursa hii kuupongeza uongozi wa Wizara ya Fedha na Mipango imefanya kazi kubwa sana na ni haki yao kupongezwa, kwasababu wamevuka lengo la makusanyo wao walijikadiria kukusanya bilioni 389,953,000,540,000/= lakini wame *over* mpaka bilioni 446 ni ongezeko la shilingi bilioni 563,179,000,000/= ni hisabu nzuri na kiwango kikubwa ambacho ni cha kujivunia. *(Makofi)*

Lakini pamoja na ongezeko hilo nilikuwa nawaomba wizara waendelee wasitosheke na wala wasisimame na faraja waliyoipata ya kuongeza kiwango hicho cha makusanyo, kwasababu bado tuna kazi kubwa ambayo inatukabili mbele yetu. Hivyo, ni wajibu wetu kwa pamoja kushirikiana, ili kuhakikisha kwamba makusanyo haya yanakwenda mbele kasi hii iliyoanza kujitokeza mwaka iwe ni endelevu.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kutoa ushauri mwengine kwa wizara pamoja na serikali kwa ujumla kuchukua hatua za haraka za kutafuta *solution* ya kutumia *IFB machine*. Kwakweli, kama wenzangu walivyosema ni muda muafaka sasa kwasababu ulimwenguni sasa tumeshatoka na huo utaratibu wa kukusanya kodi kwa njia nyengine, ili kufikia lengo zaidi na kuweza kupata mapato zaidi. Hivyo, ni vyema sasa tukatumia utaalam huu wa kutumia mashine hizi za ukusanyaji wa kodi zipatikane na zianze kufanya kazi, ambapo ni imani yangu kwamba kama tunaweza kukusanya tumefikia kiwango hichi kwa makusanyo ya kawaida kwa kutumia ukusanyaji wa kawaida, tutakapokuwa na mashine hizi tunaweza kufika mara mbili au mara tatu ya hapa tulipo sasa hivi.

Lakini Mheshimiwa pamoja na hayo katika ripoti hii kuna mambo ambayo pia nataka niende kidogo niyaangalie kwa kuyachangia sisi kwa upande wetu kuna kitu hiki kilichozungumzwa hapa katika mstari wa kwanza, kinahusiana na mkonga wa taifa mstari wa pili mashamba ya mpira. Serikali imejipangia kukusanya pesa dola za kimarekani laki moja kwa kila mwaka ambazo kwa mwaka 2014/2015 zilitakiwa pesa hizi ziingie serikalini na ziweze kusaidia, lakini mashamba haya pamoja na kwamba yamerudi serikalini tutizame ni faida gani inayopatikana kwa serikali kwa kuwepo mashamba haya kwa hivi sasa.

Kwakweli, kama ilivyoelezwa na kamati kwamba mashamba tayari yameshachoka na kweli yamechoka uzalishaji wake umeshuka. Kwahivyo, naomba wataalam wa Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi kama walivyokuwa ni wataalam basi waishauri serikali njia bora ambayo itasababisha mashamba hayo kuongeza tija kwa serikali, sio tu kuhisabu kwamba tuna mashamba ya mpira ambayo yatakuwa hayaleti maslahi makubwa tuliyoyakusudia ambapo tumetumia ardhi nyingi.

Kwakweli, kama itakuwa mashamba ya mpira hayawezi kuzalisha tena uzalishaji umeshuka, basi sasa wajibu wetu tubadilishe matumizi kutoka mashamba ya mpira tutizame namna bora ambayo itaweza kutuletea faida, ardhi ni mali.

Lakini pia nilitaka nijue hii Kampuni ya *Agro Tax Limited* pamoja na kuwa iliyumba lakini si bado ina deni la serikali, kama ina deni la serikali kwa nini isilipe deni hili?

Kwahivyo, naiomba wizara isimamie Wizara ya Fedha na Mipango, ili tuweze kujua namna bora ya kuongeza mapato kutokana na mashamba yale ya mpira ambayo sasa hivi yanaonekana uzalishaji wake ni wa kusua sua.

Kwakweli, pia kama hilo halitoshi nilikuwa nina masikitiko kidogo kuhusiana na ripoti kwamba kwenye ripoti hii utaona mapungufu mengi ya manunuzi ambayo yamefanywa kwa wizara na taasisi za Serikali ambayo hayakufuata utaratibu, tumezoea kupata Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kila mwaka tunawasilishiwa hapa ripoti hiyo, lakini hatuoni utekelezaji wake. Kwahivyo, naiomba serikali kwenye mara hii wakati wa uwasilishaji wa Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali tupewe na ripoti ya utekelezaji.

Jambo hili litatusaidia sisi kuweza kuishauri serikali, kwasababu tunaona mapungufu tele yaliyomo humu, lakini baada ya kuyazungumza hatuoni kitu kinachochukuwa hatua. Kwahiyo, tunaiomba sana serikali kupitia Wizara ya Fedha na Mipango kwamba zinapokuja ripoti hizi iwepo na ripoti ya utekelezaji, isiwepo tu ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, lakini na ripoti ya utekelezaji wa yale maagizo

yaliyotolewa na nini kimetekelezwa baada ya kuonekana na ile Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Nasema hivyo kwasababu gani, ukiangalia leo hapa kwenye ukurasa wa 119 Afisi ya Usajili wa Vitambulisho utaona kuna matatizo kama hayo. Ukija kwenye 110 mapaka 111 nataka kujua kuhusu kucheleweshe kubadilisha jina la umiliki wa magari. Maana yake mambo kama haya *ZRB* wanapiga kelele kwa wananchi kwamba tubadilisheni majina, ili serikali iweze kupata mapato. Lakini leo taasisi ya serikali kwenye ripoti ukiiyona hapa ukifungua ukurasa wa 111 inasema.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kunukuu ukurasa wa 111.

"Aidha Kamati iliagiza kupatiwa *copy* ya *card* ya umiliki ya hiyo gari ambayo iliwasilishwa na baadaye ilibainika kuwa jina la mmiliki wa gari hiyo ni Abrahman Simai Vuai na badala yake jeshi la Kujenga Uchumi pia jina hilo ni tofauti na lile liloainishwa katika mkataba wa Mauziano ambapo kwenye mkataba wa mauziano jina la muuzaji liloainishwa ni Abrahmani Ismail Vuai".

Utashika wapi, utamshika nani hapa, utamuuliza nani hapa, utamuhoji nani hapa. Utamuhoji Abrahmani Ismail Vuai, au utamuhoji Abrahman Simai Vuai, nani utamuhoji hapa.

Mhe. Mwenyekiti, hata hiyo *ZRB* hawawezi kukusanya mapato kwa sababu hawana mtu maalum ambaye wanaweza waka *collect revenue.* Kwa nini taasisi kama hii imefikia hatua ya kununua chombo, kinakaa mwaka mmoja taasisi ya serikali haijabadilisha jina, haiwezekani. Kutokana na hali hiyo, naomba kutoa ushauri taasisi hii na napenda kuiulizia maswali sana katika kwenye taasisi hii. Najua ni taasisi ambayo ni chombo chenye wataalamu ambapo kuna wanasheria mule, kuna kila kitu kinafanywa. Ukija

kwenye kifungu kidogo cha 2 ukikisoma maoni ya ripoti ya kamati wanasema. Mhe. Mwenyekiti, naomba kunukuu:

"barua kutoka Wizara ya Fedha na Mipango ya kuthibitisha uteuzi wa Wajumbe wa Kamati ya Kuthamini Zabuni ambapo ilielezwa kuwa Wajumbe wake hawakupewa barua ya uteuzi".

Mhe. Mwenyekiti, ina maana hakuna kitu kilichokuwa kilikwenda sawa hata kimoja. Ikiwa taasisi za serikali zinashindwa kwenda kwenye mstari tukaweza kuwa na lengo moja tukafikia kukusanya mapato kwa pamoja na wananchi na wao wataiga kwasababu hawa ni kama wazazi. Wazazi na watoto, watoto wanapokosea, wanapoona wazee wao wanafanya mambo mabaya na watoto ni rahisi na wao kuiga mwenendo wa wazazi.

Sasa ikiwa sisi leo tunasoma taarifa ya serikali ya kamati hii kuhusiana na taafisi za serikali ambazo hazifanyi haya, hazihaulishi, raia wetu wa kawaida tutakuwa na uwezo gani wa kuwalazimisha kufanya, tutakuwa hatuna uweo wa kuwalazimisha. Kutokana na hali hiyo, ili lengo hili la *ZRB* na *TRA* waweze kufikia malengo ya kukusanya kodi kutokana na kubadilisha majina ya vyombo vya moto au vya umiliki ni lazima na taasisi zetu za serikali nazo zinaponunua wahakikishe kwamba wanafuata utaratibu, ndio ilivyo na ndio linalopendeza. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, tukizingumzia hilo tunazungumzia sambamba na Maoni ya Kamati Uk. 112 ambapo wanasema wamebaini kwamba zipo taasisi za serikali zinazodaiwa na JKU. Tumepiga kelele sana na tunaendelea kusema tunapotoa huduma taasisi ya serikai yoyote inapotoa huduma kuipa taasisi nyengine ni vyema zikalipwa tena kwa wakati, ili nazo kuziwezesha kutekeleza majukumu yake. Kwa mfano, leo ikiwa JKU wanawadai Bunge,

wanadai *ZAWA*, wanawadai *ZECO*, wanawadai wengine hawalipwi, hawapewi hizi fedha, vipi wataweza kujiendesha. Vipi wataweza kukidhi mahitaji yao. Kwahiyo, wito wangu kwa taasisi za serikali ambazo zimepewa huduma za ulinzi na huduma nyengine na taasisi au sekta binafsi zilipe. Ukiangalia katika ripoti hii utakuta kuna mambo mengi ambayo yamezungumzwa.

Mhe. Mwenyekiti, samahani nipe dakika mbili.

Baraza la Mji, leo hii ni sekta inayokusanya pesa kwa wingi, leo utakuta kuna madeni ya raia binafsi inakuwaje! Mhe. Mwenyekiti, napendekeza na naomba Baraza la Mji na sekta zote za serikai ni vyema kujitathmini kabla ya kuingia mikataba, wajuwe kwamba nachukua huduma hii je, nina uwezo wa kuirejesha au ya kuilipa, kabla ya kuingia mkataba na hatimaye kuja kuyaona kama haya. Najua Mhe. Mwenyekiti, umeshaanza kuniwashia taa.

Baada ya hapa naunga mkono sana hotuba hii kwa asilimia mia na naomba na sana kwamba Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo wenzangu wameuzungumza na mimi kidogo naukazia kazia uharakishwe. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

**Mhe. Mwenyekiti:** Asante nakushukuru Mhe. Omar Seif Abeid kwa mchango wako. Lakini kabla sijamwita Mhe. Suleiman Sarahan Said, naomba nimwite Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais atumie Kanuni ya Kutengua muda.

## KUONGEZA MUDA WA BARAZA

**Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais:** Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Kwakuwa shughuli iliyombeleyetu na kwakuwa Mawaziri na wao wapate nafasi ya kutoa baadhi ya maelezo na kwa kuwa tunaona upo umuhimu wa kumaliza shughuli hii katika kikao hichi cha mchana, naomba

tuweke Kanuni kando ya muda, ili tuweze kumaliza shughuli iliyombele yetu. Mhe. Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

**Mhe. Waziri wa Afya:** Mhe. Mwenyekiti, naafiki.

**Mhe. Mwenyekiti:** Waheshiiwa Wajumbe hoja imetolewa na naomba niwahoji wanaokubaliana na hoja hiyo.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

*(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)*

**Mhe. Mohammed Said Mohammed:** Kuhusu utaratibu.

**Mhe. Mwenyekiti:** Wanaokataa, waliokubali wameshinda. Naam Mhe. Mohammed Said Mohammed kuhusu utaratibu.

## UTARATIBU

**Mhe. Mohammed Said Mohammed:** Mhe. Mwenyekiti, Kanuni ya 23 ambayo ndiyo Kanuni ya kuakhirisha muda Mhe. Waziri aliposimama hakutaja Kanuni hiyo na tumeenda kwa mazoea. Kwahivyo, hata maamuzi yako kwenye kiti chako unayumbishwa kutokana na kanuni hizi ambazo tumejipangia na kanuni hii itakuwa batili na hii uliyoihoji na kama utaridhia wewe mmoja ndiye utakayekuwa unavunja Kanuni ya 23 kwasababu kanuni hiyo haikutajwa,

Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru.

**Mhe. Mwenyekiti:** Nakushukuru Mhe. Mjumbe kwa kunikumbusha. Mhe. Waziri naomba uitaje hiyo Kanuni.

**Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais:** Namshukuru Mhe. Mohammed Said Mohammed, kwa kutukumbushia kuitaja Kanuni ya 23 na kufuata kanuni hiyo. Naomba tuweke kando Kanuni hiyo, ili tupate muda wa kutosha kumalizia shughuli iliyokuwepo mbele yetu, hasa tukiangalia umuhimu wa kulimaliza jambo hili kwa mchana huu. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

**Mhe. Waziri wa Afya:** Mhe. Mwenyekiti, naafiki.

**Mhe. Mwenyekiti:** Nakushukuru sana Mhe. Waziri. Waheshimiwa Wajumbe naomba niwahoji wale wote wanaokubaliana na hoja hiyo wanyooshe mkono na wanaokataa, nawashukuru waliokubali wameshinda.

*(Hoja imetolewa iamuliwe)*
*(Hoja imeamuliwa na kuafikiwa)*

**Mhe. Mwenyekiti:** Waheshimiwa Wajumbe, tunaendelea, nimwite mchangiaji wetu Mhe. Suleiman Sarahan Said, atafuatiwa na Mhe. Shaib Said Ali, na baadaye nitampa nafasi Mhe. Waziri.

**Mhe. Suleiman Sarahan Said:** Nakushukuru sana Mhe. Mwenyekiti, mimi nilimuona Mhe. Mohammed Said Mohammed (Dimwa) alipotaka kupata masahihisho. Lakini hata Mwenyekiti, aliposema kwamba aliyekubali hoja hiyo pia hakukubali, inaonekana huyu hakubali Kanuni wala Sheria, yumo tu kwasababu aliposahihisha hakunyanyua tena mkono. Mhe. Mwenyekiti, tuendelee. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nasaidia kuchangia katika kitabu chetu hichi ambapo kwa kweli Mhe. Mwenyekiti, nimpe pongezi sana, hichi ni kitabu karibu cha bajeti, ni kitabu kikubwa kweli kweli,

kinataka wiki nzima hiki tuweze kukisoma. Namshukuru sana Mheshimiwa amefunua mengi sana na sisi tutapata dondoo chache chache. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nataka kuchangia kwa ujumla kuna mambo ambayo bado yanahitaji kuyatizama kwa kina, ili kuweza kuendeleza jukumu letu hili la serikali kutokana na matatizo mengi yanayotokana na kifedha au katika sekta nyengine tunazozihitaji kwa wananchi.

Mhe. Mwenyekiti, tunautaratibu mmoja wa kuona mtu yeyote ambaye kasoma ndani ya nchi ambaye hajasoma nje basi tunaona hajasoma mpaka akasome nje. Kwakweli, ningekuwa kama kiongozi wa nchi, basi ningesema ilivyokuwa vyuo vyetu vinatosheleza watu wasingekwenda kusoma nje, wangesoma hapa hapa kutokana na mazingira yaliyopo. Mpango mwengine ni kupoteza pesa wala hausaidii kitu. Kwasababu tunakwenda tofauti na itikadi zetu na silka zetu na maadili yetu. Kwa mfano, unamtoa mtu hapa unakwenda China kwenda kusomea kilimo au mifugo, anakwenda kufuga chura, ukimleta huku sisi chura hatuli, sasa unakwenda kumsomesha nini. Angekuwepo hapa tungeweza kumsomesha vitu vyengine akaweza kuendeleza. Tunawasomesha wengine wakija huku wanataka kutupeleka kwengine na sisi mazingira yetu hayendi. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, lingetizamwa hili kwa kina wale wanaokwenda kusomea nnje waende kwa sababu maalum, sio kila kitu wakasomee nje, vitu vyengine haviendani na silka zetu. Hapa Zanzibar hatufugi nguruwe, wengine wanakwenda kule kusomea nguruwe, akija hapa elimu yake haisaidii kitu, tungeona vitu vyengine vikaweza kuratibika kabisa.

Mhe. Mwenyekiti, pia na vitu vyengine ambavyo vinatuvunja moyo katika maeneo ni baadhi ya viongozi wanaopewa maeneo

katika kuongoza ukikuta menaja au kiongozi anapewa kampuni au anapewa shirika badala ya kwenda mbele linaanguka chini, lakini baada ya muda anaondoshwa shirika lile anawekwa shirika jengine na lile jengine aende akalimalize. Hii ndiyo taratibu na tunao watu waliosoma, tuwajaribu na wengine sio vitu vya kila wakati kumng'ang'aniza mtu huyo huyo mmoja, hivi vinatupeleka nyuma.

Mhe. Mwenyekiti, bwana nataka nikwambie kitu, ukiowa mke ndugu ukimuonea haya huzai. Kila siku utasema mimi na huyu tumetoka pamoja, tumetoka pamoja, miaka inakwenda mwisho mnakuwa wazee hamzai, lazima huu uweke huku, huu uweke huku mpate watoto hili lazima Mhe. Mwenyekiti liendelee. *(Makofi)*

Lazima kuna vitu tuweze kuvitengeneza tuondokane na mazoea, mazoea yanatupeleka sipo, kila siku tunajaribu kubadilika lakini hatwendi.

Mhe. Mwenyekiti, nataka nichangie kigogo, nazungumzi habari ya mapato kwenye mambo ya miji. Bado miji ina nafasi za kutosha za kuweza kukuza pato la nchi, lakini bado viongozi waliokuwepo kwenye maeneo ya miji kwa mambo mengine inawezekana kwanza hawajapelekwa nje wakenda wakaona miji ya watu inavyoongozwa. Hawajaoneshwa kila kitu, wewe umemchukua tu kumuweka hapa ili akae kwenye mji sasa msikilize ukiritimba wake watakavyokusumbua. Kila jambo kwake ni geni, lazima kama tunataka miji yetu ikuwe na iendelee wale waliokuwepo pale wasomeshwe na wakatembezwe tusione hasara kuwatembeza wakaona miji ya watu na mji wetu utakuwa.

Mhe. Mwenyekiti, Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano aliyepita alisema huwezi kula lazima na wewe uliwe. Lazima na sisi tuweze kutoa kitoa kitu ndio na sisi tufanikiwe ni vitu ambavyo

lazima tuvitizame. Tuna Madiwani tumewachagua wenyewe kwa mambo mengi sana ni madiwani wanafanya kazi ya kutosha, hawana usafiri hata baskeli. Wewe unamwambia tu kwamba wewe hufanyi kazi, mguu haufanyi kazi umeshapitwa na wakati, hata vespa za shilingi milioni mbili tunashindwa kuwakopesha au kuwapa. Hata ukisema waende wakakope benki hawapewi benki wale, hawana mikataba ya kukopeshwa, huku serikalini ni watu wakubwa diwani.

Mhe. Mwenyekiti, lazima hapa tuwatizame madiwani wetu. Kitengo kilichohusika na Madiwani lazima kiwasaidie usafiri, *otherwise* hapafanyiki kitu, hata kama ni kuwakopesha. Madiwani wanafanya kazi za kujitolea, mapato yao ni madogo kutokana na hali halisi, wanadhalilika kwa ufupi nikisema kitu kama hicho.

Mhe. Mwenyekiti, nataka nizungumzie zaidi habari ya watendaji wetu katika makabidhiano. Mtu anapotaka kuhamishwa unasikia ngoja yanakuja makabidhiano *auditor* anakuja mnakabidhiana mnamaliza, yule mtu anakwenda zake nyumbani, ngoja yule mtu aende akafe, ngoja yule mtu aumwe, aondoke pengine, ngoja yule mtu afanye biashara zake linarudi bomu huku kwamba yule mtu aliiba. Wewe ulipokwenda kukabidhiwa ulifanyaje, maana ya kukabidhi ni nini. Lakini mpaka leo kwenye sekta zetu za serikali hakuna buku la *register* chochote kiingiacho wala kitokacho, hakuna kilichokuwepo wala kisichokuwepo, watu wanajichukulia wanavyotaka wenyewe halafu wakisha kuondoka ndio uje usikie na kile kilikuwa chetu.

Kwahiyo, unafanya nini mambo yameshapita ni kumuonea sasa hivi, ukisema unarudisha kile kitendo kilichopita ni kumuonea, kwenye sheria umeshamaliza. Umeshaambiwa mtoto akiharibu mpige bakora pale pale kitu alichoharibu, sio umsubiri mtoto keshakuwa mkubwa au siku ya pili ndiyo unasema ngoja

nikushtakie mambo ya mtoto ya juzi aliyofanya. Hafahamu ulikuwa unamwambia nini.

Mhe. Mwenyekiti, lazima tubadilike wanaoitwa *auditors* wanakwenda kukabidhiana basi awe anajua kwamba sio anasema nakwenda pale kutia saini tu, siyo saini wewe umepelekwa pale kwenda kutizama kilichopo. Lakini na wao usiwalaumu, hakuna *register* buku ya kitu chochote kilichopo pale ndani atakamata nini, kilichokuwepo hakijui, kilichoingia hakifui na chochote hakijui, kwa hivyo na yeye anatia saini tuondoke ndiyo hayo safari iende, lazima tuangalie.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu mikataba, mwenye *power* ya mtu mmoja anamaliza yeye kwamba mimi mikataba yangu nitamaliza kitu gani, hatujui sasa. Kuna vitu vinaitwa bure ghali, tunasema tunatandika tenda tunaita sijui *quotation* sijui kitu gani. Unamwambia lete *quotation* tatu, nne, ile ya chini nitachukua ya kwako wewe. Bure ghali, wakati tumeamua kutaka kujenga kitu, tutizame kwa tathmini itakayokwenda baada ya miaka miwili jengo lile bovu, baada ya miaka miwili kitu kile kibovu, wakumlaumu hatuna.

Mhe. Mwenyekiti, sasa hivi tuondokane na kuweka saini katika maeneo yetu, chini andika jina kwanza halafu tia saini ili tukujue wewe nani. Wewe unafika unapigwa muhuri unatia saini halijulikana hata kama kapita kuku au kapita kitu gani, huyu alikuwa nani, wakati ule alikuwa nani. Andike jina chini halafu atie saini yake, tuwe tunamjua yule aliyeharibu pale alikuwa nani. Lakini leo unaambiwa njoo nikutilie saini unagongwa muhuri, unachanganyika saini na ule muhuri hujui kama kapita kuku wala bata, unabakisha tu *record* hivi mwaka ule alikuwepo nani? Kwa nini tulikuwa tunashindwa kuandika jina, mihuri ya sasa hivi Mheshimiwa piga jina lako haya tia saini yako chini, utajijua mwenyewe huko unakotaka kwenda. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nataka nizungumze kuna lugha inasema muhali ni nguwo ya juu ni kama koti. Hili hata mimi nikifika nje huwa nalivua na bado sijakaa uchi niko *fresh*. Muhali ni nguo ya juu, hatuwezi kwenda na muhali. Hii *PAC* yatakuwa ni haya haya kila siku itakuwa ni *PAC*, hatukomeshi tukapiga mstari mwekundu kama hapa basi. Maelezo kila siku Meli ya Mapinduzi, Uwanja wa Ndege na mengine yanakuja sio kama haya ya mwisho. Hii imeshakuwa kama wimbo wa taifa kila asubuhi tunauimba lakini hatutendi kile tunachokifanya. Meli ya Mapinduzi tuliifungua kwa sherehe, Mhe. Rais alijikaza kwa hekima zake zote, akachukua pesa kila pahala matokeo yake tumemuangusha hatujui hata tunafanya nini.

Mhe. Mwenyekiti, meli ile ile naapewe mtu kesho mkoko unakata maji unakwenda Pemba na atakwenda nao Dubai, lakini kwa serikali ikiingia tu siku ya pili inalala, tuna tatizo gani? Tujijue serikali hii tokea hapo mwanzo viwanda vyote hata iwe Jamhuri ya Muungano viwanda vyote vilikuwa vya serikali na vyote vilikufa. Maana Mwalimu Nyerere aliuliza hata hivi viwanda vya maji ambayo hununuwi pia vilikufa, vilikufa viwanda vya bia, vilikufa viwanda vya soda, vilikuwa viwanda vyote vile vya maji ya kuchota hapa hapa vilikufa, sembuse leo tuseme kwamba tutakwenda kununua mzigo tukileta.

Serikali kutokana na hali ilivyo kutokana na mambo yalivyo. Mhe. Mwenyekiti, hata hii meli nashauri ikodishwe ili tupate manufaa sisi wasafiri ikodishwe itakwenda ile tumeshakodisha meli ya mafuta, tumeshaikodisha MV. Maendeleo bora tukodishe tujuwe chetu twatakipata vipi kuliko kuendesha hasara matokeo yake tutaiuwa siku mbili tatu tunaiweka pale juu mabilioni ya pesa yatakuwa yamepotea.

Mhe. Mwenyekiti, nataka niendelee kidogo kwa kuzungumza kwamba vyanzo ambavyo tumevizoweya ambavyo hatuvijui hasa hivi leo, mimi nashukuru kwamba kuna mji wa mjini sasa hivi ndio Mjini Magharibi lakini ndio mjini pale maeneo ya Darajani ndio mjini sawa na pale mimi napaoneya huruma sijui patakuwaje, maana yake serikali ina mpango katika maeneo yale ya *taxi* kuja kujenga majengo mengine.

Lakini katika ulimwengu *taxi* maeneo ya ku *park* lazima yawepo Chake Chake hakuna eneo la ku-*park* hata moja, hakuna eneo la kushushia abiria pale mjini hakuna na bado hatujaweza kuweka mbinu watu wanaendelea kujenga hatujui tutasimama wapi. Leo mapato ya saa moja unayachukua siku nzima maana yake sasa imebidi sasa tuweke jiti njiani kwamba atakaye ingia mjini alipe chochote ndio cha kupata, wakati ange-*park* kwa saa moja tungeweza kuchukua pesa kwa muda mwingi masaa kumi na mbili masaa mangapi.

Leo mapato yote ya mtu anayekwenda mjini anatoa mapato la saa moja tu pale anapita pale kwenye jiti pita lete nini yetu uingie ndani kwenye chuma mheshimiwa pale kwenye chuma lakini ndani mapato yanapotea halafu mheshimiwa watu wanataka ku-*park* watu wanataka kupanga mizigo nafasi hatuna. Mhe. Mwenyekiti, naomba kumshauri Mhe. Waziri angetafuta nyumba mbili tatu akabomoa maeneo watu wanataka kwenda benki wana mifuko ya pesa na gari akasimame wapi hapajui, hivyo kweli utakwenda kumshusha mtu Michakaini aje na pesa huku si unamuuza kwa sijui kwa kitu gani, benki hapata *parking* benki yenyewe imeshindwa kupata *parking* haina...

**Mhe. Mwenyekiti:** Mhe. Mjumbe, malizia una dakika mbili.

**Mhe. Suleiman Sarahan Said:** Mhe. Mwenyekiti, nimalizie kabisa hamna maana yote nikayosema tutamaliza mpaka asubuhi

nakushuru sana, naunga mkono hoja. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

**Mhe. Mwenyekiti:** Ahsante sana nakushukuru Mhe. Suleiman Sarahan Said. Sasa naomba nimwite Mhe. Shaib Said Ali.

**Mhe. Shaib Said Ali:** Ahsante sana Mwenyekiti, awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu kutujaalia kukutana hapa mpaka sasa hivi kwamba tupo na tunaendelea na shughuli zetu hizi.

Mhe. Mwenyekiti, mchango wangu utakuwa mdogo tu kwa vile mimi ni mdau wa kamati hii machango wangu utakuwa ni mdogo sana. Awali ya yote kwanza nimpongeze mawaziri wote, makatibu wote, wahasibu wote pamoja na wakuu wote wa mashirika kwa jinsi kwa jinsi tulivyoshirikiana nao na kupata hili ambalo tumelipata.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hapo niende katia Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo. Katika Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo nachangia kidogo kwamba mfuko huu ulokwenda katika masuala yetu haya tumekuta kama kuna changamoto kidogo ambazo katika kitabu hiki sijaziona na ningeomba tu wenzangu wawakilishi wazikamate hizi, ili waweze kufanya kazi zao kwa ufanisi zaidi.

Moja ni mashirikiano ya kamati tujuwe na Mhe. Mwenyekiti tulipofika pale katika masuala yetu haya mashirikiano ya kamati kidogo yalikuwa ni madogo kati ya mwenyekiti na kamati yake hususan mwenyekiti huwa na katibu wake tu ndio wanaofanya kazi pamoja. Kwahiyo, naomba sis tuliopo haya mambo haya yaondoke kamba tuichanganye kamati yote iweze kufanya kazi kwa pamoja. *(Makofi)*

Jengine ambalo nililolikuta katika lile ambao sikuliona ni kwamba baadhi ya wenyeviti wanachanganya matumizi yao na ile fedha ya

serikali wanayopewa, ile fedha ya serikali wanayopewa basi huichanganya katika matumizi yao na hapa sisi pale nilipotaka kwenda pale aidha matumizi huyakuti kabisa ya ile fedha ya serikali ambayo wamepewa. Kwahivyo, nawaomba kwamba kile ambacho serikali wanakipata wenyeviti wanaofanya matumizi yao basi watumie kwa mujibu wa ile fedha waliyoipata.

Nikiendelea na mchango wangu Mhe. Mwenyekiti sasa nije katika mawizara. Mhe. Mwenyekiti, nasema kwamba mawizara na makatibu pamoja na wahasibu wote wamefanya kazi nzuri sana, lakini popote panapofanywa kazi na binadamu hapawachi makosa kwasababu kama tunavyojua kwamba mkamilifu ni mmoja tu. Kwahiyo, kuna changamoto tumeikuta kwamba matumizi huwa yanakosa vielelezo na vile vile tunasema kwamba kuna Waziri, Katibu Mkuu, Wahasibu, Wasaidizi Wahasibu mpaka Mhasibu wa ndani huwa yumo, lakini anapopita *CAG* huwa vielelezo vile havikuti. Lakini tunapopita sisi huwa vielelezo tunavikuta. Kutokana na hali hiyo, naomba kwamba hii ripoti iliyopita inasema kwamba kidogo kwamba imepita na wakati lakini hizi basi naomba kwamba Mawaziri na Makatibu wafanye masuala yao vizuri zaidi.

La mwisho ambalo Mhe. Mwenyekiti naomba kulingachangia kwasababu kama nilivyosema ni mjumbe wa kamati hii ni kuhusu halmashauri. Mhe. Mwenyekiti, matatizo makubwa halmashauri tuliyoyakuta kwamba ndani ya halmashauri bado kuna ufanisi mdogo wa wafanyakazi hususan wahasibu.

Mhe. Mwenyekiti, tumebahatika tumekuta halmashauri nyengine kuna bajeti mbili kwa muda wa mwaka moja kitu ambacho Mhe. Mwenyekiti sijui kilikuwaje utakuta halmashauri nyengine wanatumia fedha wanakopeshana fedha, lakini zinaporudishwa fedha zile huzijui wapi mtu gani anazipokea. Kwahiyo,

namuomba Mhe. Waziri hizi halmashauri azipe mafunzo zaidi, ili zipate kutekeleza kazi zake vizuri zaidi. *(Makofi)*

Baada ya hayo Mhe. Mwenyekiti, sina mchango mkubwa zaidi ni kutilia nguvu tu hapo, kwahivyo naunga mkono hoja hii kwa vile mimi ndio sauti kubwa naipongeza kabisa. Ahsante sana.

**Mhe. Mwenyekiti:** Ahsante nakushukuru sana Mhe. Shaib Said Ali kwa mchango wako. Sasa kabla sijamwita Mwenyekiti wa Kamati naomba nimwite Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango.

## MICHANGO YA MAANDISHI

**Mhe. Ali Suleiman Ali:** Naipongeza Ripoti ya Kudumu ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali na Mashirika (*PAC*) ya Baraza la Wawakilishi Zanzibar kwa mwaka wa Fedha 2017/2018.

Naupongeza Mfuko wa Jimbo, ombi langu fedha za Mfuko zitolewe kwa wakati.

Naipongeza Wizara ya Fedha na Mipango kwa juhudi zao nzuri ya ukusanyaji wa mapato. Aidha, napongeza kwa usimamizi mzuri wa matumizi mazuri ya fedha hizo.

Mwisho naipongeza kamati kwa kazi yake nzuri ya kufuatilia Mfuko wa Jimbo, hongera sana. Naiunga mkono ripoti hii kwa asilimia mia moja. Ahsante.

**Mhe. Salma Mussa Bilal:** Mhe. Mwenyekiti, naomba kuchangia changamoto za Ofisi ya *CAG*.

Kwanza naomba kuchangia suala la changamoto za uhaba wa wafanyakazi wa ofisi hiyo. Suala hili linachangiwa na wizara

kwani ofisi hii taratibu zote za uajiri zimeshakamilika, lakini bado wizara wamezuwia ruhusa ya ajira hiyo. Hivyo, naomba wizara nayo ikamilishe taratibu hizo ili vijana nao ambao mchakato wao wa ajira umeshakamilika waweze kuanza kazi ili changamoto hiyo iweze kuondoka.

Jengine ni changamoto ya wakuu wa idara na taasisi kushindwa kutoa ushirikiano kwa watendaji wa ofisi ya *CAG* kwa kutokuhudhuria katika mikutano ya kufungua au kufunga ukaguzi katika taasisi zao. Jambo ambalo linakwanza utendaji na ucheleweshaji wa kazi za *CAG* .Hivyo, naomba kuwekwe mikakati maalum kwa wakuu watakaoshindwa kutoa ushirikiano na ofisi hii, ili waweze kutekeleza shughuli zao ipasavyo.

**Mhe. Ussi Yahya Haji:** Awali ya yote naipongeza Kamati ya Kudumu ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali, chini ya Mwenyekiwiti wake mahiri Mhe. Miraji Khamis Mussa pamoja na wajumbe wake.

Kazi waliyoifanya ni kubwa na nzuri kupelekea kupata taarifa iliyojaa ukweli na ushauri mzuri kwa Serikali, mimi mchango wangu kwa jumla ni kwamba yale majimbo ambayo hayakutoa ushirikiano wa kuweza kupata taarifa ya matumizi ya fedha za Serikali yasiachwe hivi hivi tu. Serikali ichukue hatua zifaazo.

Mwisho naipongeza Wizara ya Fedha kwa namna ilivyopania, kwa kuongeza makusanyo ya mapato ya Serikali kwa kiwango ambacho kwa miaka mingi hakijapatapo kufikiwa. Kwa hayo machache sana naomba kuunga mkono tarifa hii, ahsante.

**Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango:** Mhe. Mwenyekiti, kwanza nianze kwa kukushukuru wewe mwenyewe binafsi kwa kunipa fursa hii na mimi kupata nafasi ya kuchangia hoja iliyowasilishwa. *(Makofi)*

Vilevile, nimshukuru sana Mwenyekita wa Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali (*PAC*) Mhe. Miraji Khamis Mussa nimshukuru yeye pamoja na wajumbe wa kamati yake wote kwa mashirikiano mazuri wanayotupa katika kipindi chote tutakapokuwepo katika nafasi hii. Lakini nimshukuru sana Mhe. Abdalla Maulid Diwani ambaye aliwasilisha taarifa ya kamati kwa niaba ya mwenyekiti. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, taarifa hii ni ya ukaguzi uliofanyika mwaka 2014/2015 na umehusisha wizara za serikali wizara mbalimbali lakini vile vile umehusisha mashirika na taasisi za serikali na pia umegusia pia katika Serikali za Mitaa, na kama ulivyo utaratibu kwamba baada ya Mhe. Waziri kuwasilisha taarifa na nadhani aliwasilisha taarifa yake ya taarifa ya kazi mwezi Mei tarehe 12 Mei, 2017. Kamati ilikwenda ikafanya kazi yake imeyaona waliyoyaona, wameainisha katika taarifa yao changamoto lakini pia wametoa maoni yao. Kwakweli, suala hili linahusu taasisi mbalimbali linahusu wizara tofauti, basi kama ilivyo utaratibu wetu tutakaa na taasisi hizo, tutatizama changamoto zilizoainishwa moja baada ya moja lakini vile vile tutatizama na maoni ya kamati.

Lakini, kama alivyosema mjumbe mmoja hapa hii ni taarifa ya mwaka 2014/2015 yawezekana yako mambo mengi ambayo yamegundulika humo tayari yamesharekebishwa na ukweli ndio huo na hali sio mbaya ni hali nzuri sana. Kwakweli, kuna *improvement* kubwa sana katika masuala ya usimamizi wa fedha na mali za umma, kwahiyo taarifa hii pamoja na kwamba tutaitolea maelezo ya mwezi wa Septemba, lakini yanaweza yakawa tayari yameshafanyiwa kazi. *(Makofi)*

Kamati, imeona mapungufu katika maeneo mengi lakini moja la Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo wamelizungumza, wamezungumza mapungufu katika maswali ya ununuzi na

wakataja pia Wizara ya Fedha na Mipango katika maswali ya ununuzi wa matajuri, hayo yote tutayatolea ufafanuzi wakati ukifika. Suala la taaluma kwa watendaji wanaohusika na masuala ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Serikali, suala hili linaendelea na nadhani juzi tu waliona mimi mwenyewe nilifungua semina ya mafunzo ya watendaji wanaohusika na masuala ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Serikali.

Lakini pia walizungumza maswali ya uwekaji wa kumbukumbu za mali za serikali *asset register* na usimamizi wake mali za serikali jinsi zinavyosimamiwa, madeni ya serikali waliyazungumza na jinsi taasisi zetu na mashirika yanavyofata taratibu za fedha katika uhaulishaji, vilevile, kuweka stakabadhi katika malipo ambayo yanafanyika haya yote wameyaona na niseme tu kwamba sisi tunayachukua tutayafanyia kazi na mwezi Septemba *Inshaallah* tutakuja kutowa ufafanuzi kwa kila hoja ambayo imeelezwa na kamati.

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako niseme jambo moja tu hili la Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo. Kwakweli, Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo umezungumzwa na wengine wakasema kwamba wenzetu wabunge tayari wamepata mara tatu sisi tumepata mara moja ni kweli. Lakini najua kwamba Waheshimiwa Wajumbe wanakumbuka vizuri sana kwamba fedha za Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo wa mwaka 2015 hatukutoa na tulikubaliana kwamba kutokana na matokeo yetu ya kurudia kwa uchaguzi fedha zile ziliondoka katika utaratibu wa utowaji wa fedha za Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo.

Kwahiyo, fedha ambazo tulizotoa zilikuwa ni fedha za mwaka za fedha 2015/2016 na hivi sasa zinadaiwa fedha za mwaka 2016/2017 na mwaka huu haujesha niwambie tu Waheshimiwa Wajumbe kwamba tayari Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais wameshawasilisha maombi ya fedha hizo na Wizara ya Fedha na

Mipango hivi sasa iko katika taratibu za kulipa kutoa malipo ya fedha hizo. Kwahivyo, wasiwe na wasiwasi si muda mrefu sana fedha hizo zitapatika. *(Makofi)*

Lakini kuna suala zima la jinsi ya kurejesha marejesho ya matumizi ya fedha za nyuma hayo ni kwa mujibu wa sheria, ambayo sheria hiyo imepitishwa hapa hapana tukiri kwamba baadhi ya majimbo utumiaji wa fedha hizi haukwenda vizuri. Sasa ni wajibu wetu dhamira ile ile ya serikali ya kutoa fedha hizi sasa sisi kama wajumbe lakini kama wenyeviti wa kamati za mfuko wa jimbo tusimamie na tusimamie kwanza katika hatua ya kuibuwa hiyo miradi ya wananchi na sheria inaeleza wazi jinsi ya kuibua hiyo miradi, kuwashirikisa wananchi wenyewe suala litakalofuata ni utekelezaji wa miradi hiyo na usimamizi wake, lakini baadaye kukusanya stakabadhi za malipo na kufanya marudisho Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais.

Mhe. Mwenyekiti, kwa baadhi ya majimbo hilo halifanyiki. Sasa wakati tunaomba kwamba serikali izingatie kuongeza kwa mfuko huu, lakini na sisi basi tuchukuwe wajibu wetu wa kuhakikisha kwamba tunasimamia matumizi mazuri ya fedha hizi, mimi naamini kabisa serikali hii ilivyo sikivu chini ya uongozi wa Dkt. Ali Mohamed Shein na iwapo fedha hizi zitakuwa zinatumia vizuri na zinaleta tija kwa wananchi kama inavyokusudiwa na serikali basi serikali inaweza ikazingatia ombi hilo na tujuwe tu kwamba huko nyuma ilikuwa mfuko huu, unahudumia miradi midogo midogo chini ya Wizara ya Fedha zilikuwa zinatoka shilingi milioni tano. Serikali hii hii imepandisha zikawa milioni kumi, zikawa milioni kumi na tano sasa milioni ishirini lakini wajibu wetu kuhakikisha kwamba fedha hizo zinatumika vizuri, ili pale tunapoomba basi serikali iyongeze kuwe na *justification* ya kufanya kazi. *(Makofi)*

Baada ya kusema hayo Mhe. Mwenyekiti, naomba kupokea hoja zote kama zilivyotolewa nauonga mkono hoja na *Inshaallah* mwezi wa Septemba tutatoa majibu. Ahsante sana.

**Mhe. Mwenyekiti:** Nakushukuru sana Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango. Sasa naomba nimwite Mwenyekti wa Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti, Hesabu za Serikali. *(Makofi)*

Ahsante Mhe. Abdalla Diwani kwa niaba ya mwenyekiti.

**Mhe. Abdalla Maulid Diwani** (**Kny. Mwenyekiti wa Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti, Hesabu za Serikali):** Ahsante Mhe. Mwenyekiti kwa kunipa mimi fursa kupokea au ku *windup* hoja hii ambayo niliwasilisha punde tu kwenye Baraza lako Tukufu. Lakini kabla ya kuendelea kusema chochote kwanza niwatambue wachangia wa hoja yetu hii ya Kamati ya *PAC*.

Hoja yetu Mhe. Mwenyekiti, imepata mchango wa wajumbe kumi na nane. Wajumbe kumi na moja walichangia kwa kusema na wajumbe saba walichangia kwa maandishi, kwa ruhusa yako mwenyekiti naomba niwatambue wajumbe waliochangia kwa kusema.

Wajumbe walichangia ni hawa wafuatao:-

1. Mhe. Abdalla Maulid Diwani
2. Mhe. Simai Mohammed Said
3. Mhe. Rashid Makame Shamsi
4. Mhe. Shehe Hamad Mattar
5. Mhe. Hussein Ibrahim Makungu
6. Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi
7. Mhe. Yussuf Hassan Iddi
8. Mhe. Omar Seif Abeid
9. Mhe. Suleiman Sarahan Said

10. Mhe. Shaib Said Ali
11. Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango.

Lakini vile vile niwatambue au niwataje waliochangia kwa maandishi.

1. Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi
2. Mhe. Masoud Abrahman Masoud
3. Mhe. Mohamed Mgaza Jecha
4. Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais
5. Mhe. Ali Salim Haji
6. Mhe. Ali Suleiman Ali
7. Mhe. Ussi Yahya Haji.

Kwa niaba ya kamati ile michango yote tumeichukua na sisi kama walivyosema serikali kwamba mwezi wa tisa ndio wanakuja kuleta majibu ya zile hoja ambazo tumezileta. Lakini nichukue nafasi hii kidogo tu kumjibu kaka yangu Mhe. Hussein Ibrahim Makungu katika hoja zake mbili alizosema kwamba, kwa nini Kamati ya *PAC* haiendi kuchunguza *ZAWA* na kwenye meli.

Sisi utaratibu wetu tunafanya uchunguzi wetu kupitia kitabu cha Mkaguzi wa Hesabu za Serikali, mara kupata kitabu cha mkaguzi ndio tunafanya mlolongo ule kwa zile taasisi alizozitaja japokuwa kama kamati tuna mamlaka hayo, tuliona bora kwanza tufanye haya ambayo ya lazima wakati tunajipanga kuyafanya hayo ya ziada wakati utaporuhusu kwa kupata baraka Baraza la Wawakilishi basi tutakwenda kuchunguza kila panapotumika fedha za zerikali.

Kwahiyo, kama Kamati ya *PAC* ina nguvu ya kwenda kuchunguza kwa sababu ndio kazi yake, lakini tulisema kwamba mwanzo tuyafanye haya ambapo kitabu chetu tulichopewa na

mkaguzi na tulikifanya tulikimaliza tunashukuru. Sasa tutaangalia siku za mbele je, tuna nafasi  ya kwenda kuangalia huko basi tutapata wasaa tutakwenda moja kwa moja kwasababu sheria hazitubani, sheria zimetupa nguvu kufanya hivyo kama Kamati ya *PAC*. Hilo halina shaka kabisa.

Kwahivyo, namuomba Mhe. Mjumbe kwamba mawazo yake tumeyachukua na tumeyapokea, basi tutaangalia utaratibu wa Baraza utatwambiaje kuona kwamba tunakwenda katika kuangalia masuala haya.

Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi katika michango mingi iliyokuwepo hapa ni suala zima la Mfuko wa Jimbo na Mhe. Waziri katutolea ufafanuzi mzuri sana tu. Lakini tutakuwa wakosefu wa fadhila kwa kutomshukuru shukurani za kipekee Mtendaji Mkuu wa Shughuli za Serikali Balozi Seif Ali Iddi, Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar na ofisi yake kwa usimamizi mzima wa upatikanaji wa fedha hizi mpaka kufika majimboni mwetu tukaweza kuzitumia. *(Makofi)*

Vilevile, isitoshe shukurani zangu za pekee katika suala zima la Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo, namsifu na nampongeza sana Katibu Mkuu na ndugu yangu Mkurugenzi Mratibu Khalid Amran. Shukurani za pekee kwasababu tulishirikiana naye kuanzia mwanzo mpaka mwisho kuona hizi changamoto zinazotukabili katika Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo juu ya upatikanaji wa fedha na mpaka kukagua hii miradi tulihangaika naye, tunamshukuru sana. Kwasababu amefanya kazi nzuri kutokana na maelekezo ya mwenyewe Mhe. Makamu wa Pili wa Rais wa nchi hii nafikiri hajamuangusha kafanya kazi vizuri tunampongeza sana katika hilo.*(Makofi)*

Isiwe mwisho tu katika hilo tunaamini kwamba atafanya kazi vizuri zaidi ya hayo na tutafanya kuona kwamba zile changamoto

zilizozungumzwa kwenye Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo na hata upatikanaji wa fedha nina imani kwamba muda si mkubwa pengine kesho tukitoka hapo Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango anaweza kurejea ile kutokana na hii changamoto inavyohitajika. *(Makofi)*

Vilevile, tutakuta wakosefu wa fadhila bila kuwashukuru mawaziri wote wa wizara zote, ambapo tulikwenda kufanya nao kazi kukagua zile kadhia zote tulizokabiliana nazo kutoka katika Kitabu cha Mkaguzi. Manaibu Waziri, Makatibu Wakuu na wakurugenzi wote wametupa mashirikiano ya hali ya juu sana, tunawashukuru sana.

Kamati ya *PAC* inapokwenda kukagua sio kama inakwenda kwa utashi wake au kwa hamu ya kumkomoa mtu hapana, Kamati ya *PAC* inakwenda kwa taratibu zilizopangwa na Baraza hili na serikali na kwenye Katiba ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imo Kamati ya *PAC*. Kwa hivyo, tunapokwenda kule hatwendi kumchokonoa mtu wala kumtafuta na kumuangamiza katika suala lake, bali ni kusimamia taratibu za nchi yetu na serikali yetu.

Mhe. Mwenyekiti, pia naipongeza serikali katika hilo kwa namna ya kipekee tumeona tulizungumza suala la *asset register* kuona kwamba limechagua wizara tano kuwa *pilot area* katika suala zima la kutengeneza *asset register*, ili kuwa na umiliki wa mali za serikali ziko katika sehemu husika. Naipongeza sana serikali katika hilo najua imefikia hatua nzuri, basi nisiseme sana juu ya hilo najua serikali kwamba inafanya mambo mazuri.

Mhe. Mwenyekiti, kupitia muda huu ahsante sana, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

**Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi**

**Mhe. Mwenyekiti:** Nakushukuru sana Mhe. Abdalla Maulid Diwani kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati. Waheshimiwa Wajumbe, hoja imetolewa, sasa naomba niwahoji wanaokubaliana na hoja hiyo wanyooshe mkono, wanaokataa, wanaokubali wameshinda.

*(Hoja imetolewa iamuliwe)*

*(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)*

Waheshimiwa Wajumbe, na nichukue fursa hii kuwashukuru sana kwa utulivu wenu na umakini wenu, na niwapongeze wale wote waliochangia na pia niipongeze Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali (*PAC*). Pia nimpongeze kwa dhati kabisa muwasilishaji ambaye ni Mhe. Abdalla Maulid Diwani, Mwakilishi wa Jimbo la Jang'ombe kwa umahiri wake na kwa hisia kabisa katika kuwasilisha ripoti hii, nawapongeza sana naishukuru serikali. *(Makofi)*

Namshukuru pia Waziri wa Fedha na Mipango na yeye ambaye amefafanua kwa kiasi fulani mpaka sote Waheshimiwa Wajumbe wanasubiri mwezi wa 9 *insha-Allah*, ili wapate majibu ya uhakika. Lakini na mimi nashukuru pia na niseme kuwa ipo haja ya mfuko wa jimbo kuongezwa kwa maslahi wananchi.

Waheshimiwa Wajumbe, nawashukuru sana kabla ya kuakhirisha niwatangazie Waheshimiwa Wajumbe kwamba Wawakilishi wote wa CCM wahudhurie katika ukumbi wa juu kuna kikao cha *caucus* baada tu ya kuakhirisha.

Waheshimiwa Wajumbe naomba niahirishe Baraza letu Tukufu mpaka kesho tarehe 23/02/2018 saa 3:00 asubuhi. Nawashukuru sana.

*(Saa 7:21 mchana Baraza liliahirishwa hadi tarehe 23/02/2018 saa 3:00 asubuhi)*